**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 11 Mei, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Kamili Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, mwongozo!

**SPIKA:** Ahsante sana. Nitakupa nafasi dakika mbili tu zijazo. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Longido. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nilisikia mwongozo, Mheshimiwa Mlinga.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilikuwa naomba mwongozo kwa busara zako.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nchi yetu iko katika kipindi cha Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, hilo moja. La pili, ni kipindi ambacho wanafunzi na watoto wetu wote wakiwa nyumbani ambapo wanakunywa sana chai na wanahitaji matunzo mazuri ili waweze kukaa nyumbani vizuri na hata hao wanaofunga muda ule wanaofungulia huwa wanatumia uji ambapo lazima watumie sukari.

Mheshimiwa Spika, lakini wote tumeshuhudia kukiwa na taharuki kubwa katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Morogoro na miji mingine ambapo kuna shida kubwa kabisa ya sukari yaani hamna na hata ikipatikana, inapatikana kwa magendo na bei kubwa lakini sisi kama Bunge hatujapata taarifa yoyote kutoka Serikalini kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kwa busara zako Serikali ituambie ni nini kinaendelea kwenye suala hili la sukari ili na sisi tuweze kuwaambia

wananchi wetu huko na wapiga kura waweze kusikia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, ushauri wangu nitautoa mwishoni mwa *session* ya leo, kwa hiyo sasa hivi tuendelee, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 240

### Kuboresha Vituo vya Afya – Korogwe

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Jiografia ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ni changamoto kwa upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wa Tarafa ya Bungu na Magoma na suluhisho ni uboreshaji wa vituo vya afya vya maeneo hayo.

(a) Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa Vituo vya Afya vya Bungu na Magoma?

(b) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi iliyoitoa kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI ya kujenga Kituo cha Afya Kerenge?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya nchini ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Kituo cha Afya kila Kata kwa awamu. Hadi sasa Serikali imekamilisha ujenzi na ukarabati wa Kituo cha Afya cha Mkumbala kilichogharimu jumla ya shilingi milioni 500. Aidha, Halmashauri hiyo pia imepokea shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri. Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya vikiwemo vya Bungu na Magoma kadri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Kerenge kimepokea shilingi milioni 200 katika mwaka wa fedha 2019/2020 na ujenzi unaendelea ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Serikali iliyotolewa kuhusu ujenzi wa kituo hicho.

Na. 241

**Hitaji la Gari la Wagongwa – Vituo vya Afya Kata za Makete**

**MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING** aliuliza:-

Je ni lini Serikali itapeleka magari ya wagonjwa kwenye Vituo vya Afya vya Kata za Mbalache, Lupila na Bulongwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Norman Adamson Sigalla, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vituo vya kutolea huduma ya afya vilivyoko Kata ya Bulongwa vinatumia gari la wagonjwa la Hospitali ya Misheni ya Bulongwa ambayo ina ubia na Serikali. Kituo cha Afya cha Lupila kina gari dogo la wagonjwa ambalo linafanya kazi vizuri. Kwa upande wa Kata ya Mbalache, Halmashauri imeingia mkataba wa huduma na Hospitali ya Misheni ya Ikonda ambapo kunapokuwa na

uhitaji wa huduma ya rufaa ya dharura, Halmashauri huwasiliana na uongozi wa hospitali ili kupata huduma. Aidha, azma ya Serikali ni kuendelea kuwezesha vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kuvipatia magari ya kuhudumia wagonjwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

Na. 242

**Uchafuzi wa Mazingira Unaofanywa na Kiwanda cha Bakhresa**

**MHE. RUTH H. MOLLEL** aliuliza:-

Kiwanda cha juisi cha Bakhresa kilichopo Vikindu, Wilaya ya Mkuranga, hutupa hovyo juisi zilizokwisha muda wake na hivyo kuhatarisha usalama wa mazingira na afya za wananchi wa maeneo hayo:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua ili kudhibiti hali hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha *Bakhresa Food Production Co. Ltd* kinachozalisha vinywaji baridi aina ya juisi na soda kimejengwa katika Mtaa wa Mwandege, Kata ya Vikindu, Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani. Aidha, eneo linalomilikiwa na kiwanda hicho ambalo linatumika kama dampo kwa ajili ya taka ngumu kutokana na shughuli za kiwanda hicho liko katika Kijiji cha Kazole, Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wakazi wa eneo hilo, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* ilifanya ukaguzi katika kiwanda husika na kubaini yafuatayo:-

(a) Hakukuwepo juisi zilizokwisha muda wake;

(b) Eneo la dampo lipo karibu na makazi ya watu na halina uzio hali inayoweza kusababisha mlipuko wa magonjwa;

(c) Mifereji inayotumika katika utiririshaji wa majitaka kuelekea katika mitambo ya kusafisha majitaka *(wastewater treatment plant)* imechakaa na kuharibika. Hali hii ni kinyume na kifungu cha 106(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004; na

(d) Wakati wa mvua majitaka hutiririka toka kwenye dampo kuelekea kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hiyo, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* imeelekeza kiwanda kufanya yafuatayo:-

(a) Kuboresha miundombinu ya majitaka ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaoweza kujitokeza;

(b) Kujenga mara moja uzio kuzunguka eneo la dampo ili kuzuia kutawanyika kwa taka na watu kuingia katika eneo hilo;

(c) Kuangalia uwezekano wa kulipa fidia kwa waliojenga karibu na eneo la dampo; na

(d) Kuwasiliana na mamlaka husika ya kutoa Kibali cha Kumwaga Majitaka Yaliyotibiwa *(Discharge Permit)* na yawe yamekidhi viwango vya mazingira vya majitaka vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Viwango vya Ubora wa Maji za mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kuhamasisha viwanda nchini kuhakikisha kuwa vinazingatia uzalishaji bora na hifadhi ya mazingira kwa faida yetu na ya vizazi vijavyo.

Na. 243

**Ujenzi wa Nyumba za Polisi Mangenya**

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB** aliuliza:-

Serikali imejenga Kituo cha Polisi cha Mangenya Wilayani Muheza lakini haikujenga nyumba za askari karibu na kituo hicho:-

Je, ni lini Serikali itajenga nyumba kwa ajili ya askari karibu na kituo hicho?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Mangenya ni kati ya Vituo vya Polisi visivyo na nyumba za kuishi askari. Aidha, Serikali ina mpango madhubuti wa kujenga nyumba za kuishi askari kwa awamu katika vituo mbalimbali hapa nchini ikiwemo Kituo cha Polisi cha Mangenya, Wilayani Muheza.

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa nyumba za kuishi askari, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inakusudia kutumia rasilimali na wataalamu wa ndani ya Wizara na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kufanikisha ujenzi wa nyumba hizo.

Na. 244

**Serikali Kulipa Madeni ya Watumishi**

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED** aliuliza:-

Kwa kipindi kirefu sasa Serikali imekuwa na madeni makubwa inayodaiwa na watumishi katika maeneo mbalimbali ya watumishi wa umma.

(a) Je, ni lini Serikali itawalipa watumishi hao madeni yao?

(b) Je, Serikali haioni aibu kuwa na madeni ya watumishi wake kwa muda mrefu?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kulipa madeni mbalimbali inayodaiwa yakiwemo madeni ya watumishi. Katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2019/2020 jumla ya shilingi billioni 375.7 zilitolewa na Serikali kugharamia madeni mbalimbali ya watumishi, ambapo kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 113.8 ni madeni ya kimshahara na shilingi bilioni 261.9 ni madeni yasiyo ya kimshahara. Hata hivyo, kufuatia changamoto ya uwepo wa madeni hewa Serikali ilizuia ulipaji wa madeni kabla ya kuhakikiwa ikiwa ni mojawapo ya mkakati wa kuleta nidhamu na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya shilingi bilioni 600 zimetengwa na kuidhinishwa na Bunge kugharamia malipo ya madeni mbalimbali ikijumuisha madeni ya watumishi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya shilingi bilioni 364.7 zimelipwa kama madai ya watumishi, wazabuni na wakandarasi ambapo kati ya hizo kiasi cha shilingi bilioni 97.6 zimelipwa kama madeni ya watumishi pekee.

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu hizo, Serikali haina sababu za kuona aibu bali inajisikia fahari na inahitaji kupongezwa kutokana na juhudi mbalimbali inazochukua katika kuhakikisha madeni yote ya watumishi yanalipwa pale tu yanapothibitika kwamba ni halali.

Na. 245

**Kuanzishwa Mkoa wa Kitanesco Mbagala**

**MHE. ISSA A. MANGUNGU** aliuliza:-

Jimbo la Mbagala lina wakazi zaidi ya 800,000, *TANESCO* Wilaya ya Mbagala ina wateja zaidi ya 400,000 mara nne zaidi ya baadhi ya Mikoa ya KITANESCO:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha Mkoa wa *TANESCO* Mbagala ili kukabiliana na changamoto za umeme zilizopo na kuongeza ufanisi?

(b) Ni lini usambazaji wa umeme utakamilika katika maeneo ya Kilimahewa, Changanyikeni, Vikunai – Kata ya Tuangoma, Mponda, Vigozi, Churuvi - Kata ya Mianzini?

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Ofisi ya *TANESCO,* Wilaya ya Mbagala ipo katika Mkoa wa *TANESCO* Temeke. Kiutendaji, *TANESCO* Wilaya ya Mbagala inahudumia Kata tisa (9) zenye mitaa 56 katika maeneo ya Chamazi, Charambe, Kibondemaji, Kiburugwa, Kijichi, Kilungule, Mianzini, Mbagala, Mbagala Kuu na maeneo ya Kongowe Mzinga. Kata za Tuangoma na Mianzini zinahudumiwa na Ofisi za *TANESCO* za Wilaya ya Kigamboni na Mkuranga. Jimbo la Mbagala lina wateja 64,501 wanaohudumiwa na njia za kusambaza umeme zenye urefu wa kilomita 1,469.01 kupitia transfoma 301 katika maeneo mbalimbali ya Kata hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza gharama za uendeshaji wa Shirika na kuimarisha huduma kwa wateja, Jimbo la Mbagala litaendelea kuhudumiwa na Ofisi za *TANESCO* za Wilaya za Kigamboni, Mkuranga na Mbagala.

Kwa sasa, hali ya upatikanaji wa umeme katika maeneo ya Mbagala imezidi kuimarika baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme cha Mbagala cha msongo wa kilovoti 132/33 chenye uwezo wa *MVA* 50 ambacho kilizinduliwa tarehe 22 Februari, 2018.

(b) Kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika maeneo ya Kilimahewa, Changanyikeni, Vikunai Kata ya Tuangoma na maeneo ya Mponda, Vigozi, Churuvi, Kata ya Mianzini ilikamilika kati ya Oktoba, 2018 na Mei, 2019. Aidha, kukamilika kwa utekelezaji wa miradi hii kumesaidia kuimarika kwa hali ya upatikanaji umeme katika maeneo ya Jimbo la Mbagala.

Na. 246

**Ujenzi wa Ukuta wa Bahari Ruvula**

**MHE. HAWA A. GHASIA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga ukuta wa bahari *(sea wall)* wa Ruvula Mtwara ili kuvilinda visima vya gesi vya Mnazi bay?

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la mmomonyoko wa ardhi katika ufukwe wa Mnazi Bay lilitokea kwa mara ya kwanza Januari, 2015 baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha mawimbi makali ya bahari ambayo yalisomba kipande cha ufukwe chenye upana wa takribani mita mia moja (100m). Katika hatua za muda mfupi za kutatua tatizo hilo, Serikali kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mtwara ilijaza mawe katika eneo hilo kwa lengo la kudhibiti mmomonyoko huo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017, Serikali kupitia *TPDC* kwa kushirikiana na Kampuni ya Maurel & Prom (M&P) ilifanya utafiti wa kina katika eneo hilo. Lengo ni Serikali kupata mapendekezo na ushauri wa kitaalam kuhusu namna bora ya kuimarisha ufukwe huo. Aidha, taarifa za awali za utafiti zinapendekeza kujengwa ukuta wa mawe kukinga mawimbi yasielekee upande wa bomba na mtambo wa kuchakata gesi asilia ya Mnazi Bay.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha uchambuzi wa taarifa ya utafiti huo na kazi za kudhibiti mmomonyoko huo zinategemea kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Na. 247

**Hitaji la Maji Jimbo la Singida Kaskazini**

**MHE. JUSTIN J. MONKO** aliuliza:-

Jimbo la Singida Kaskazini linakabiliwa na shida kubwa ya majisafi na salama kwa ajili ya matumizi ya wananchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma ya maji katika Vijiji vya Ng'ongoampoku, Mwalala, Lamba, Mughunga na Endesh?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/ 2020, Serikali ilipanga kutekeleza uchimbaji wa visima virefu saba katika vijiji vya Misinko, Ughandi 'B', Mitula, Migugu, Mwighanji, N'gongoampoku na Mwalala. Visima vitano (5) vimekamilika katika vijiji vya Misinko, Ughandi 'B', Mitula, Migugu na Mwighanji. Kwa sasa, kazi ya uchimbaji inaendelea katika kijiji cha Mwalala na N'gongoampoku, kazi

hii inafanywa na Kitengo cha Uchimbaji wa Visima chini ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(RUWASA).*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kero ya maji wanayoipata wananchi wa Wilaya ya Singida Kaskazini, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021, Serikali itatekeleza mradi wa kisima, uchimbaji na usambazaji wa maji katika vijiji vya Lamba, Kinyamwenda, Msikii na Sekotoure. Pia, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo (*World Serve International*) inatarajia kuchimba visima viwili (2) katika vijiji vya Mughunga na Endeshi katika mwaka wa fedha wa 2020/2021. Kutekelezwa kwa mipango hii kutawezesha utatuzi na kero ya maji kwa kiasi kikubwa katika Jimbo la Singida Kaskazini.

Na. 248

### Uzinduzi wa *VIP* kwa Wageni Wanaopanda Mlima Kilimanjaro

**MHE. ESTER M. MMASI** aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Old Moshi Mashariki kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakingoja uzinduzi wa njia ya *VIP* kwa wageni waendao kupanda Mlima Kilimanjaro.

Je, kwa nini Serikali isione umuhimu wa kutekeleza azma hiyo iliyodumu kwa muda mrefu sasa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* ilishaona umuhimu wa kufungua njia ya Kidia itakayotumika kwa wageni maarufu *(VIP)* watakaokuwa wanapanda Mlima Kilimanjaro. Kutokana na umuhimu wa njia hiyo, Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)*

limeiweka kwenye Mpango wa Jumla wa Usimamizi wa Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro *(General Management Plan – GMP)* wa mwaka 2016 - 2026.

Mheshimiwa Spika, katika maandalizi ya kufungua njia hiyo, jumla ya shilingi milioni 200 zimetengwa kwa mwaka 2019/2020, kwa ajili ya kufungua njia ya wageni ya Kidia yenye urefu wa kilometa 25 ambapo kwa sasa kazi inaendelea. Pia, shilingi milioni 230 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya kupokea na kuhudumia wageni, lango pamoja na kutengeneza njia *(trail)* ya kupandia mlima kuanzia Kidia. Kuzinduliwa kwa njia hiyo, kutaongeza mapato ya Serikali kupitia utalii, lakini pia kutaongeza fursa kwa wananchi wa Kata ya Old Moshi Mashariki kufanya biashara kwa watalii, mawakala wa utalii na watoa huduma ya utalii watakaokuwa wanatumia njia hiyo.

Na. 249

**Kurasimisha Matumizi ya Dawa aina ya *Misoprostol***

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

*Misoprostol* ni dawa ambayo inatumika kwa ajili ya matatizo ya akina mama:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurasimisha matumizi ya dawa hii?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeendelea kusimamia utekelezaji wa juhudi mbalimbali za kuboresha huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto ikiwemo upatikanaji wa

dawa muhimu ikiwa na lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesharasimisha matumizi sahihi ya Misoprostol kwa kuandaa mwongozo ambao umeanza kutumika nchini mwezi Julai 2019 juu ya matumizi bora ya dawa muhimu kwa wajawazito wakati na baada ya kujifungua *"Clinical Practice Guidelines on Appropriate Use of Uterotonics*", ili kuendana na lengo hilo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga nchini. Katika mwongozo huu, mojawapo ya dawa iliyoanishwa ni matumizi ya Misoprostol ambapo dawa hii ni ya mstari wa tatu *(third line),* dawa aina ya *Oxytocin* ikianza, ikifuatiwa na dawa aina *Ergometrine* halafu ndio dawa ya Misoprostol. Matumizi ya dawa ya Misoprostol ni kwa ajili ya kutoa huduma muhimu baada ya mimba kuharibika, kuanzisha uchungu kwa wajawazito ambao wamepitiliza muda wao wa kujifungua na kukinga na kutibu utokaji wa damu nyingi baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwataka watoa huduma wote wa afya nchini kutumia mwongozo huu ili kuwezesha kuboresha huduma za afya ya uzazi. Kwa pamoja tunaweza kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

**SPIKA:** Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa ajili ya kuokoa muda moja kwa moja sasa nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa William Lukuvi. Mheshimiwa Waziri karibu uwasilishe hoja yako, tafadhali.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hi. Kama ilivyo ada napenda kutoa hoja mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayohusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu 48 na Fungu 3 la Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya mwaka 2019/2020. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Bajeti ya Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema.

Aidha, kufuatia kifo cha Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Newala Vijijini kilichotokea mwezi Januari mwaka huu, Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kilichotokea mwezi Aprili mwaka huu, Mheshimiwa Richard Mganda Ndassa aliyekuwa Mbunge wa Sumve kilichotokea mwezi Aprili mwaka huu na Balozi Dkt. Augustino Philip Mahiga aliyekuwa Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria kilichotokea mwezi Mei mwaka huu, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kutoa pole kwako wewe binafsi, Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu, jamaa na wananchi walioguswa na misiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile natoa pole kwa wananchi wote walioathirika kwa namna moja au nyingine na majanga yaliyotokea katika maeneo mbalimbali nchini hususani mafuriko na mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa virusi vya aina ya *corona (COVID 19)*. Tunawaombea marehemu wote kwa Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza sana kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi makini katika kusimamia rasilimali za Taifa, kupambana na rushwa na kuimarisha nidhamu ya uwajibikaji katika Utumishi wa Umma. Katika Awamu ya Tano tumeshuhudia mageuzi makubwa ndani ya Sekta ya Ardhi, kuimarika kwa nidhamu ya Watendaji wa sekta yangu ya ardhi na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kitaifa ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kati ya miradi hiyo mingi lakini michache ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania, ujenzi wa bwawa la uzalishaji wa umeme la Julius Nyerere na ujenzi wa bomba la mafuta ghafi ambalo litajengwa kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga na viwanda na miradi mingi mingine ambayo inatarajiwa kuleta manufaa makubwa kiuchumi na kijamii kwa Watanzania. Hakika uongozi wake mahiri umeendelea kuijengea heshima kubwa nchi yetu Kitaifa na Kimataifa, nasi Wizara ya Ardhi tunajivunia. Bila maono na uongozi wake Mheshimiwa Rais tusingefanikiwa kujenga nidhamu kama nilivyofanikiwa katika Wizara hii ya Ardhi kwa kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Mheshimiwa Samia Suhuhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali. Napenda kuwashukuru kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Vilevile nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uongozi imara katika kusimamia maslahi na ustawi wa wananchi wa Tanzania Zanzibar na kuendelea kudumisha misingi ya muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda bila aibu kukupongeza sana wewe, binafsi kwa kazi kubwa na usimamizi wa kizalendo wa Bunge lako Tukufu. Wewe ni kisiki cha mpingo kama walivyosema Wamakonde, pamoja na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Ackson Mwansasu Mbunge kwa kuongoza na kusimamia kwa umahiri shughuli za Bunge letu. Vilevile nawapongeza Wenyeviti wote wa Bunge waliopita na waliopo ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakisimamia na kuongoza shughuli za Bunge kwa ufanisi, tunawaombea Mwenyezi Mungu aendelee sana kuwajalia afya njema na hekima katika kuwatumikia wananchi na *insha Allah* Mwenyezi wajalie ili tukutane tena Bunge lijalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibwakwe kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi; Mheshimiwa Iddi Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala kwa kuteulia kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira; na Mheshimiwa Dkt. Mwiguku Lameck Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria tunawatakia kheri katika utekelezaji wa majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imeelezea utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2019/2020 na mwelekeo wa shughuli za Serikali zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/ 2021. Wizara yangu imezingatia na itatekeleza maelekezo na maagizo yanahusu Sekta ya Ardhi ili kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali yanatimizwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mwenyekiti Kemilembe Rose Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia kwa kipindi chote pamoja na ushauri wao ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pia nawashukuru

Wajumbe wote wa Kamati kwa uchambuzi makini walioufanya na ushauri walioutoa wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi Fungu 48 na Fungu namba 3 ambayo yote yako ndani Wizara ya Ardhi kwa mwaka huu 2020/2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha nawashukuru kwa maoni na ushauri walioutoa wakati wa kusimamia shughuli zinazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake kwa kipindi chote cha Serikali ya Awamu ya Tano. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba maoni ya Kamati yetu, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii na kutoa mwelekeo mpya wa mabadiliko katika Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru Wenyeviti na wajumbe wote ambao nimefanya nao kazi katika miaka hii mitano ambayo sasa wanatumikia Kamati nyingine. Mwenyekiti wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Mwanjwelwa na Mwenyekiti wangu mwingine alikuwa Mheshimiwa Nape; nawashukuru sana kwa usimamizi katika miaka hii mitano ambayo tumefanya kazi pamoja. Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Ismani kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, nawapongeza kwa juhudi wanazozifanya katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kujiletea maendeleo yao binafsi pamoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie hali ya Sekta ya Ardhi nchini. Sekta hii ni sekta wezeshi na mtambua na imeendelea kuimarika na kuchangia katika maendeleo ya wananchi, kukuza pato la Taifa, kuchochea uwekezaji na uzalishaji mali katika Sekta za Kilimo, Viwanda, Ujenzi, Mifugo, Uvuvi, Maliasili, Nishati, Madini, Miundombinu na hivyo kuongeza ajira na pia kuwezesha Serikali kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za Sekta ya Ardhi na mapato mengine yanayokusanywa na vyombo vingine vya Serikali ambavyo ni wadau na watumiaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, Mwelekeo wa Sekta ya Ardhi; hotuba yangu ninayowasilisha hii ni ya tano tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani. Aidha, Wizara yangu inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2020 - 2025; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 - 2020/2021; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015; hotuba ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli wakati wa kuzindua Bunge la Kumi na Moja, mwezi Novemba, 2015; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi ulioasisiwa mwaka 2013 na utaisha mwaka 2033; Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000; pamoja na Sheria na Miongozo mbalimbali iliyotolewa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba nitoe kwa ufupi mafanikio ya Sekta ya Ardhi na baadhi ya kazi zilizofanya zihusuzo utatuzi wa migogoro, upangaji, upimaji ardhi na ukusanyaji wa mapato na hotuba yangu yote ambayo ina ukurasa 202 inapatikana kwenye mtandao wa Wizara yaani *www.lands.go.tz* na kwenye *tablets* za Waheshimiwa Wabunge wote, kitabu hiki chote kiko ndani ya mtandao wenu na pia kipo kwenye mtandao wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, zoezi la Usimamizi na Upangaji na Umilikishaji wa Ardhi uligubikwa na kero nyingi za kiutendaji na urasimu, Wizara yangu imetekeleza kwa vitendo maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kuwaondolea kero wananchi kwa kutekeleza mikakati mbalimbali:-

(i) kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Serikali iliunda Kamati ya Mawaziri nane na baadaye Baraza la Mawaziri liliamua Vijiji 920 kati ya 975 vilivyokuwa kwenye hifadhi mbalimbali vipimwe na vibaki katika maeneo yao;

(ii) Serikali iliamua kufuta mapori tengefu 12 yenye ukubwa wa ekari laki 707,659.4 na misitu ya hifadhi saba yenye ukubwa wa ekari 46,715 ili ardhi hiyo ipangwe na kupimwa na kugawiwa kwa vijiji na iandaliwe matumizi bora ya ardhi.

(iii) Serikali imeagiza kumegwa kwa hifadhi 14 zilizopo za misitu ili ardhi hiyo itumike kwa shughuli za ufugaji na kilimo.

Mheshimiwa Spika, kazi hizi za utekelezaji zinaendelea na Wizara mbalimbali zinazohusika zimepanga bajeti za kukamilisha zoezi hili la upangaji wa ardhi katika maeneo haya ya vijiji. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuhimiza na kuamua jambo hili ambalo limekuwa zito kwa wananchi hasa maskini wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia program ya Funguka kwa Waziri pia ilishughulikia migogoro 15,808 nchi nzima kwa njia ya kiutawala, katika halmashauri mbalimbali nchini. Mimi na Naibu wangu tumekuwa tunatembea mikoani na wilayani kusikiliza kero za wananchi ambazo kwa kiasi kikubwa siku za nyuma viongozi wengi wa Serikali walikuwa hawasikilizi kero hizi za wananchi, lakini nafurahi kwamba baada ya uchokozi huu sasa viongozi wa Mikoa, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na viongozi wengine wa halmashauri wako sambamba na sisi kuhakikisha kwamba wanatokomeza migogoro hii kwa kusikiliza na kwenda kusikiliza migogoro hii kwa wananchi. Nawashukuru sana viongozi wa Mikoa nao kwa kujitolea muda wao kufanya kazi hii. Aidha, jumla ya migogoro mingine laki 131,603 ya matumizi ya ardhi imetatuliwa sasa kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika miaka mitano yaani kupitia Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote wananchi waliopima na kulipia gharama za kupata Hati Miliki walitakiwa kuzifuata hizo kwenye Kanda kwa gharama zao wenyewe. Mwanzo kabisa kila mwananchi aliyekuwa amelipia hati alikuwa anaifuata Dar es Salaam, lakini baadaye wakaanza kuzifuata Dodoma na Dar es Salaam, baadaye wananchi wote nchi nzima wakawa wanafuata hati katika Kanda nane zilizokuwepo na hivyo kulifanya suala la umilikishaji ardhi wananchi kwa Hati Miliki kukosa mvuto na kasi kwani gharama ya usumbufu kwa kufuatilia hati katika mikoa mbalimbali ni kubwa maradufu kuliko gharama za kisheria za upatikanaji wa Hati Miliki.

Mheshimiwa Spika, aidha halmashauri za Wilaya zilikuwa zinatumia mamilioni ya pesa kila mwaka kwa kuwatuma vijana wataalam wa ardhi wa mipango miji, upimaji, uthamini na ardhi kupeleka nyaraka na ramani, michoro, hati, kwenye Kanda za Mikoa ya mbali ili kupata idhini au sahihi pamoja na usajili kwenye Kanda za Wizara ya Ardhi. Hata mabenki pia yalipunguza kasi ya ukopeshaji kwani walitakiwa kwenda kupekua taarifa za zamani yaani zile hati za wakopeshwaji kwenye Kanda jambo ambalo liliongeza gharama za uendeshaji na usumbufu na kwa hiyo wananchi walishindwa kupata haki yao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kero hizo sasa tumezimaliza, awamu hii tumetoa majibu sahihi na ya kudumu ambayo yatarahisisha utendaji na utoaji wa huduma kwa Sekta ya Ardhi na kuleta nafuu kwa wananchi hasa walioko mikoani na pia itaimarisha amani utulivu kwa wananchi na kuimarisha uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi huu Wizara imeanzisha rasmi nataka kutoa taarifa kwa wananchi wanaosikiliza kupitia Bunge lako kwamba, Wizara imeanzisha rasmi Ofisi za Ardhi katika kila Mkoa ambazo zitatoa huduma zote zilizokuwa zinatolewa kwenye Kanda nane tu au Makao Makuu Dar es Salaam na Dodoma. Hivyo basi, kuanzia mwezi huu wa Mei wananchi watapata huduma zote ndani ya mikoa yao husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huduma tulizokuwa tunazitoa zamani ili mwananchi aweze kupata Hati Miliki ilikuwa kwamba lazima ardhi hiyo ipangwe ipimwe. Kwa hiyo, kuna michoro ambayo ilikuwa inatoka wilayani kwenda kwenye Kanda, kwa hiyo watendaji lazima waende kupeleka michoro ya upimaji, upangaji, wapeleke tena michoro ya upimaji, wapeleke na hati. Kwa hiyo halmashauri zilikuwa zinaingia gharama kubwa sana kuwatuma hawa vijana na vijana hawa wa ardhi walikuwa wajanja, walikuwa wanatumia nafasi hiyo kuchukua fedha nyingi kwa kisingizo kwamba wanapeleka michoro au hati kwenye Kanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kazi hiyo sasa kazi zote zilizokuwa zinafanywa, uidhinishaji wa michoro ya mipango miji, uidhinishaji wa michoro ya upimaji, uidhinishaji wa Taarifa mbalimbali za uthamini ili kila mwananchi aweze kuuza nyumba yake au shamba. Ilitakiwa lazima afanyiwe utathmini na tathmini hiyo iende kwa *Chief Valuer* hapa Dodoma. Imecheleweshwa sana lakini kwa sasa uidhinishaji wa taarifa zote za uthamini utafanyika kwenye Mikoa yote 26. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara yangu imeshateua hivi sasa, imeshateua Watendaji wote wanaoongozwa na Kamishna Msaidizi. Kila Mkoa tumempeleka Kamishna Msaidizi ambaye atakuwa anafanya kazi kwa niaba ya Kamishna. Kazi zote za upitishaji wa Ardhi atafanya. Lakini pia kila Mkoa tumeshampeleka Msajili wa Hati. Lakini kila Mkoa tumerudisha nyaraka zote ambazo zina historia ya mkoa husika zilizokuwa kwenye Mikoa mingine. Tangu kabla ya uhuru na baada ya uhuru, tumezirudisha kwenye Mkoa husika *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini, kila mwananchi anayemiliki Hati Nchi hii huwa anapata Hati mbili, yeye anapata moja na moja inabaki kwenye Ofisi ya Usajili. Hati hizi mlizokuwa nazo zilikuwa zinatunzwa kwenye Kanda 8 tu. Kwa hiyo rekodi zenu zote zilizokuwa zinamilikisha wananchi au rekodi za wananchi wa kila mkoa, sasa zimerudishwa kwenye mkoa husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa zote za kijiografia za upimaji, upangaji, uthamini, na nyaraka zote pamoja na Hati zimesharudishwa kwenye mikoa husika. Na kwa kukamilisha hilo, kisheria nilitakiwa nitoe tangazo kama lifuatalo; kwamba nilitaka kutoa taarifa kwenye Bunge lako kwamba zoezi hili nimelikamilisha kisheria kwa Mamlaka niliyonayo chini ya fungu la 3(1) cha sheria ya usajili wa ardhi sura ya 334 nimetoa tamko la kuanzisha Masjala za kusajili Hati Miliki na miamala yake katika mikoa yote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni *order* ya mwaka 2020 ambalo limetangazwa tayari katika gazeti la Serikali toleo la tarehe 8

mwezi huu wa tano, mwaka wa 2020 kama taarifa na limepewa namba ya GN 308. Kwa hiyo haya ninayoyasema tayari yapo kisheria na kazi hizi sasa zinaweza zikafanyika Mikoani kisheria.

Mheshimiwa Spika, lengo la tangazo hili ni utekelezaji wa adhma ya Wizara ya kuanzisha Ofisi za Ardhi katika Mikoa ili kuwezesha utoaji wa huduma ya Sekta ya Ardhi ikiwemo usajili wa Hati Miliki na Miamala katika kila mkoa, nchini kote ambazo awali huduma hizi zilikuwa zikitolewa katika Ofisi za Kanda. Hatua hii inawasogezea huduma wananchi na hivyo kuwaondolea usumbufu.

Mheshimiwa Spika, maana yake nini, sasa Wananchi wa Mikoa ya Kigoma na Katavi waliokuwa wanakwenda kuchukua Hati binafsi Tabora. Sasa basi Hati zao watazipata pale pale Kigoma. Wananchi wa Mikoa ya Tanga, Manyara na Arusha wote walikuwa wanatakiwa waende Moshi kufuata Hati zao hata kama wameshalipia gharama zote kwenye Mikoa yao. Sasa basi Hati zao watachukulia ndani ya Mikoa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Mikoa ya Iringa, Njombe na Rukwa wasiende tena Mbeya kwasababu shughuli zilizokuwa zinafanywa Mbeya sasa zinafanywa kwenye Mikoa yao.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Ruvuma na Lindi wasiende Mtwara tena, kwasababu shughuli zote sasa zimeshahamishiwa na wataalamu wote na vifaa vyote tumewapelekea hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Mkoa wa Kagera walikuwa wanatakiwa kuvuka Ziwa Victoria na Geita kwenda Mwanza, basi sasa watachukulia kila kitu ndani ya Mikoa yao. Wananchi wa Mikoa ya Mara na Shinyanga wasiende Simiyu, watapata huduma zao katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya hapo, ni kwamba wananchi kwa utaratibu wa Sheria anatakiwa kulipia

gharama zote za Hati kwa Afisa Ardhi wa Wilaya hata kwa utaratibu huu kisheria mwananchi anatakiwa akachukue Hati yake Mkoani, nalo nimelirekebisha. Mwananchi akilipia Hati kwenye Wilaya yoyote ya Tanzania Msajili wa Hati atakwenda kutoa Hati kwenye Wilaya, mwananchi hatakwenda mkoani. Kwa hiyo, kila mwananchi atakayelipia Hati kwenye Wilaya yoyote ndani ya nchi hii, ahakikishe kwamba anapewa Hati ndani ya Wilaya ile wala asiende hata Mkoani kuchukua Hati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, shughuli za utoaji wa Hati kwa Wananchi zitarudishwa Wilayani, kwa hiyo watasajili Mkoani, nyaraka zitatunzwa Mkoani lakini Mwananchi atapewa Hati zake Mkoani. Kwa hiyo, Mikoa ambayo ilikuwa na Kanda kama Mkoa wa Dodoma kwa Mheshimiwa Spika sasa walikuwa wamebanwa sana wanahudumia na Singida sasa watahudumia Mkoa wa Dodoma peke yake.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kilimanjaro utahudumia Mkoa wa Kilimanjaro peke yake. Kanda iliyokuwa Mbeya itahudumia Mkoa wa Mbeya peke yake. Kwa hiyo, wananchi nataka niwape matumaini kwamba, mpango huu utarahisisha sana uendeshaji wa shughuli za Ardhi pia kwa janga hili pia vilevile itaondoa msongamano na adha ya kupanda mabasi kutoka Babati kwenda Moshi kufuata Hati. Sasa hakuna sababu ya kusongamana kwenda Moshi kufuata Hati kwasababu Hati utazipata hapo hapo Babati.

Mheshimiwa Spika, hili ni tangazo muhimu kwa uchumi wa nchi hii, kwasababu tunajua sasa hata Benki hawatakuwa na haja ya kwenda kwenye Kanda za mbali kwenda kupekua dhamana za wakopaji wakati Hati na Masjala ziko Mkoani. Itapunguza gharama na ukopeshaji utakuwa kwa rahisi zaidi kwa Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nyaraka zote, watumishi na vitendea kazi vyote viko Mikoani hivi sasa. Taasisi kama Mabenki sasa watakopesha kwa kasi kwani dhamana za wakopeshwaji yaani Hati ziko Mkoani na Masjala za Hati zimerudishwa kila Mkoa. Wasajili wa Hati wa Mikoa watatoa

Hati kwa Wananchi kupitia ofisi za Ardhi za Wilaya na sio Wananchi kufuata Hati kwenye Kanda au Mkoani.

Mheshimiwa Spika, aidha vifaa mbalimbali vya upimaji, ambavyo halmashauri mbalimbali walikuwa wanakodisha kifaa kinaitwa *RPK* kwa shilingi laki mbili na nusu, sasa tumevinunua na tumevigawa Mikoani. Kwa hiyo halmashauri zote zinatakiwa kwenda kuazima Mkoani bila kugharamia fedha zozote na kutumia wataalamu waliopo ndani ya Mkoa kwenda kutoa usimamizi wa kazi katika Wilaya husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo vifaa tumepeleka pamoja na Masjala lakini na vifaa vya upimaji tunapeleka. Na kuanzia mwezi huu tutaanza kuongeza vifaa vingine katika baadhi ya mikoa.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Ofisi hizi ni utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli aliyetutaka Wizara ya Ardhi tuondoe kero na mzigo wa gharama kwa wananchi na wadau mbalimbali. Lakini pia utekelezaji wa mpango huu wa *COVID 19* wa kupunguza maambukizi ya Corona kwa kuondoa msongamano na ulazima wa wananchi kusafiri safari kwenda kufuata Hati zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunataraji wananchi sasa watamiliki ardhi zao, watatumia ardhi kwa faida kwasababu Serikali sasa imeondoa kero zote zilizokuwapo katika kipindi chote cha uhai wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pia mmekuwa mkilalamikia gharama za umilikishaji na urasimishaji. Sasa tumetoa majibu ya kero hii, kwasababu warasimishaji wote sekta binafsi walikuwa wanaweka gharama kwa wananchi zile gharama za kufuata huduma ya uidhinishaji wa michoro yao kwenye Kanda, walikuwa wanawabambikia wananchi. Halmashauri nazo zilikuwa zinaweka gharama wanazitumia kuwatuma wale vijana kwenda kwenye Kanda kupitisha michoro kwa gharama ya wananchi. Kwa hiyo, naamini sasa suluhisho hili litapunguza

hata gharama za umilikishaji kwa Wananchi maskini ili kila mmoja apate haki ya kumiliki ardhi yake.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Sekta ya Ardhi. Ambayo yameongezeka kutoka bilioni 54.55 katika mwaka wa fedha ulioishia Awamu ya Nne 2014/2015 hadi leo tunavyozungumza kabla hatujafikia mwisho wa mwaka huu wa fedha tumeshakusanya bilioni 84.5 lakini tunavyoelekea tunaweza tukazidi tukafikia lengo la juu zaidi. Na tunaendelea kwa kasi kufikia malengo tuliyojiwekea katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, lakini aidha ukusanyaji wa kodi vilevile umerahisishwa sasa wananchi wanaweza wakalipia pango la ardhi au kodi mbalimbali zitokanazo na ardhi kwa kupitia njia ya *electronic* au kupitia simu za viganjani wakiwa majumbani.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usalama wa miliki za ardhi kwa Wananchi hadi kufikia tarehe 30 mwezi wa nne mwaka huu jumla ya Vijiji vilivyopimwa na kupewa Vyeti vya Ardhi katika nchi hii ni Vijiji 11,743 kati ya Vijiji tulivyonavyo 12,319 hii ni zaidi ya asilimia 90. Kwa hiyo, Vijiji vilivyobaki tutakamilisha hii kazi na kuvipa Vyeti vya Ardhi.

(ii) Idadi ya Hati Miliki za Kimila zilizotolewa ndani ya miaka mitano zimefikia 375,259. Na katika Hati hizi jumla ya Hati 1,516 zimetumika kama rehani ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 61.3 kwenye Taasisi za Fedha. Kwa hiyo, nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge waliokuwa na mashaka kwamba Hati za Kimila zinakataliwa na Benki, hapana Benki zimeweza kukopesha shilingi bilioni 61.3 kwa kutumia dhamana ya Hati za Kimila.

(iii) Kwa kipindi cha miaka mitano Wizara imeratibu uandaaji wa utoaji wa Hati Miliki 195,170, majedwali yote yapo ndani ya vitabu vyenu. Na Hati za umiliki wa sehemu ya jengo yaani *unit titles* 3,522. Waheshimiwa Wabunge mlipitisha Sheria hapa sasa mtu anaweza akamiliki nyumba

hata juu ya ghorofa ukapewa hati yako. Hizi *unit titles* zimetolewa 3,522 katika halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano Kamati ya Taifa ya ugawaji wa Ardhi ilipokea na kuidhinisha jumla ya maombi 527 ya umilikishaji ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

(iv) Kwa kipindi cha miaka mitano Wizara yangu iliidhinisha taarifa ya uthamini wa kawaida wa mali 52,645 na uthamini wa fidia wa mali zipatazo 84,223 jedwali linaoonyesha. Lakini katika kipindi hicho wizara imeshiriki kufanya uthamini wa mali katika maeneo ya miradi mikubwa ya kitaifa na ya kimkakati. Katika miradi hiyo majedwali matatu ya fidia yenye jumla ya fidia 9,881 na fidia ya mali kiasi cha shilingi bilioni 113.9 yaliandaliwa na kuidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uimarishwaji wa mipaka ya kimataifa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina mipaka 10 ya kimataifa yenye urefu upatao wa kilometa 1,841 katika eneo la nchi kavu na kilometa 2,086 katika maji. Jumla ya kilometa 329.9 za mipaka ya nchi kavu zimehakikiwa ambapo Awamu ya Tano pekee tumehakiki kilometa 172 na kujenga alama ndogo za kati 973, alama kuu 67 na kukarabati alama kuu za zamani 95 na za mpaka wa nchi kavu kwa Tanzania na Kenya na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, upangaji wa miji na makazi, Wizara imetangaza maeneo 75 kutoka Mamlaka za upangaji. Maeneo hayo yamepandishwa kutoka hadhi ya Vijiji na kuwa maeneo ya Mipangomiji yanaendelea kuandaliwa mipango kina.

Mheshimiwa Spika, wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji iliratibu uandaaji na kuidhinisha mipango kabambe 24 katika Miji saba (7) na Manispaa 13 na Majiji manne (4) ikiwepo Dar es Salaam na Dodoma. Katika kuunga mkono dhana ya Tanzania ya viwanda jumla ya ekari 284,349.7 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda katika miji mbalimbali nchini. Wizara pia ilipokea na kuidhinisha

michoro ya Mipangomiji 6,143 yenye jumla ya viwanja 1,456,548.

Mheshimiwa Spika, lengo la urasimishaji ni kuhakikisha usalama wa miliki na kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili huduma za kijamii, miundombinu kwa njia shirikishi. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara ilidhinisha michoro ya Mipango miji ya urasimishaji kwa maeneo ya maskini ambao walijenga bila vibali viwanja 703,836 katika halmashauri mbalimbali vijijini. Katika hilo Sekta binafsi tumeshirikiana nao wapimaji na wapangaji binafsi wao walishiriki kupima viwanja 419,240.

Katika kipindi cha miaka mitano Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewezesha upatikanani wa Mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kama ifuatavyo:-

(i) Mikopo midogo midogo ya ujenzi wa nyumba kutoka Taasisi za fedha kiasi cha shilingi bilioni 29.87, ilitolewa kwa wananchi 1914;

(ii) Benki za Biashara zinazotoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zimeongezeka kutoka tatu zilizokuwepo miaka ya 2015 hadi 34 sasa ambapo mikopo ya nyumba yenye thamani ya shilingi bilioni 438.58 imetolewa kwa wananchi 5460;

(iii) Kiwango cha riba cha ya mikopo ya ujenzi wa nyumba katika taasisi za fedha kimeshuka kutoka kati ya asilimia 21 hadi 23 mwaka 2015 hadi sasa kufikia kati ya asilimia 13 hadi 18, muda wa kurejesha mikopo midogo midogo umeongezwa kutoka miaka mitano ambayo ilikuwa wanapewa mwaka 2015 sasa wanapewa miaka 10.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali pia imeridhia ongezeko la kiwango cha mkopo kwa mikopo ya watumishi wa Serikali kutoka milioni 20 mpaka milioni 40 na shilingi bilioni 2.13 zimeshatolewa kwa watumishi 121, watumishi wa Serikali ambao wamekopeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa *land tenure support program* ambao umetekelezwa katika Mkoa wa Morogoro kama kielelezo cha mwanzo umeweza kutoa Hati za Kimila 182,126 katika Wilaya ya Kilombero, Ulanga na Malinyi. Hii ni kazi ya awali ya mfano tumeifanya tumefanikiwa sasa katika bajeti hii mtakayoidhinisha mpango huu, tuna mpango wa kueneza sasa mwaka ujao wa fedha tumepata fedha kwa kushirikiana na wadau wa Benki ya Dunia na Korea tutatekeleza mpango huu wa kupanga na kupima kila kipande cha ardhi nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, tumeimarisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kwa kusanifu na kutengeneza mfumo unganishi wa *electronic* wa taarifa za ardhi. Kwa mara ya kwanza tumejenga Kituo cha Taifa cha Taarifa ya Ardhi, taarifa zote za ardhi sasa zinaingia kwenye kituo kile cha taifa za ardhi. Tumenunua vifaa vya kisasa vya upimaji wa ardhi na tulivisambaza kwenye Ofisi zote za Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano hii tumeanza kuhama kutoka analogia kwenda kwenye eneo la *digital*, wale watu wa Dar es Salaam watajua sasa badala ya kupata Hati zile za makarasi makubwa sasa tumeanza kutoa Hati ya karatasi moja na tuna mpango sasa mwakani kwa kuanzia Dodoma tumeanza kutengeneza mfumo wetu kwa kutumia vijana wazalendo, tutaanza kutekeleza mpango huu Dodoma na mwakani katika bajeti mtakayotupa tunaanzisha mpango mkubwa wa kuhama kutoka analogia kwenda *digital* nchi zima pamoja na kujenga ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano hii Serikali imewezesha kuundwa kwa kusimikwa kwa mfumo wa *iLMS* katika Mkoa wa Dar es Salaam. Jumla ya kumbukumbu ya majalada 728,370 za usajili wa Hati, upimaji umilikishwaji wa ardhi yamebadilishwa kutoka mfumo wa analogia kuwa ki-*digital*. Viwanja 239,317viliingizwa kwenye mfumo *iLMS***.** Lakini jumla ya miamala 258,044 ilipitia mfumo wa *iLMS* ambao sasa utakwenda nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza usalama wamiliki nchini kuboresha makazi Wizara imebuni miradi miwili katika bajeti hii tunayoombea fedha leo. Ambayo inatarajiwa kutekelezwa kuanzia mwaka fedha 2021 miradi hiyo ni mradi wa kuboresha miliki utakaotekelezwa na Serikali kwa kushikirikana na Benki ya Dunia. Mradi huu una lengo la kupanga, kupima na kusajili miliki milioni mbili na nusu nchi nzima, na kupanga na kupima kila kipande cha ardhi nchi zima huu mradi uko kwenye bajeti hii. Kuboresha mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za ardhi, ujenzi wa ofisi za ardhi na mikoa na halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ni mengi, kupitia Shirika la Nyumba kwa mara ya kwanza *National Housing* imeanza kuaminika kujenga hata majengo makubwa ya Taasisi za Umma. Hivi sasa *National Housing* inajenga machinjio ya kisasa Ilala - Vingunguti, inajenga Hospital ya Rufaa kule Mtwara, inajenga Hospitali ya Rufaa kule Musoma pamoja na majengo mbalimbali. Kwa kuitikia wito wako mwaka huu tutajenga nyumba 400 za ghorofa za kupangisha hapa Dodoma. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ulitoa wazo kwa Dodoma tusijenge nyumba ndogo ndogo kama hizi tumeitikia wito wako tutakuja kujenga nyumba 400 hivi sasa za ghorofa kwa ajili ya kupangisha, na muelekeo wa *National Housing* sasa katika miradi yote tutakayotekeleza ya shirika asilimia 80 tutajenga nyumba za kupangisha ni asilimia ndogo tu 20 ndiyo tunauza tungetaka Shikirika la Nyumba libaki na nyumba za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba nihitimishe kwa hotuba yangu naomba Waheshimiwa Wabunge maelezo ni mengi ya mafanikio ya miaka mitano na ninyi mnajua sasa kama Wasimamizi wa Serikali Sekta ya Ardhi imetulia, ulaghai, ujambazi, wizi, utapeli umepungua sana. Kwa hiyo, naomba nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimwa Rais ambaye ametupa shime kufanya kazi hii vizuri nataka kuwahakikishia kwamba jambo kazi inaendelea lakini kazi kubwa imefanyika katika Sekta ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ambaye amekuwa msaidizi wangu wa dhati ukimtuma hata usiku kesho amekwenda. Lakini nimshukuru sana Katibu Mkuu wangu Mary Makondo ambaye Kamati kila mara mlikuwa mnamuombea awe Katibu Mkuu na Rais amesikia kilio chenu amemteua kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi. Huyu ni mtoto wa ndani ameanzia kazi humu ndani anaijua Wizara *in, out*, lakini nimshukuru Bwana Nicolaus Mkapa Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Kamishna wetu Mathew na Wakuu wa Idara wote na Watendaji wote waliopo kwenye Halmashauri na Mikoani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wakuu wa Mikoa, Ma-RAS kwa kutupa Ofisi hizi za Mikoa, Ofisi hizi wametupa bure tumeshirikiana nao katika kukarabati Ofisi zote hizi lakini wenzetu Wakuu wa Mikoa wamechangamkia jambo hili wametupa Ofisi zote kama mnavyoziona bila kutupangisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa kwa heshima hii mliyotupa. Pia nawashukuru Washirika wa Maendeleo; *DFID*, *SIDA* na *DANIDA, World Bank* na Korea ya Kusini kwa kuwezesha miradi tuliyotekeleza Morogoro na tutakayotekeleza mwakani.

Pia nawashukuru wadau mbalimbali ambao wametuunga mkono katika zoezi hili la kupeleka mamlaka mikoani; *NMB, CRDB, NBC, AZANIA Bank, STAN Bank, TPB* na Taasisi ya ASASI ambayo imetusaidia katika ukarabati wa jengo Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, nashukuru sana kwa kunivumilia, heshima kubwa sana kwako kwa kazi kubwa ambayo umefanya, umetulea sana hata sisi Mawaziri, pamoja na uzoefu wetu, lakini tumeshuhudia makubwa katika uongozi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA WILLIAM V. LUKUVI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## 1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika*****;** naomba kutoa hoja mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayohusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sasa Bunge likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka wa fedha 2019/20. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Bajeti ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2020/21.

2. ***Mheshimiwa Spika*****;** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uzima, afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge la Bajeti. Aidha, kufuatia kifo cha Mhe. Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Newala Vijijini, kilichotokea mwezi Januari, 2020, Mhe. Dkt. Getrude Pangalile Lwakatare aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kilichotokea mwezi Aprili, 2020, Mhe.Richard Mganga Ndassa aliyekuwa mbunge wa Sumve kilichotokea mwezi Aprili 2020 na Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga aliyekuwa mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria kilichotokea tarehe 1 Mei, 2020, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kutoa pole kwako wewe binafsi Mhe. Spika, Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu, jamaa na wananchi walioguswa na misiba hiyo. Vilevile, natoa pole kwa wananchi wote walioathiriwa kwa namna moja ama nyingine na majanga yaliyotokea katika maeneo mbalimbali nchini hususan mafuriko na mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi aina ya Corona (COVID-

19). Tunawaombea marehemu wote kwa Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahala pema peponi, Amina.

*3. **Mheshimiwa Spika;*** kwa namna ya kipekee, naomba pia nitumie fursa hii adhimu kuendelea kutambua na kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi makini katika kusimamia rasilimali za Taifa, kupambana na rushwa na kuimarisha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma.

*4. **Mheshimiwa Spika**;* katika Serikali ya Awamu ya Tano tumeshuhudia mageuzi makubwa ndani ya sekta ya ardhi na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo ni pamoja na Ujenzi wa Reli ya Kisasa (*standard gauge*); kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania; ujenzi wa bwawa la uzalishaji umeme la Julius Nyerere na Ujenzi wa Bomba la Mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) ambayo inatarajiwa kuleta manufaa makubwa kiuchumi na kijamii kwa watanzania. Hakika uongozi wake mahiri umeendelea kuijengea heshima kubwa nchi yetu kitaifa na kimataifa.

*5. **Mheshimiwa Spika**;* kwa nyakati tofauti tumeshuhudia baadhi ya viongozi au wawakilishi kutoka nchi mbalimbali duniani wakitembelea Tanzania kujifunza kuhusu yanayoendelea katika nyanja za siasa, utawala, uwekezaji, mapambano dhidi ya rushwa, nidhamu ya ukusanyaji wa mapato na matumizi, mfumo wa utoaji elimu bila ada ngazi ya msingi hadi sekondari pamoja na masuala ya ukuzaji demokrasia na udumishaji wa amani nchini.

*6. **Mheshimiwa Spika;*** nawapongeza pia Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali wakilenga kuboresha huduma za msingi kwa Umma kama kichocheo cha kudumisha amani, upendo, mshikamano na utulivu nchini. Napenda

kuwashukuru kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Vilevile, nawapongeza Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Balozi Seif Ali Idd (Mb.), Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uongozi imara katika kusimamia maslahi, ustawi wa wananchi wa Tanzania Zanzibar na kuendelea kudumisha misingi ya Muungano wetu.

7. ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), kwa kuongoza na kusimamia kwa umahiri shughuli za Bunge letu. Vilevile ninawapongeza Wenyeviti wote wa Bunge ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakisimamia na kuongoza shughuli za Bunge kwa ufanisi. Tunawaombea Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema na hekima katika kuwatumikia wananchi.

8. ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kuwapongeza Mhe. George Simbachawene Mbunge wa Kibakwe kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Iddi Azzan Zungu Mbunge wa Ilala kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira na Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Mbunge wa Iramba Magharibi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Nawatakia kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

9. ***Mheshimiwa Spika;*** naomba kutumia fursa hii kumpongeza tena Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imeelezea utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2019/20 na mwelekeo wa shughuli za Serikali zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21. Wizara yangu imezingatia na itatekeleza maelekezo na maagizo yanayoihusu Sekta ya Ardhi ili kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali yanatimizwa ipasavyo.

10. ***Mheshimiwa Spika;*** kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mhe. Kemilembe Rose Julius Lwota (Mb.), kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia kwa kipindi chote pamoja na ushauri wao ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pia, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa uchambuzi makini walioufanya na ushauri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu **48** –Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03 –** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, ninawashukuru kwa maoni na ushauri walioutoa wakati wa kusimamia shughuli zinazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake kwa kipindi chote cha Serikali ya Awamu ya Tano. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii na kutoa mwelekeo mpya wa mabadiliko katika Sekta ya Ardhi.

*11.* ***Mheshimiwa Spika;*** napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Ismani kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa bungeni. Aidha, nawapongeza kwa juhudi wanazofanya katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kujiletea maendeleo yao binafsi pamoja na Taifa kwa ujumla.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA

***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu inatekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995;

ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000;

iii) Kusimamia utawala wa ardhi;

iv) Kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji;

v) Kusimamia na kuwezesha upimaji wa ardhi na kutayarisha ramani;

vi) Kumilikisha ardhi na kuwezesha utoaji wa hati za hakimiliki ya kimila;

vii) Kusajili hatimiliki za ardhi, nyaraka za kisheria na kuimarisha usalama wa milki;

viii) Kusimamia uthamini wa mali nchini;

ix) Kuhamasisha na kuwezesha ujenzi wa nyumba bora;

x) Kusimamia uendelezaji milki;

xi) Kusimamia utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;

xii) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na huduma za Sekta ya Ardhi;

xiii) Kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wake;

xiv) Kusimamia taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Shirika la Nyumba la Taifa na Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro; na,

xv) Kusimamia maslahi, utendaji kazi na maendeleo ya watumishi wa Wizara.

## 3.0 HALI YA SEKTA YA ARDHI NCHINI

*12.* ***Mheshimiwa Spika;*** Sekta ya Ardhi imeendelea kuimarika na kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa kila mwananchi na Taifa kwa ujumla hasa kwa kuwa mhimili na kichocheo cha uwekezaji na uzalishaji katika sekta za kilimo, viwanda, ujenzi, mifugo, uvuvi, maliasili, nishati, madini, miundombinu na hivyo kuongeza ajira na kukuza pato la Taifa.

13. ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuhakikisha Sekta ya Ardhi inaimarika zaidi, Wizara imeendelea kujenga mifumo ya utawala na usimamizi wa ardhi kwa kuanzisha Ofisi za ardhi za Mikoa yote **26** pamoja na kuendelea kuimarisha Ofisi za Ardhi ngazi ya Halmashauri zote nchini

14. ***Mheshimiwa Spika*;** Wizara imeendelea kufanya mageuzi katika utumiaji wa teknolojia katika utoaji wa huduma za ardhi. Hali hii imerahisisha mifumo ya upangaji, upimaji, usimamizi wa ardhi, usajili na utoaji hati, na uhifadhi wa kumbukumbu. Utumiaji wa teknolojia pia umeongeza uwazi katika utendaji kazi na upatikanaji wa taarifa hivyo kupunguza uwezekano wa kutokea kwa migogoro.

15. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi iliyokuwa imekithiri nchini. Aidha, katika utatuzi wa migogoro ya ardhi, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya msingi yanayohusu Sekta ya Ardhi.

16. ***Mheshimiwa Spika;*** hali ya uendelezaji wa makazi nchini imeendelea kuimarika kwa kutekeleza programu na mikakati ya upangaji na urasimishaji makazi nchini. Wizara imeendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji, sekta binafsi na washirika wa maendeleo katika kutekeleza kazi hizo. Vilevile, Wizara imeendelea kuandaa na kusimamia miongozo mbalimbali ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi.

17. ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kuimarisha huduma za upimaji wa ardhi nchini kwa kusimika miundombinu ya mtandao mpya wenye alama za upimaji **831** nchi nzima zinazorahisisha upimaji wa ardhi ndani ya kilometa **40**. Pamoja na juhudi hizi, Serikali inaendelea kuongeza alama hizo ili kupunguza umbali kati ya alama moja na nyingine utakaosaidia kupunguza gharama za upimaji.

18. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kuimarisha usalama wa milki kwa wananchi kwa kurahisisha mifumo ya utoaji hati, utambuzi wa vipande vya ardhi mijini na vijijini na upatikanaji wa taarifa za wamiliki. Vilevile, Wizara imeendelea

kufanya maboresho ya sera, sheria na kanuni mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na utoaji huduma kwa wananchi.

## 4.0 MWELEKEO WA SEKTA YA ARDHI NCHINI

*19.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 hadi 2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati wa kuzindua Bunge la 11 mwezi Novemba, 2015; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013-2033); Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000; pamoja na sheria na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali.

*20.* ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kuzingatia nyaraka na miongozo hiyo muhimu, Wizara yangu itaendelea kutekeleza kwa makini masuala yaliyomo yanayohusu Sekta ya Ardhi mwaka hadi mwaka ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa na Serikali. Mwelekeo wa Wizara ni kuleta mageuzi katika utoaji wa huduma karibu na maeneo ya wananchi ili kuwa na uhakika wa milki salama, nyumba bora, makazi endelevu, mifumo imara ya upimaji ardhi, ukusanyaji wa maduhuli na kumbukumbu za ardhi nchini.

*21.* ***Mheshimiwa Spika;*** ardhi ni rasilimali muhimu kwa jamii na matumizi yake ni mtambuka hivyo maendeleo katika sekta mbalimbali nchini yanategemea ardhi. Wizara itaendelea kuhakikisha ardhi inatumika kwa ajili ya kuongeza uwekezaji katika uzalishaji mali, kilimo, viwanda, ufugaji, uchimbaji madini, ujenzi wa miundombinu ya kimkakati ambayo itaongeza ajira, mapato na mauzo ya nje. Serikali itaendelea kutambua na kuhakiki uwekezaji katika ardhi ili kutambua mchango wake katika uchumi wa nchi.

*22.* ***Mheshimiwa Spika;*** migogoro ya ardhi kwa muda mrefu imekuwa ni kero kwa wananchi nchini. Katika kuhakikisha

migogoro hiyo inakoma Wizara imekuwa ikishirikiana na Wizara nyingine za kisekta na taasisi mbalimbali kuhakikisha migogoro hiyo inatatuliwa na kupunguza uwezekano wa kuibuka kwa migogoro mipya. Wizara itaendelea kujenga uelewa kwa wananchi na wadau kuhusu masuala mbalimbali ya ardhi pamoja na kuwajengea uwezo watumishi ili kuimarisha huduma zitolewazo kwa jamii. Vilevile, Wizara itaendelea kujenga Mifumo ya Kitaasisi itakayosaidia utatuzi wa migogoro.

*23.* ***Mheshimiwa Spika;*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, majukumu na hali ya Sekta ya Ardhi, naomba sasa nitoe ufafanuzi kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**), pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka wa fedha 2019/20 na makadirio ya mapato na matumizi ya mafungu haya kwa mwaka wa fedha 2020/21. Takwimu za utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 zilizopo katika hotuba hii zinaishia tarehe 30 Aprili, 2020. Hotuba hii inatoa pia taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa kipindi cha miaka mitano (2015/16 hadi 2019/20).

## 5.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/20 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2020/21

*24.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imetekeleza majukumu yake kupitia Fungu **48**-Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03**-Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

### Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 48

***Mapato***

*25.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni **180** kutokana na vyanzo vya mapato ya kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara imekusanya shilingi bilioni **84.5** sawa na asilimia **47** ya lengo (**Jedwali Na. 1A & Na. 1B).**

*26.* ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kipindi cha miaka mitano, hali ya makusanyo ya maduhuli yatokanayo na sekta ya ardhi imeendelea kuimarika. Makusanyo haya yameongezeka kutoka shilingi **bilioni 74.71** mwaka 2015/16 hadi kufikia wastani wa shilingi **bilioni 100** mwaka 2019/20 **(Jedwali Na.2).** Ongezeko hili limechangiwa na hatua za makusudi zilizochukuliwa na Wizara ikiwemo kuimarisha matumizi ya mifumo ya ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki na kuongezeka kwa idadi ya walipa kodi. Wizara inaendelea kuweka utaratibu wa namna ya kuhakikisha kila mmiliki wa ardhi anachangia pato la Taifa kupitia kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na sekta ya ardhi.

*27.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inaendelea kuhamasisha na kufuatilia wamiliki wa ardhi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari. Natumia fursa hii kuwapongeza wamiliki wa ardhi waliolipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. **Natoa rai kwa wananchi waliopimiwa ardhi, kutambuliwa milki zao na kumilikishwa kulipa kodi kwa wakati ili kuepuka tozo ya adhabu au hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa dhidi yao.**

*28.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara yangu inatarajia kukusanya shilingi **bilioni 200** kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

i) Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri itakayosaidia ukusanyaji wa mapato kwa urahisi;

ii) Kuboresha kanzidata ya wamiliki wa ardhi kwa kutumia mfumo unganishi wa kielektroniki utakaosaidia kuhifadhi kumbukumbu za ardhi na kuwasiliana na wamiliki kwa urahisi kupitia mawasiliano ya simu na barua pepe;

iii) Kushirikiana na Serikali za Mitaa kusambaza hati za madai, kufuatilia malipo ya madeni na kuwafikisha mahakamani

wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi kwa mujibu wa sheria;

iv) Kuongeza wigo wa makusanyo kwa kuwahamasisha wananchi kumilikishwa viwanja vilivyopimwa pamoja na kutambua na kusajili wamiliki wa kila kipande cha ardhi katika maeneo ambayo hayajapangwa na kupimwa;

v) Kupima maeneo ya uchimbaji wa madini na kutoza kodi stahiki;

vi) Kuhakiki matumizi ya ardhi iliyomilikishwa yakiwemo maeneo ya taasisi za umma na za kidini ili sehemu ya ardhi inayotumiwa kibiashara itozwe kodi stahiki;

vii) Kuweka utaratibu wa kutoza kodi ya pango la ardhi kwa mashamba makubwa yanayotumika kibiashara;

viii) Kutambua na kutoza kodi wamiliki wenye Hatimiliki za Sehemu ya Jengo (Unit Titles); na

ix) Kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wamiliki wa ardhi kulipa kodi kwa wakati.

## Matumizi

*29.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliidhinishiwa shilingi **bilioni 63.9** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **bilioni 17.4** zilikuwa kwa ajili ya mishahara; shilingi **bilioni 19.7** kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi **bilioni 26.8** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara iliongezewa bajeti ya Shilingi **bilioni 6.48** kwa ajili ya kulipa madeni ya Wazabuni na Watumishi baada ya uhakiki uliofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango na kuifanya bajeti kuwa jumla ya shilingi bilioni **63.9.** Hadi tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara ilipokea shilingi **bilioni 40.5** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, sawa na asilimia **63.4** ya bajeti. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **14.9** ni kwa ajili ya mishahara na shilingi **bilioni 15.8** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi

**bilioni 9.8** zilitolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo (**Jedwali Na. 3)**.

**Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 03**
***Mapato***
*30.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilitarajia kupata **shilingi milioni 706.** Kati ya fedha hizo, shilingi **milioni 700** ni kutoka kwa wadau wa kimkakati na shilingi **milioni 6** ni kutokana na makusanyo ya kodi ya pango la nyumba za Tabora. Hadi tarehe 30 Aprili, 2020, Tume imepokea shilingi milioni **446.58** sawa na asilimia **63.3** ya lengo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni **435.61** ni fedha kutoka kwa wadau wa kimkakati na shilingi milioni **10.97** ni mapato ya ndani.

***Matumizi***
*31.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Tume iliidhinishiwa shilingi **bilioni 5.24** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **bilioni 1.27** ni kwa ajili ya mishahara, shilingi **milioni 979.82** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi **bilioni 3.00** ni kwa ajili ya mradi wa maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 Tume ilipokea kiasi cha shilingi bilioni **1.53** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia **29.1.** Kati ya fedha hizo, shilingi milioni **922.06** ni kwa ajili ya mishahara na shilingi milioni **604.85** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

## 5.1 UTAWALA WA ARDHI
***Usimamizi wa sekta ya ardhi***

*32.* ***Mheshimiwa Spika;*** utawala wa ardhi unalenga kuhakikisha ardhi yote nchini inapangwa, inapimwa na kumilikishwa kwa lengo la kuboresha huduma katika uwekezaji, uboreshaji wa makazi, milki salama na kuwa kichocheo cha kuinua uchumi wa jamii na Taifa kwa ujumla. Majukumu haya yanatekelezwa kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza sekta ya ardhi.

*33.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa huduma za sekta ya

ardhi zinapatikana karibu na wananchi ili kuwapunguzia usumbufu na gharama za upatikanaji wake. Juhudi za kusogeza huduma hizi kwa wananchi zilianza kwa kuanzisha Ofisi za Ardhi katika Kanda tisa (**9**). Pamoja na juhudi hizo, bado wananchi wamekuwa wakipata usumbufu na kutumia gharama kubwa kuzifikia Ofisi hizo. Kwa muktadha huu, Wizara imeanzisha Ofisi za Ardhi katika Mikoa yote **26** nchini ambapo huduma zote za upangaji, upimaji, umilikishaji, uthamini, usajili wa Hati na Nyaraka, ramani na michoro zitapatikana katika ofisi hizo. **Natoa rai kwa wananchi na viongozi wa Mikoa na Halmashauri kutoa ushirikiano na kuzitumia ofisi hizo kupata huduma za ardhi.**

*34.* ***Mheshimiwa Spika*;** Wizara yangu imeendelea kuziimarisha Ofisi za Ardhi katika Halmashauri zote nchini kwa kuwapanga na kuwasimamia watumishi wa sekta ya ardhi wa kada zote kwa uwiano sawia. Aidha, Wizara itaendelea kuzipatia ofisi hizo vitendea kazi, rasilimali fedha pamoja na watumishi wa kada zinazohitajika ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma.

***Uandaaji na Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria***

*35.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kutekeleza Sera na Sheria za Ardhi, Wizara inaratibu uandaaji, usajili na utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji, Hati za Hakimiliki za Kimila na Hatimiliki za Ardhi. Azma hii inalenga kuimarisha usalama wa milki za ardhi kwa wananchi.

*36.* ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa katika kipindi cha miaka mitano,Wizara imeratibu upimaji, uandaaji na usajili wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **2,905** na hivyo kuzipatia Halmashauri za Vijiji mamlaka ya usimamizi wa ardhi ya kijiji kwa mujibu wa sheria. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji iliahidi kuandaa na kusajili Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, jumla ya Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **540** viliandaliwa. Hii inaifanya nchi kuwa na jumla ya vijiji **11,743** vilivyopimwa na kupewa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji kati ya vijiji **12,319** vilivyopo nchini.

37. ***Mheshimiwa Spika;*** vilevile, kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeratibu uandaaji na utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **375,259** katika Halmashauri mbalimbali nchini. Kwa mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kuratibu uandaaji na utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **150,000**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020, Jumla ya Hati za Hakimiliki ya Kimila **92,585** zimetolewa (**Jedwali Na. 4**). Kwa kipindi hicho jumla ya hati **1,516** zimetumika kama rehani ya mikopo yenye thamani ya shilingi **bilioni 61.3** kwenye taasisi za fedha.

38. ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara imeratibu uandaaji na utoaji wa Hatimiliki **195,170** (**Jedwali:- 5A**), Nyaraka za Kisheria **255,662** (**Jedwali:- 5B**) na hati za umiliki wa sehemu ya jengo zipatazo **3,522** katika Halmashauri mbalimbali nchini. Kwa mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kuandaa na kutoa hatimiliki **100,000,** Nyaraka za Kisheria **50,000** na hati za umiliki wa sehemu ya jengo zipatazo **2,000**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, jumla ya hatimiliki **37,870**, Nyaraka za Kisheria **55,179** na hati za umiliki wa Sehemu ya Jengo zipatazo **310** zimetolewa. Aidha, Wizara imesajili rehani za ardhi **3,070** chini ya Sheria ya Ardhi (Sura 113). Rehani hizo zimesaidia wananchi kupata mikopo na hivyo kuwanufaisha kiuchumi. **Natoa rai kwa wananchi waone umuhimu wa kumiliki ardhi kisheria na kutumia nyaraka za umiliki walizopewa kuwainua kiuchumi.**

39. ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara inakusudia kusajili na kutoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100**, Hati za Hakimiliki ya Kimila **520,000**, Hatimiliki **200,000**, nyaraka za kisheria **100,000**, hati za umiliki wa sehemu ya jengo **1,000** na rehani za ardhi kadri maombi yatakavyopokelewa na kusajiliwa. **Natoa rai kwa Mamlaka za Upangaji nchini kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi ili kuongeza usalama wa milki.**

***Usimamizi wa Masharti ya Umiliki***

40. ***Mheshimiwa Spika;*** Sheria za Ardhi zinamtaka kila mmiliki kuiendeleza ardhi aliyomilikishwa kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika nyaraka za umiliki. Kwa kipindi cha

miaka mitano, Wizara ilikagua mashamba **1,985** ili kujiridhisha uendelezaji wake. Kati ya hayo mashamba **45** yenye jumla ya ekari **121,032.2** umiliki wake ulibatilishwa baada ya kukiuka masharti ya Umiliki. Kati ya ekari hizo zilizobatilishwa ekari **12,448.5** zilitengwa kwa ajili ya uwekezaji na sehemu kuandaliwa mipango ya matumizi mengine na kugawiwa kwa wananchi kupitia mamlaka za upangaji. **Natoa wito kwa wamiliki wa mashamba kuyaendeleza kwa mujibu wa masharti ya umiliki. Serikali itachukua hatua stahiki kwa wamiliki wote watakaokiuka masharti ikiwemo kufutiwa milki zao.**

*41.* ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara itaendelea kufanya utambuzi na ukaguzi wa mashamba ili kubaini wamiliki wasiozingatia masharti ya umiliki na kuwachukulia hatua za kisheria. Aidha, ardhi ya mashamba ambayo milki zake zitabatilishwa itakuwa sehemu ya hazina ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji pamoja na kuwapatia wananchi wenye mahitaji kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji baada ya kupangwa na kupimwa upya.

***Uthamini wa Mali***

*42.* ***Mheshimiwa Spika;*** uthamini wa mali zinazohamishika na zisizohamishika, na uidhinishaji wa taarifa za uthamini ni miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa na Wizara yangu. Uthamini hufanyika ili kuwezesha ulipaji wa fidia, utozaji wa ushuru wa Serikali unaotokana na mauzo au uhamisho wa umiliki wa mali, utozaji wa malipo ya awali (*premium*) wakati wa kutoa milki, mizania, kuweka mali rehani kwa ajili ya kupata mikopo, mirathi, kinga ya bima na utozaji kodi ya pango la ardhi.

*43.* ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara yangu iliidhinisha taarifa za uthamini wa kawaida wa mali **52,645** na uthamini wa fidia wa mali **84,223** (**Jedwali Na. 6**). Katika kipindi hicho, Wizara pia imeshiriki kufanya uthamini wa mali katika maeneo ya miradi mikubwa ya kitaifa na ya kimkakati. Katika miradi hiyo, majedwali matatu (**3**) ya fidia yenye jumla ya wafidiwa **9,881** na fidia ya mali kiasi cha shilingi bilioni **113.9** yaliandaliwa na kuidhinishwa **(Jedwali Na.7).**

*44.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara ilipanga kuidhinisha taarifa za uthamini **29,000**, ambapo kati ya hizo uthamini wa kawaida ni **10,000** na uthamini wa fidia ni **19,000** na kushughulikia malalamiko **120** ya uthamini wa fidia. Vilevile, Wizara ilipanga kuimarisha kumbukumbu za uthamini ikiwemo kukamilisha uhuishaji wa viwango vya bei ya soko la ardhi katika mikoa **26**.

*45.* ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini **34,276** ambapo kati ya hizo taarifa za uthamini wa kawaida ni **13,060** na uthamini wa fidia **21,216** (**Jedwali Na. 8**). Jumla ya malalamiko **25** ya uthamini wa fidia yalipokelewa na kushughulikiwa kati ya malalamiko **120** yaliyotarajiwa. Kupungua kwa malalamiko kunatokana na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi na ushirikishwaji uliofanywa na wataalam wakati wa uthamini Aidha, jedwali la thamani ya mimea ambalo limekuwa likitumika kuanzia mwaka 2012 limehuishwa hivyo kuwa na jedwali jipya la viwango vya thamani ya mimea vya mwaka 2020. Kazi ya kuhuisha viwango vya bei ya soko la ardhi katika mikoa **26** inaendelea.

*46.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara yangu itaratibu uandaaji wa taarifa za uthamini wa kawaida wa mali **15,700** na uthamini wa fidia wa mali **24,300**. Kadhalika, Wizara itaendelea kushughulikia malalamiko **120** ya uthamini wa fidia, kuendelea kufanya utafiti na kuandaa viwango vya thamani ya ardhi katika mikoa yote **26** nchini.

***Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi nchini***

*47.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kushughulikia migogoro ya ardhi ambayo imekuwa kero kubwa nchini kadri inavyojitokeza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Migogoro hiyo ipo katika sura mbili ambazo ni migogoro ya mipaka ya kiutawala na migogoro inayotokana na mwingiliano wa matumizi ya ardhi. Sheria za ardhi zimeweka utaratibu wa namna ya kushughulikia migogoro ya ardhi na pale inaposhindikana migogoro hiyo hupelekwa katika ngazi ya mahakama kutatuliwa.

*48.* ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara yangu imekuwa na mikakati mbalimbali ya kushughulikia utatuzi wa migogoro. Mikakati hiyo ni pamoja na kushirikiana na viongozi wa Serikali, kutoa elimu kwa umma kuhusu utatuzi wa migogoro, kuanzisha madawati ya malalamiko katika ofisi za ardhi za halmashauri nchini, na programu ya '**Funguka kwa Waziri'.** Kupitia mikakati hiyo jumla ya migogoro **15,808** ilitatuliwa kwa njia ya kiutawala katika halmashauri mbalimbali nchini (**Jedwali Na. 9**). Pia, jumla ya migogoro **131,603** ya matumizi ya ardhi ilitatuliwa kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. **Natoa rai kwa viongozi na watumishi kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na maadili ya utumishi wa umma na kuendelea kushirikiana na wananchi katika utatuzi wa migogoro na kuepuka kusababisha migogoro mipya**.

*49.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi hiki cha miaka mitano, Wizara iliimarisha utaratibu wa utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi ambayo ni mtambuka kwa njia shirikishi kwa kushirikiana na Wizara za kisekta za OR-TAMISEMI, Maliasili na Utalii, Mifugo na Uvuvi, Maji, Kilimo, Viwanda, Ulinzi na Mazingira. Kupitia utaratibu huo, taarifa mbalimbali zinazohusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya ufugaji, kilimo, misitu, hifadhi za wanyamapori, vyanzo vya maji, hifadhi za mazingira, ulinzi, mipaka ya kiutawala na fidia ya ardhi ziliainishwa kutoka kwa waheshimiwa wabunge, sekta na halmashauri mbalimbali na kuandaa mapendekezo yenye ufumbuzi wa kudumu wa migogoro ya matumizi ya ardhi nchini.

*50.* ***Mheshimiwa Spika;*** kutokana na kukithiri kwa migogoro ya ardhi, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliunda Kamati ya Mawaziri wa Kisekta ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu. Kufuatia mapendekezo ya Kamati, Baraza la Mawaziri mnamo mwezi Septemba, 2019, liliridhia kuwa vijiji **920** kati ya vijiji **975** vilivyokuwemo ndani ya hifadhi, mapori ya akiba na ranchi kuhalalishwa rasmi kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na kijamii. Aidha, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya vijiji **55** vilivyobaki ili kutoa maamuzi. Wizara kwa kushirikiana na

Wizara za kisekta na wadau mbalimbali inaendelea kuhakiki mipaka, kupanga na kupima ili kuzipa Serikali za vijiji mamlaka ya kusimamia ardhi za vijiji hivyo.

*51.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu iliahidi kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi kiutawala na kushughulikia mashauri **500** yaliyopo na yatakayofikishwa mahakamani. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, hadi tarehe 30 Aprili, 2020 migogoro ya Matumizi ya ardhi **5,892** ilishughulikiwa kiutawala. Kwa mwaka wa fedha 2020/21 Wizara imepanga kutatua migogoro **1,000** ya umilikaji ardhi kiutawala.

### *Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya*

*52.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu imeendelea kusimamia na kuhudumia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanayofanya kazi ya kupokea, kusikiliza na kuamua mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kushughulikia mashauri **28,615** yaliyokuwepo na yatakayofunguliwa. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 mashauri mapya **15,841** yalifunguliwa na kufanya jumla ya mashauri yote kuwa **44,456**. Kati ya hayo, mashauri **19,360** yaliamuliwa.

*53.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kutekeleza azma ya kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini ikiwa ni pamoja na utatuzi wa migogoro ya ardhi, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kuanzia mwaka wa fedha 2020/21, Serikali inakusudia kuhamishia shughuli za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika mhimili wa Mahakama.

### *Usimamizi wa Visiwa na Fukwe Nchini*

*54.* ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta ilifanya uhakiki uwandani wa visiwa **289** nchini na kuandaa taarifa kuhusu namna bora ya kuvisimamia, kudhibiti na kuviendeleza. Visiwa hivyo vyenye ukubwa tofauti na matumizi mbalimbali vinasimamiwa na mamlaka zaidi ya moja. Mamlaka hizo

zinajumuisha Hifadhi za Taifa (TANAPA), Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU), Wizara ya Ulinzi, Wakala wa Misitu na Serikali za Mitaa.

*55.* ***Mheshimiwa Spika;*** tathmini iliyofanyika imebaini kuwepo kwa changamoto katika mfumo wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi na uendelezaji wa visiwa na fukwe nchini. Hali hii imesababisha baadhi ya visiwa na fukwe kutumika kama maficho ya wahalifu, njia za kupitisha bidhaa za magendo, uhamiaji haramu, na pia kuna uharibifu mkubwa wa mazingira. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21 itaimarisha mfumo wa usimamizi na uendelezaji wa visiwa na fukwe ili kuwa na matumizi endelevu kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

***Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi***

*56.* ***Mheshimiwa Spika****;* Wizara yangu kupitia Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi ina jukumu la kuidhinisha maombi ya umilikishaji ardhi kwa ajili ya uwekezaji, uendelezaji fukwe, pamoja na maeneo ya kimkakati yenye maslahi ya umma. Katika kipindi cha miaka mitano, Kamati ilipokea na kuidhinisha jumla ya maombi **527** ya umilikishaji ardhi. Kati ya hayo, maombi **331** yalikuwa ya uwekezaji na **196** ya viwanja vya fukwe, ofisi za Balozi na Mashirika ya Kimataifa (**Jedwali Na. 10**). Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kuiwezesha Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi kutimiza majukumu yake.

***Bodi za Usajili wa Wataalam wa Fani za Ardhi***

*57.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu inasimamia shughuli za bodi mbalimbali za Wataalam wa sekta ya ardhi. Bodi hizo ni; Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Wathamini na Bodi ya Usajili wa Wapima Ardhi. Majukumu ya Bodi hizi ni kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi wa wataalam na kutoa adhabu kwa ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma. Katika kipindi cha miaka mitano, jumla ya Wataalam wa Mipangomiji **158,** Wathamini **114** na Wapima Ardhi **134** walisajiliwa na bodi zao. Aidha, jumla ya kampuni za upangaji **57,** upimaji **22** na uthamini **42** zimesajiliwa na kufikia jumla ya kampuni za

upangaji **76** na upimaji **82** (**Jedwali Na. 11A,11B na 11C**). Uwepo wa wataalam na kampuni hizo umesaidia kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na urasimishaji ardhi.

*58.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuendelea kusimamia weledi na maadili ya utendaji kazi, Wizara kwa kushirikiana na bodi za wataalam wa sekta ya ardhi ilibaini ukiukwaji wa maadili unaofanywa na baadhi ya kampuni ikiwemo kuongeza gharama za upangaji na upimaji kinyume na miongozo iliyowekwa na Wizara. Kampuni za upangaji tano **(5)** na ya upimaji moja **(1)** zimefutiwa usajili na wataalam watano (**5**) wa mipangomiji na mpima ardhi mmoja **(1)** wamechukuliwa hatua za kinidhamu.

## 5.2 HUDUMA ZA TEHAMA

***Utunzaji wa Kumbukumbu za Ardhi***

*59.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Wizara ilibuni na kutekeleza Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (Integrated Land Management Information System – ILMIS) na kujenga Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi. Huduma za ardhi kwa kutumia Mfumo wa ILMIS zinatolewa katika Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam. Mfumo huu umerahisisha utoaji wa huduma za ardhi ambapo muda wa utoaji hati umepungua kutoka siku **90** hadi siku saba (**7**) endapo mwombaji atawasilisha nyaraka zote zinazohitajika kwa wakati.

*60.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kuendelea kuunganisha mfumo wa ILMIS na utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kidigitali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia 30 Aprili, 2020 Wizara imekamilisha kuunganisha mfumo huo katika Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam na Hati za kielektroniki zinatolewa. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara itaendelea kuboresha mfumo kwa kujenga miundombinu, kuchambua, kupiga picha (scanning) na kuhifadhi michoro, ramani na hati katika Ofisi za ardhi za mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini.

61. ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Wizara yangu imeendelea kuwekeza, kuboresha na kuongeza kasi katika matumizi ya mifumo ya kidigitali ili kwenda sambamba na mabadiliko ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Katika kutekeleza haya, Wizara imesimika Mfumo wa Ofisi Mtandao (***e-office)*** ambao unasaidia katika mawasiliano na kutoa maamuzi kwa wakati. Sambamba na hilo, Wizara ilinunua na kusambaza mashine za kieletroniki (*Point of Sales Machine-PoS*) **238** kwenye ofisi za ardhi zilizoko katika Halmashauri zote nchini na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Mashine hizo zinarahisisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Wizara pia imeunganisha mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli ya sekta ya ardhi katika Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali (*GePG*). Hivyo, kwa kutumia simu ya mkononi mwananchi anaweza kulipa kodi ya pango la ardhi kupitia simu yake.

62. ***Mheshimiwa Spika****;* Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali kuboresha mifumo ya TEHAMA na kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi. Wizara imewezeshwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao kuunganisha Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi (NLIC) na Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (GovNet). Pia, imeunganisha mifumo ya kutunza kumbukumbu za ardhi na Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA) ili kuhakiki uraia wa wamiliki wa ardhi nchini.

63. ***Mheshimiwa Spika****;* katika kuwajengea uwezo watumishi wa sekta ya ardhi wa kutumia Mifumo ya TEHAMA, Wizara iliendesha mafunzo ya matumizi bora ya mifumo ya TEHAMA kwa watumishi **422** kutoka Halmashauri na Sekretarieti za mikoa yote nchini.

## 5.3 UPIMAJI ARDHI NA UTAYARISHAJI WA RAMANI

64. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu ina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za upimaji ardhi wa nchi kavu na ndani ya maji, na utayarishaji wa ramani za msingi kwa ajili ya utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Serikali. Wizara imeendelea kutoa miongozo ya upimaji ardhi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu hayo.

***Utayarishaji wa Ramani za Msingi***

*65.* ***Mheshimiwa Spika***; kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara imepiga picha za anga na kuandaa ramani picha yenye uwiano mkubwa wa **1: 2,500** katika Mkoa wa Dar es Salaam na sehemu ya Mkoa wa Pwani kwa eneo la ukubwa wa kilometa za mraba **4,300**. Vilevile, katika kipindi hicho, Wizara imehuisha ramani za msingi **144** za uwiano mdogo wa **1: 50,000** katika mikoa ya Dodoma, Geita, Songwe na Ruvuma. Ramani hizo zimewezesha kurahisisha upangaji na upimaji wa maeneo mbalimbali katika mikoa hiyo. Aidha, Wizara imehuisha ramani ya Tanzania na kuwa na ramani inayojumuisha mipaka ya Mikoa na Wilaya mpya, uoto wa asili, miundombinu ya usafirishaji, mito na maziwa (**Kiambatisho Na.1**)

*66.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) imeandaa ramani za uhakiki wa mali za wananchi waliopisha Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Morogoro hadi Makutopora Wilayani Manyoni yenye urefu wa kilometa **336.** Ramani hizi zilisaidia kuharakisha zoezi la uthamini wa mali na hivyo kuepusha migogoro ya malipo ya fidia (**Kiambatisho Na. 2).**

*67.* ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara yangu iliahidi kuhuisha ramani za msingi **68** pamoja na ramani nyingine katika wilaya mbalimbali. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia 30 Aprili, 2020, ramani za msingi **68** zenye uwiano wa 1: 50,000 na ramani za Mikoa **23** zilihuishwa. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kuhuisha ramani za msingi 66 katika wilaya mbalimbali nchini.

*68.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na OR - TAMISEMI imeendelea kutafsiri Matangazo ya Serikali (GN) ya maeneo ya utawala na hifadhi. Tafsiri hizo zimewezesha kutatua migogoro ya mipaka kati ya Kijiji na kijiji, Wilaya na Wilaya, Mkoa na Mkoa pamoja na Vijiji na Hifadhi. Katika kipindi cha miaka mitano, jumla ya

Matangazo ya Serikali (GN) **24** yalitafsiriwa kwa kupima na kuweka alama za mipaka ya utawala na hifadhi (**Jedwali Na. 12A, 12B, 12C & 12D**).

**Upimaji wa ardhi nchi kavu**

*69.* ***Mheshimiwa* Spika;** upimaji wa ardhi nchi kavu unajumuisha upimaji wa viwanja, mashamba, mipaka ya ndani ya nchi na mipaka ya kimataifa. Katika kuwezesha na kurahisisha upimaji kufanyika kwa ufanisi alama za msingi husimikwa ardhini. Katika kipindi cha miaka mitano, Wizara imesimika alama za msingi za upimaji **191** za nyongeza katika mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga Kagera, Songwe na Ruvuma na kufanya kuwa na jumla ya alama za msingi **831** kutoka alama **640** za awali. Wizara itaendelea kusimika alama za msingi mpya **150** katika mwaka wa fedha 2020/21.

***Upimaji wa Viwanja na Mashamba***

*70.* ***Mheshimiwa* Spika**; Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba unaofanywa na Mamlaka za Upangaji na sekta binafsi. Upimaji huu huwezesha wananchi na taasisi mbalimbali kupata hatimiliki za ardhi na kutatua migogoro ya ardhi. Katika kipindi cha miaka mitano, Wizara ilipokea na kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **988,526** na mashamba **5,940** kutoka Halmashauri mbalimbali nchini (**Jedwali Na. 13**).

*71.* ***Mheshimiwa Spika*****;** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara yangu iliahidi kupokea na kuidhinisha ramani za upimaji wa viwanja na mashamba **200,000** pamoja na kutatua migogoro **50** ya mipaka ya vijiji, hifadhi na Wilaya. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 30 Aprili, 2020, ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja **222,849** na mashamba **268** ziliidhinishwa. Aidha, migogoro ya mipaka ya vijiji, hifadhi na ya Wilaya ilitatuliwa wakati wa upimaji.

***Upimaji wa Mipaka ya Maeneo ya Hifadhi***

*72.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na jukumu la uhakiki na upimaji wa mipaka ya maeneo ya hifadhi kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara imehakiki na kupima maeneo manne (**4**) ya

Hifadhi za Taifa za Saadani, Serengeti, Rumanyika na Burigi. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kuhakiki na kupima mipaka ya maeneo ya Hifadhi za Taifa, Mapori Tengefu, Mapori ya Akiba na Misitu ya Hifadhi.

***Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa***

*73.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara ina jukumu la kuimarisha alama za mipaka ya Tanzania na nchi jirani. Tanzania inapakana na nchi **10** kwa mpaka wenye urefu wa kilomita **1,841** nchi kavu na kilometa **2,086** ndani ya maji. Nchi na urefu wa mipaka yake ni kama ifuatavyo:- Uganda (km. **149** nchi kavu na km. **246** ndani ya maji), Kenya (km. **758** nchi kavu na km. **59.71** ndani ya maji), Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (km. **554** ndani ya maji), Burundi (km. **446** nchi kavu na km. **22.85** ndani ya maji), Malawi (km. **146** nchi kavu na km. **248** ndani ya maji), Rwanda (km. **230** ndani ya maji), Msumbiji (km. **51** nchi kavu na km. **670** ndani ya maji), Zambia (km. **289** nchi kavu na km. **56** ndani ya maji). Mipaka baina ya Tanzania na nchi za Comoro (km. **289.81** ndani ya maji) na Shelisheli (km. **341.88** ndani ya maji) inasubiri kuidhinishwa na Umoja wa Mataifa. Aidha, Tanzania iliwasilisha Umoja wa Mataifa maombi ya nyongeza ya eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba **60,000** nje ya ukanda wa kiuchumi baharini. Upatikanaji wa eneo hilo utaongeza wigo na fursa za kiuchumi ikiwemo uchimbaji wa mafuta na gesi.

*74.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Wizara imeimarisha mpaka wenye urefu wa kilomita **172** za nchi kavu kati ya Tanzania na Kenya. Kazi zilizofanyika kuimarisha mpaka huu ni kufanya vikao vya pamoja vya majadiliano, kujenga alama mpya za msingi zilizoharibika, kuweka alama za katikati, ukarabati wa alama zilizoharibika, kupima alama za mpaka, kufyeka mkuza wa mpaka, kupima alama za picha za anga, kutambua majina ya kijiografia ya maeneo, kuandika majina na kupaka rangi alama za mpaka na kuandaa rasimu ya mkataba wa makubaliano ya mpaka. Wizara yangu itaendelea kuimarisha mipaka baina ya Tanzania na nchi jirani kwa mwaka wa fedha 2020/21.

***Upimaji ndani ya maji***

*75.* ***Mheshimiwa Spika;*** upimaji ndani ya maji ni moja ya jukumu la Wizara yangu. Upimaji huu husaidia kuandaa ramani elekezi za njia za vyombo vya usafiri ndani ya maji, kuainisha mipaka ya kimataifa na ujenzi wa mitambo ya uzalishaji umeme, gesi na mafuta, ujenzi wa madaraja, utafiti, kutandaza mabomba, kuongeza vina vya maji, ulinzi na usalama na uhifadhi wa mazingira. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara ilipima bandari tano (**5**) za Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga, Pemba na Wete. Upimaji huu umesaidia kuandaa ramani elekezi za njia za vyombo vya usafirishaji ndani ya maji katika bandari. Jumla ya ramani nane (**8**) zinazoonesha vina vya maji, miamba, mawimbi, mito na milima ziliandaliwa. Wizara yangu itaendelea kupima bandari na maeneo mengine ya ndani ya maji katika mwaka wa fedha 2020/21.

## 5.4 UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI

*76.* ***Mheshimiwa Spika;*** upangaji miji na uendelezaji makazi ni miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa na Wizara yangu. Majukumu haya yanajumuisha uandaaji wa mipango ya jumla (mipango kabambe), mipangokina, utangazaji wa maeneo yaliyoiva kwa upangaji, udhibiti wa uendelezaji miji na vijiji, urasimishaji makazi pamoja na usimamizi na uratibu wa uendelezaji nyumba.

### Upangaji na Usanifu wa Miji

***Utangazaji wa maeneo ya upangaji miji***

*77.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu ina jukumu la kutangaza maeneo ya vijiji yanayokua na kufikia sifa ya kupangwa na kuendelezwa kimji kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007. Vigezo vya kutangaza maeneo hayo ni pamoja na idadi ya watu wasiopungua **10,000**, uwepo wa huduma za msingi za kijamii kama vile zahanati au kituo cha afya, shule ya msingi, huduma za kiuchumi ikiwemo soko na maduka yasiyopungua matano **(5)**. Wizara hutangaza maeneo yenye sifa hizi baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye mamlaka za upangaji. Maeneo hayo huandaliwa mipango ya jumla na mipangokina na mamlaka

za upangaji kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali.

*78.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Wizara ilipokea, kuidhinisha na kutangaza maeneo **72** kutoka katika mamlaka za upangaji. Maeneo hayo yamepandishwa kutoka hadhi ya vijiji na kuwa maeneo ya mipangomiji na yanaendelea kuandaliwa mipangokina (**Jedwali Na. 14**). Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji kutambua, kupokea mapendekezo na kutangaza maeneo yaliyoiva kimipango miji.

***Uandaaji wa Mipango Kabambe***

*79.* ***Mheshimiwa Spika;*** ukuaji na uendelezaji wa miji huongozwa na mipango kabambe inayoainisha matumizi mbalimbali ya ardhi katika miji nchini. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji iliratibu uandaaji na kuidhinisha mipango kabambe **24** katika miji saba **(7)** Manispaa **13** na majiji manne **(4)**. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini kukamilisha Mipango Kabambe **6** na kufuatilia utelekezaji wake katika kanda tatu (**3**). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mipango Kabambe **7** imeandaliwa na kuidhinishwa katika miji **3** manispaa **2** na majiji **2**. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango kabambe umefanyika katika Jiji la Arusha na Mji wa Korogwe na kuonesha uandaaji wa mipangokina unazingatia mipango kabambe. Aidha, mpango kabambe wa Manispaa ya Kigamboni umehuishwa kwenye mpango kabambe wa jiji la Dar es salaam (**Jedwali Na. 15**).

*80.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuunga mkono dhana ya Tanzania ya viwanda jumla ya ekari **284,349.07** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda katika miji mbalimbali nchini iliyoandaliwa mipango kabambe (**Jedwali Na. 16)**. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji itaendelea kufuatilia utekelezaji wa mipango kabambe kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo. **Natoa rai kwa**

**mamlaka za upangaji kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji, utekelezaji wake na kudhibiti uendelezaji miji ili uendane na mipango kabambe**

***Uandaaji wa Mipangokina***

*81.* ***Mheshimiwa Spika;*** mipangokina (michoro ya mipangomiji) huandaliwa na mamlaka za upangaji kwa lengo la kuelekeza ukuaji na uboreshaji wa makazi, kuhifadhi mazingira, kuondoa ukinzani wa matumizi ya ardhi na kutoa uhakika wa upatikanaji wa maeneo yenye matumizi mbalimbali ikiwemo ya uwekezaji. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara ilipokea na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **6,143** yenye jumla ya viwanja **1,456,548** kutoka katika mamlaka za upangaji nchini.

*82.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kupokea, kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka Mamlaka za Upangaji nchini. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, michoro ya Mipangomiji **1,195** yenye jumla ya viwanja **348,918** ilipokelewa na kuidhinishwa. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara yangu inatarajia kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini.

***Urasimishaji Makazi***

*83.* ***Mheshimiwa Spika;*** urasimishaji makazi nchini unahusisha kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha maeneo yaliyoendelezwa bila kupangwa. Lengo la urasimishaji ni kuhakikisha usalama wa milki na kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili huduma za kijamii na miundombinu kwa njia shirikishi. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara ilidhinisha michoro ya Mipangomiji ya urasimishaji yenye viwanja **703,836** katika Halmashauri mbalimbali nchini (**Jedwali Na. 17A)**. Kati ya viwanja hivyo, makampuni binafsi yalipanga viwanja **419,240.** (**Jedwali Na. 17B).**

*84.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji iliahidi kuendelea na zoezi la urasimishaji katika halmashauri katika kanda zote tisa (**9)** ambapo takriban viwanja/makazi **600,000** vitatambuliwa na kurasimishwa. Hadi tarehe 30 Aprili, 2020,

Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji iliandaa michoro ya urasimishaji **334** yenye viwanja/makazi **148,000** katika halmashauri mbalimbali nchini. Katika Mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za urasimishaji makazi zitakazotekelezwa na mamlaka za upangaji nchini.

***Uendelezaji miji***

*85.* ***Mheshimiwa Spika;*** udhibiti wa uendelezaji miji ni suala mtambuka linalotekelezwa kwa kushirikisha Wizara na mamlaka za upangaji. Kutokana na ongezeko la watu, shughuli za kiuchumi na kukua kwa teknolojia, miji hubadilika na kuhitaji uratibu katika uendelezaji wake yakiwemo mabadiliko ya matumizi ya ardhi. Kwa muktadha huu, Wizara yangu, ina jukumu la kuidhinisha mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka mamlaka za upangaji. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara ilipokea na kuidhinisha maombi **1,005** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi.

*86.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara iliahidi kukagua na kuidhinisha maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka Kanda tisa (**9**). Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 Wizara ilipokea na kuidhinisha jumla ya maombi **285** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka mamlaka za upangaji. Wizara itaendelea kuratibu uidhinishaji wa maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi katika mwaka wa fedha 2020/21.

***Usimamizi na uratibu wa uendelezaji nyumba***

*87.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia na kuratibu uendelezaji wa nyumba nchini. Uendelezaji wa nyumba hufanywa na watu binafsi, taasisi za umma au binafsi, Shirika la Nyumba la Taifa, Vyama vya Ushirika wa Nyumba na mamlaka mbalimbali za Serikali. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma za uendelezaji nyumba nchini. Huduma hizo ni pamoja na:- upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, ubunifu wa

nyumba za gharama nafuu, utoaji wa mikopo ya nyumba kwa watumishi wa serikali.

***Mikopo ya ujenzi wa nyumba***

*88.* ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewezesha kuboreshwa kwa mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ambapo: i) Mikopo midogo midogo ya ujenzi wa nyumba kutoka taasisi za fedha kiasi cha shilingi **bilioni 29.87** kilitolewa kwa wananchi **1,914** (**Jedwali Na. 18A**); ii) Benki za biashara zinazotoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zimeongezeka kutoka tatu (**3**) hadi **34** ambapo, mikopo ya nyumba yenye thamani ya shilingi **bilioni 438.58** ilitolewa kwa wananchi **5,460 (Jedwali Na. 18B)**; iii) Kiwango cha riba ya mikopo ya ujenzi wa nyumba katika taasisi za fedha kimeshuka kutoka kati ya asilimia **21-23** hadi kufikia kati ya asilimia **13-18**; na iv) Muda wa kurejesha mikopo midogo midogo umeongezwa kutoka miaka mitano (**5**) hadi **10**.

***Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali***

*89.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali iliahidi kuongeza kiwango cha juu cha mkopo kinachotolewa na Mfuko kutoka shilingi milioni **20** hadi kufikia shilingi milioni **40.** Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Serikali imeridhia ongezeko la kiwango cha mkopo hadi shilingi **milioni 40** ili kukidhi ongezeko la gharama za ujenzi wa Nyumba. Mikopo yenye thamani ya jumla ya **shilingi bilioni 2.13** imeidhinishwa kwa watumishi **121**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 marejesho ya mikopo kiasi cha shilingi **403,719,092** yalikusanywa.

*90.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu iliahidi kuendelea kuboresha taarifa za Nyumba katika kanzidata ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uundwaji wa vyama vya ushirika wa nyumba. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, taarifa za waendelezaji na wasimamiaji milki **139** ambao wamejenga jumla ya nyumba **26,421** zimeingizwa katika kanzidata ya nyumba. Aidha, Vyama vya Ushirika wa Nyumba vinne (4) vimeongezeka katika kanzidata na kufikia vyama vilivyo hai **38** ambavyo vimejenga jumla ya nyumba

**1,056** katika Mikoa ya Dar es Salaam (**818**), Dodoma (**77**), Iringa (**16**), Kagera (**56**), Musoma (**22**), Morogoro (**36**), Mwanza (**15**) na Shinyanga (**16**). Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara yangu itaendelea kuhamasisha ujenzi wa nyumba kupitia ushirika wa nyumba na kuvijengea mazingira ya kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka taasisi za fedha kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika.

*91.* ***Mheshimiwa Spika;*** pamoja na Wizara kuwa na kanzidata ya nyumba za waendelezaji miliki wa mashirika na taasisi mbalimbali, Wizara inaandaa utaratibu wa kufanya sensa ya nyumba nchi nzima na kuunda kanzidata ya nyumba kwa kutumia Mifumo unganishi ya kielektroniki ambayo inaweza kutumiwa na wadau wote wa sekta ya nyumba. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) imefanya sensa ya majaribio katika Wilaya ya Kondoa ikiwa ni hatua ya awali ya uboreshaji wa kanzidata.

***Ushirikiano na Taasisi za kimataifa Katika Uendelezaji wa Makazi***

*92.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu imeendelea kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kimataifa yenye lengo la kujenga mahusiano na kubadilishana uzoefu katika usimamizi na uendelezaji makazi. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara imeshiriki katika mikutano **15** ya kimataifa. Mikutano hiyo iliwezesha kubuni uanzishwaji wa mfuko wa nyumba, ushiriki wa nchi katika kuandaa agenda za kimataifa za uendelezaji miji, upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu ya ujenzi wa nyumba kwa Shirika la Nyumba la Taifa, *Tanzania Investment Bank*, *Tanzania Mortgage Refinancing Company, AGM Holding Limited* na *Dar Village.*

*93.* ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2019/20, Wizara yangu iliahidi kusimamia na kuratibu ushirikiano wa Taasisi mbalimbali katika uendelezaji wa makazi nchini. Wizara yangu imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya Kimataifa ambapo Tanzania iliweza kushiriki katika mikutano

mitatu ya Kimataifa ikiwemo Mkutano wa kupitia mkataba wa masuala ya maliasili katika nchi za Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Nairobi Desemba, 2019, Kusanyiko la Wataalam wa Masuala ya Maendeleo ya Miji kwa kushirikiana na UN - Habitat lililofanyika Jijini Dodoma mwezi Januari, 2020, na Mkutano wa Kumi wa Jukwaa la Miji Duniani uliofanyika Abu Dhabi, Falme za Kiarabu mwezi Februari, 2020. Katika mwaka 2020/21, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu ushirikiano na Taasisi mbalimbali za Kimataifa kwa lengo la kutekeleza Malengo na mikakati inayoandaliwa na taasisi hizo.

## 5.5 MIRADI YA MAENDELEO

*94.* ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara yangu ilibuni, kutekeleza na kushiriki kwenye miradi mbalimbali. Miradi hii ni pamoja na Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi, Mradi wa Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi, Mradi wa Kuboresha Mipaka ya Kimataifa, Mradi wa Kuwezesha Ushindani katika Sekta Binafsi (Sekta ya Ardhi), Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, Bomba la Mafuta na Reli ya Kisasa.

### *Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi*

*95.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Wizara imetekeleza Program hii yenye lengo la kuhakikisha milki salama kwa wananchi. Kiasi cha shilingi bilioni **10.8** zilitolewa na Serikali kutekeleza mradi huu. Kati ya hizo, shilingi bilioni **8.36** zilitolewa ili kuwezesha upangaji, upimaji, umilikishaji, ununuzi wa vifaa na ulipaji wa fidia katika Halmashauri **27** nchini. Jumla ya viwanja **37,351** vilipimwa na hatua za umilikishaji wake zinaendelea (**Jedwali Na. 19**). Vilevile jumla ya shilingi bilioni **2.44** zilitumika kuandaa mpango kabambe wa Jiji la Dodoma, kuandaa mipangokina ya vitovu vya vijiji katika vijiji vitano (5) katika Wilaya ya Morogoro na kutoa hati za Hakimiliki za Kimila **5,845.** Vilevile vipande vya ardhi **134,239** vilitambuliwa na leseni za makazi **868** zilitolewa katika jiji la Dar es Salaam. Wizara itaendelea kuzijengea uwezo na kuziwezesha Halmashauri kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa mwaka wa fedha 2020/21.

***Mradi wa Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi***

*96.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu imetekeleza Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi *(Land Tenure Support Programme)* katika Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi kuanzia Januari, 2016 kwa kushirikiana na mashirika ya maendeleo ya Serikali za Uingereza (DFID), Sweden (SIDA), na Denmark (DANIDA). Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imekamilisha utekelezaji wa Programu hiyo mwezi Disemba, 2019. Programu hii imewezesha uandaaji wa Mipango mitatu (**3**) ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi. Mipango hiyo imebainisha mgawanyo wa rasilimali mbalimbali katika kila Wilaya. Vilevile, jumla ya mipaka ya vijiji **129** imepimwa katika Wilaya za Kilombero (**65**), Ulanga (**42**) na Malinyi (**22**). Pia, jumla ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **119** imetayarishwa katika Wilaya za Kilombero (**50**), Ulanga (**42**) na Malinyi (**27**) (**Jedwali Na. 20**). Wataalam **32** wa Halmashauri hizo wamejengewa uwezo kuhusu uandaaji na usimamizi wa Mipango hiyo. Aidha, halmashauri hizo ziliwezeshwa kwa kupatiwa vifaa vya kisasa vya upimaji na mafunzo ya matumizi yake.

*97.* ***Mheshimiwa Spika;*** Programu hii imewezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **182,126** kwa wananchi katika wilaya za Kilombero (**76,750**), Ulanga (**62,055**) na Malinyi (**43,321**). Hati hizo zimewawezesha wananchi kuzitumia kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo yenye thamani ya takriban shilingi bilioni **1.64** kutoka benki za CRDB, NMB na TADB. Sehemu kubwa ya wanufaika wa mikopo hiyo wameitumia mikopo yao kuwekeza katika shughuli za kilimo na biashara.

*98.* ***Mheshimiwa Spika;*** Programu hii pia imewezesha ujenzi wa ofisi za ardhi za Halmashauri za wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi. Vilevile, jumla ya vijiji **75** vimewezeshwa kukarabati masjala za ardhi za vijiji kwa ajili ya kutunza nakala za hati zilizoandaliwa. Wajumbe **641** wa Mabaraza ya Kata **66** na wajumbe **1,102** wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji katika vijiji **129** wamejengewa uwezo kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi. Aidha, Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya 2002 na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999

zilitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuelewa zaidi sheria na kanuni za sekta ya ardhi, ambapo nakala **15,000** zilichapishwa na kugawiwa kwa wananchi.

***Mradi wa Upimaji Mipaka ya Kimataifa***

*99.* ***Mheshimiwa Spika*;** katika kuimarisha usalama, maendeleo na ushirikiano barani Afrika, Umoja wa Afrika ulifikia makubaliano ya kuhakiki mipaka ya nchi za Afrika ili kutatua migogoro ya mipaka iliyowekwa enzi za ukoloni. Lengo la zoezi hili lilikuwa kuimarisha ulinzi na usalama katika mipaka kati ya nchi na hivyo kuepuka kutokea migogoro baina ya nchi. Azimio namba ***Assembly/AU/Dec.369 (XVII)*** lililofikiwa na Wakuu wa Nchi za Afrika huko Durban na baadaye kufuatiwa na kikao kilichofanyika Malabo, Equatorial Guinea tarehe 30 Juni hadi 1 Julai, 2011 kilizitaka nchi zote za Afrika zihakiki mipaka yake na nchi jirani ifikapo mwaka 2017. Hata hivyo, muda huo uliongezwa tena hadi mwaka 2022 baada ya utekelezaji kutokamilika.

*100.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kutekeleza azimio hilo, Wizara imeimarisha jumla ya **km. 369.9** za mpaka kati ya **km. 1,841** ya mipaka ya nchi kavu kati ya Tanzania na nchi jirani kama ifuatavyo: Tanzania na Kenya (**km. 172**), Tanzania na Msumbiji (**km.51**), Tanzania na Zambia (**km. 11.9**) na Tanzania na Burundi (**km. 135**). Aidha, Wizara inaendelea na uimarishaji wa mipaka ya nchi kavu iliyobaki na mipaka ya ndani ya maji yenye jumla ya **km. 2,086** kabla ya mwaka 2022.

***Mradi wa Kuwezesha Ushindani wa Sekta Binafsi (Sekta ya Ardhi)***

*101.* ***Mheshimiwa Spika*;** mradi huu ulianza kutekelezwa chini ya uratibu wa ofisi ya Waziri Mkuu kwa madhumuni ya kuboresha mazingira ya biashara nchini. Kwa upande wa sekta ya ardhi, mradi ulilenga:-

(i) Kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kwa kusanifu na kutengeneza mfumo unganishi wa kielektroniki wa taarifa za ardhi,

(j) (ii) Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha taarifa za ardhi, (iii) Ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upimaji na uwekaji wa alama za msingi za upimaji. Kwa kipindi cha miaka mitano, mradi umewezesha kuundwa na kusimikwa kwa mfumo wa ILMIS katika Mkoa wa Dar es Salaam. Jumla ya kumbukumbu za majalada yenye taarifa **728,370** za usajili wa hati; upimaji na umilikishaji wa ardhi yamebadilishwa kutoka mfumo wa analojia na kuwa wa kidijitali. Viwanja **239,317** viliingizwa kwenye mfumo wa ILMIS na hatimiliki za ardhi **3,868** ziliandaliwa na kutolewa kwa njia ya kielektroniki. Aidha, jumla ya miamala **254,944** ilifanyika kupitia mfumo huo. Uanzishwaji wa mfumo wa ILMIS umehusisha pia ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu za Ardhi kilichopo jijini Dar es Salaam ambacho kitatumika kuhifadhi kumbukumbu zote za ardhi kwa njia ya kielektroniki kwa nchi nzima. Vilevile, mradi huu umewezesha ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upimaji vilivyosambazwa katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na uwekaji wa mtandao wa alama za msingi ardhini.

***Ushiriki wa Wizara katika Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa***

*102.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Wizara imeendelea kushiriki katika shughuli za miradi ya Kitaifa ambayo ni Ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima, nchini Uganda mpaka Chongoleani – Tanga pamoja na Ujenzi wa Reli ya Kisasa. Katika utekelezaji wa miradi hii ya Kitaifa Wizara imeshiriki katika upangaji, upimaji na uthamini wa mali katika maeneo ya miradi.

***Mradi wa uzalishaji umeme wa Julius Nyerere***

*103.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika uendelezaji wa eneo la mradi, Wizara inaendelea kuandaa mpango wa uendelezaji wa ukanda wa mradi (Corridor Development Plan) utakaowezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika miji midogo na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji katika ukanda huu. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 jumla ya mipangokina **19** yenye viwanja **4,309** iliandaliwa katika mji mdogo wa Kisaki na upimaji unaendelea. Aidha, mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji cha Mloka wenye matumizi ya Makazi, uwekezaji, hifadhi za wanyamapori, utalii, kilimo,

misitu na vyanzo vya maji uliandaliwa. Katika mpango huo jumla ya viwanja **1,342** vimepangwa kwa ajili ya makazi (**1,110**), biashara (**217**), hoteli za kitalii (**15**) na matumizi mengine.

*104.* ***Mheshimiwa Spika;*** Shughuli nyingine zilizotekelezwa na Wizara yangu ni uwekaji alama za Upimaji ardhi nne (**4**) kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na upimaji wa hekta **1,402** za eneo la kujenga mitambo ya umeme kwenye maporomoko ya Mto Rufiji na hekta **4,711** kwa ajili ya ujenzi wa karakana na makazi ya mradi wa umeme. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara itaendelea kuratibu uandaaji wa mipangokina katika miji midogo na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji.

***Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa***

*105.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Taasisi mbalimbali imeandaa rasimu ya awali ya mpango wa uendelezaji wa ukanda wa mradi (Corridor Development Plan). Mpango huu utawezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika maeneo ya miji na mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya vijiji. Maeneo yote yaliyopendekezwa kuwa vituo vya treni na kwa matumizi mengine yanayohusiana na reli, yametambuliwa na taratibu za kisheria za kuyatangaza kuwa maeneo ya kimipangomiji zinaendelea. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara itaendelea na uandaaji wa mpango wa uendelezaji wa ukanda wa mradi, utangazaji wa maeneo ya miji midogo na uratibu wa uandaaji wa mipangokina na mipango ya matumizi ya ardhi ya kijiji.

***Mradi wa Ujenzi wa Bomba la mafuta***

*106.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Taasisi mbalimbali imeandaa pia, rasimu ya awali ya mpango wa uendelezaji ukanda wa mradi wa Bomba la Mafuta. Mpango huu utawezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika maeneo ya miji na mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya vijiji. Mamlaka za Upangaji za Wilaya za Misenyi, Bukombe, Kondoa, Handeni na Muheza zimeandaa Mipangokina katika maeneo yatakayojengwa kambi na mitambo ya mafuta. Mipangokina

iliandaliwa kama ifuatavyo: Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi viwanja **306** vimepangwa na kupimwa katika eneo la Bulifani; Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe viwanja **341** katika eneo la Bukombe mjini; Halmashauri ya Kondoa viwanja **794** katika eneo la Serya; Halmashauri ya Muheza viwanja **185** katika eneo la Komoza na viwanja **144** katika eneola Kwedigongo pamoja na eneo lenye ukubwa wa ekari **44.93** katika eneo la Tanganyika, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

**Miradi mipya ya Wizara**

*107.* ***Mheshimiwa Spika;*** ili kuongeza usalama wa milki ya ardhi nchini na kuboresha makazi, Wizara imebuni miradi miwili (**2**) ambayo inatarajiwa kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2020/21. Miradi hiyo ni: -(i) Mradi wa Kuboresha Milki utakaotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Mradi huu una lengo la kusajili milki za ardhi milioni **2.5**, kuboresha Mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu za ardhi, Ujenzi wa Ofisi za ardhi za Mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini na, kuwajengea uwezo watumishi wa sekta ya ardhi na taasisi zilizo chini ya Wizara. (ii) Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani utakaotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini kupitia Benki ya Exim. Mradi huu una lengo la kuandaa ramani za msingi za upimaji, kuimarisha vituo vya upimaji katika miji mikuu yote na kuongeza alama za msingi za upimaji, kujenga kanzidata ya taarifa za kijiografia pamoja na mifumo ya kulinda taarifa hizo kwa watumiaji na kujenga uwezo wa wataalam wa upimaji.

## 5.6 USIMAMIZI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

*108.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara yangu pia inaratibu na kusimamia shughuli za taasisi mbalimbali. Taasisi hizo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Shirika la Nyumba la Taifa; na Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro.

**Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

*109.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeendelea kusimamia na kuratibu uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na utekelezaji wake katika maeneo ya vijiji na Wilaya, kutoa

miongozo na elimu kwa umma na mamlaka za upangaji wa namna ya uandaaji wa mipango hiyo na matumizi ya ardhi. Mipango hii inasaidia kuainisha matumizi mbalimbali ya ardhi; kuwezesha ardhi kutumika kwa ufanisi na tija; kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi; na kutoa miongozo kwa mamlaka za upangaji katika kuandaa, kutekeleza na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi.

*110.* ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara kupitia Tume imeweza kuhuisha Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013–2033), kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya **7**, vijiji **692,** na mipangokina ya vitovu vya vijiji **17**, kushiriki katika miradi ya kimkakati ya kitaifa, na kushirikiana na taasisi mbalimbali katika kupanga matumizi ya ardhi nchini (**Jedwali Na. 21**). Sambamba na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, migogoro ya mipaka katika vijiji **210** vinavyopakana na Hifadhi ya Serengeti pamoja na Hifadhi za Taifa za Misitu ilitatuliwa. Aidha, kwa kipindi hicho Tume imetoa mafunzo kwa watendaji wa Halmashauri za Wilaya **83** na watendaji wa Halmashauri za Vijiji **692** katika vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya Ardhi kote nchini.

*111.* ***Mheshimiwa Spika***; vilevile Wizara yangu kupitia Tume kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wadau imeendelea kupanga, kupima na kutoa Hati za Hakimiliki za kimila kwa wananchi katika vijiji mbalimbali nchini. Kwa kipindi cha miaka mitano, Wizara kupitia Tume imewezesha upimaji na uandaaji wa hati za hakimilki za kimila **21,790** katika vijiji **42** vilivyopo katika Wilaya za Kondoa, Mvomero, Uvinza, Urambo, Magu, Mkalama, Nzega, Kibondo, Korogwe, Muheza, Monduli, Babati, Bunda na Tarime. Wizara kupitia Tume itaendelea kuhakikisha kuwepo kwa milki salama za ardhi kwa wananchi.

*112.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kukamilisha mapitio ya Programu ya Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013–2033) ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimazingira. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 Tume imekamilisha mapitio ya Programu hii. Kwa mwaka 2020/21, Wizara yangu kupitia Tume itaendelea kuhamasisha na kuratibu utekelezaji wa Mpango huo.

*113.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara kupitia Tume iliahidi kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **95** kati ya **349** katika maeneo yanayozunguka Hifadhi za Taifa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA). Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 Wizara kupitia Tume imeweza kuratibu na kusimamia uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji **94** vinavyopakana na Hifadhi za Taifa na Misitu ya Hifadhi. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara kupitia Tume itaendelea kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji katika maeneo mbalimbali nchini kwa kushirikiana na wadau pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango hiyo.

*114.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara kupitia Tume iliahidi kuwezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **236** katika Wilaya na vijiji vinavyopitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 Wizara kupitia Tume imewezesha kufanya uchambuzi wa maandalizi ya mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 236 vinavyopitiwa na Bomba la Mafuta (EACOP). Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Tume inatarajia kuwezesha upangaji matumizi ya ardhi ya vijiji **100** katika Wilaya zinazopitiwa na njia ya Bomba la Mafuta (EACOP) na Wilaya zilizo mipakani mwa nchi.

*115.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara yangu kupitia Tume itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika kanda za maeneo ya kilimo pamoja na maeneo yanayopitiwa na miradi ya kimkakati. Maeneo hayo ni pamoja na maeneo inakotekelezwa Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), Mradi wa Bomba la Mafuta (EACOP) na maeneo yenye vyanzo vya maji ya mto Rufiji unakotekelezwa mradi wa uzalishaji wa umeme (*Mwalimu Nyerere Hydro Electric Dam Project*).

**Shirika la Nyumba la Taifa**

*116.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilitekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba nchini. Katika kipindi cha miaka mitano (2015/16 hadi 2019/

20), Shirika lilitekeleza jumla ya miradi **99** ambapo kati ya hiyo, miradi **62** imekamilika. Kupitia miradi hiyo jumla ya nyumba **6,273** zilijengwa ambapo kati ya hizo, nyumba **1,617** ni za ofisi na biashara, nyumba **3,036** ni za makazi na biashara na nyumba **1,459** ni za makazi. Kati ya nyumba za makazi, nyumba **1,185** zilijengwa kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini na nyumba **274** zilijengwa kwa ajili ya watu wa kipato cha kati (**Jedwali Na. 22**). Vilevile, Shirika linaendelea kutekeleza miradi ya uendelezaji Miji ya Pembezoni *(Satellite Towns)* katika maeneo ambayo yanamilikiwa na Shirika ambayo ni Luguruni-Ubungo (**ekari 156.53**), Uvumba - Kigamboni (**ekari 202**) na Kawe- Kinondoni (**ekari 267.71**), Burka / Matevesi-Arusha Jiji (**ekari 579.2**) na eneo la Usa River - Meru (**ekari 296**).

***(NHC) lilipo eneo la Mutukula mkoani Kagera***

*117.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha miaka mitano, Shirika limeuza nyumba za makazi **1,595** kwa wateja wapya katika miradi ya nyumba za makazi iliyoko katika maeneo mbalimbali nchini. Hii ni sehemu ya nyumba za makazi **2,879** za kuuza ambazo zinajumuisha nyumba zilizokamilika na zinazoendelea kujengwa. Walengwa katika ujenzi huu ni wananchi pamoja na Halmashauri za wilaya. Kwa upande wa maeneo ya biashara na ofisi, Shirika limefanikiwa kuuza mita za mraba **2,144.70** katika miradi mbalimbali yenye maeneo maalum ya ofisi na biashara yenye jumla ya mita za mraba **50,970** katika miradi ya *Morocco Square* na *Victoria Place*.

*118.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuhamia Dodoma, katika mwaka wa fedha 2019/ 20 Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa iliahidi kuanza ujenzi wa nyumba **1,000**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Shirika limefanya upembuzi yakinifu wa mradi huu na kuwasilisha taarifa yake Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kupata idhini ya kukopa kiasi cha takriban shilingi **bilioni 20** kutoka Mfuko wa Mradi wa Nyumba ili kuanza ujenzi wa nyumba hizi. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020, Shirika lilikuwa katika hatua za mwisho za upatikanaji wa fedha hizo. Katika

mwaka wa fedha 2020/21 Shirika linatarajia kuanza ujenzi wa nyumba **400** kwa awamu ya kwanza.

*119.* ***Mheshimiwa Spika***; katika mwaka wa fedha 2019/20 Shirika linaendelea kusanifu, kusanifu na kujenga, kumalizia ujenzi, kukarabati au kusimamia ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma pamoja na ofisi za taasisi mbalimbali za Serikali nchini ikijumuisha:-

(i) Ukarabati na upanuzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Jiji la Dodoma;

(ii) Ujenzi wa ukuta wa uzio wa Bodi ya Wahandisi Tanzania Jijini Dodoma;

(iii) Ujenzi wa majengo ya ofisi zilizoko Jijini Dodoma katika eneo la Mtumba za Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Ardhi; Wizara ya Viwanda na Biashara; na Wizara ya Nishati;

(iv) Ujenzi wa jengo la ofisi ya EWURA Medeli, Jijini Dodoma;

(v) Ujenzi wa jengo la ofisi ya Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere, Musoma;

(vi) Ujenzi wa Machinjio ya Kisasa (Modern Abbatoir), Vingunguti, Dar es Salaam;

(vii) Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwl J.K. Nyerere iliyopo Kwangwa, Musoma, Mkoani Mara;

(viii) Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini iliyopo Mtwara;

(ix) Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Mji wa Mpanda, Mkoani Katavi;

(x) Ujenzi wa Majengo 44 ya Ofisi na Makazi kwa ajili ya Wakala wa Misitu Tanzania katika sehemu 17 mbalimbali nchini;

(xi) Ujenzi wa Shule ya Msingi ya watoto wenye mahitaji maalumu Mbuye, mkoani Geita; na

(xii) Usanifu na usimamizi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara ya Fedha katika eneo la Mtumba, mkoani Dodoma.

*120.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika utekelezaji wa majukumu yake, Shirika limegawanya utekelezaji katika mikakati ya muda mfupi, muda wa kati, na muda mrefu. Katika muda mfupi, Shirika limelenga kuboresha hali ya ukwasi (liquidity position) ili kuwa na fedha za kutosha kujiendesha. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kubana matumizi kwa kuondoa baadhi ya matumizi yasiyo ya lazima;

(ii) Kupunguza matumizi ya matengenezo ya nyumba bila kuathiri ubora wa nyumba;

(iii) Kutekeleza mpango wa kupanga upya baadhi ya mikopo yake (loans restructuring plan) ili kupunguza kiasi cha malipo ya mikopo kwa mwezi;

(iv) Kupangisha nyumba zote za gharama nafuu ambazo zilikuwa zimekamilika na bado hazijapata wanunuzi ili kuongeza kipato cha Shirika kutokana na kodi ya pango;

(v) Kukamilisha ujenzi wa baadhi ya miradi midogo na ya kati (ya nyumba za makazi na biashara) ambayo ilikuwa imesimama na kuipangisha na/au kuiuza ili kuongeza kipato cha Shirika; na

(vi) Kuchukuwa hatua mbalimbali za kukusanya madeni sugu ya wapangaji wa zamani na wa sasa na kuimarisha makusanyo ya kodi ya pango kwa wapangaji waliopo.

*121.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika muda wa kati, Shirika linalenga kumalizia miradi mikubwa ambayo imekwama na kuimarisha njia mbadala za mapato kwa Shirika ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Shirika. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kutekelezaji miradi **26** ya ukandarasi na ushauri nchini kote yenye jumla ya thamani ya shilingi **bilioni 86.2**;

(ii) Kupitia upya mikataba ya wapangaji na kufanya maboresho ya vipengele ili kuhakikisha kwamba Shirika linakusanya kodi na madeni. Pia, wapangaji ambao wanakiuka masharti ya ulipaji wa kodi ya pango wanachukuliwa hatua za kisheria; na

(iii) Kufanya ukaguzi wa hali ya majengo yote ya Shirika (conditional assessment) ili kupanga mpango wa kuzifanyia maboresho na matengenezo ya kudumu nyumba zake ili kuziongeza thamani.

*122.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mikakati ya muda mrefu, Shirika linajipanga zaidi katika utekelezaji wa lengo lake kuu la kuwapatia wananchi makazi bora kwa kutanua wigo wa uwekezaji wake kama ifuatavyo:-

(i) Kubadilisha malengo ya nyumba mpya zitakazojengwa kutoka kuwa za kuuza **70%** na kupangisha **30%** na kuwa za kuuza **20%** na kupangisha **80%**; na Shirika kuwekeza katika viwanda vya utengenezaji wa vifaa vya ujenzi kama vile kokoto, matofali na mabati.

*123.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Shirika liliahidi kuandaa Mipango Kabambe ya Kwala (Ruvu) na mji mpya wa Kisarawe. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020, shirika linaendelea na hatua za awali za majadiliano na Halmashauri za Wilaya za Kibaha na Kisarawe kuhusu mipango kazi ya upangaji wa maeneo ya pembezoni ya Kwala wilayani Kibaha na Vigungu Wilayani Kisarawe. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika litaendelea na utekelezaji wa mipango kabambe ya maeneo haya ya pembezoni ya Kwala na Vigungu.

*124.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Shirika liliahidi kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi **bilioni 97**. Hadi tarehe 30 Aprili, 2020, Shirika limekusanya jumla ya shilingi **bilioni 66** sawa na asilimia **69%** ya lengo. Aidha, shilingi

**bilioni 2.9** zimekusanywa kutokana na mauzo ya nyumba na shilingi **bilioni 7.3** zikiwa ni mauzo ya viwanja. Katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Shirika limepanga kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi **bilioni 98.**

**Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi**

*125.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi inalo jukumu la kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na vifaa vya ujenzi wa nyumba. Katika kipindi cha miaka mitano, Wakala iliweza kufanya tafiti mbalimbali kuhusu vifaa vya ujenzi wa nyumba ikiwemo kununua mashine **200** za kufyatua vigae vya kuezekea nyumba na tofali.

*126.* ***Mheshimiwa Spika;*** mashine hizi zilizoundwa zimewezesha kufyatua vigae mkonge **170,000** na matofali ya kufungamana **100,000** yaliyouzwa kwa bei nafuu kwa wadau mbalimbali. Pia, Wakala katika kusambaza teknolojia ya mashine hizi iliendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya mashine kwa wananchi, vikundi na Taasisi za umma na binafsi katika mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Pwani, Manyara, Lindi, Mtwara, Geita, Kilimanjaro, Kagera, Tabora na Kigoma.

*127.* ***Mheshimiwa Spika;*** kwa kuzingatia mabadiliko ya Muundo wa Wizara, Wakala umefutwa na majukumu yake yamehamishiwa Chuo Kikuu Ardhi kuanzia mwaka wa fedha 2020/21. Hatua hii inalenga kuongeza ufanisi na tija katika kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

**Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro**

*128.* ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inasimamia vyuo viwili vya Ardhi vilivyopo Tabora na Morogoro ambavyo vinatoa mafunzo ya fani mbalimbali za ardhi katika ngazi ya Astashahada (*Certificate*) na Stashahada (*Diploma*). Fani zinazotolewa ni upangaji wa miji na vijiji, upimaji wa ardhi, usimamizi wa ardhi, uthamini na usajili, urasimu ramani na sanaa, ubunifu na uchapishaji. Wizara imeendelea kuviimarisha vyuo hivi kwa kuvipatia vitendea kazi muhimu,

kuwezesha ujenzi wa majengo ya madarasa na ajira kwa wakufunzi wa elimu ili viweze kutoa ujuzi unaokidhi viwango vya taaluma zao.

*129.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha miaka mitano, Vyuo hivyo vinavyosimamiwa na Wizara vimeweza kudahili jumla ya wanafunzi **4,902**. Vilevile jumla ya wakufunzi watano (**5**) wa fani mbalimbali wameajiriwa katika vyuo hivyo. Katika kuimarisha utendaji kazi wa vyuo hivi, Wizara imeendelea kuwezesha ujenzi na ukarabati wa majengo **17** yenye vyumba vya madarasa **12,** mabweni **9** na maktaba **3**. Aidha, Mitaala ya kufundishia katika vyuo hivi imeendelea kufanyiwa mapitio kwa lengo la kuiboresha. Wizara imeendelea pia kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kukipatia Chuo cha Ardhi Tabora vifaa na mitambo ya uchapishaji na kukifanya kuwa na uwezo wa kufanya machapisho ya nyaraka zote za wizara zinazotumika katika kazi za kila siku ikiwa ni pamoja na nyaraka za umilikishaji ardhi.

*130.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara yangu iliahidi kuboresha miundombinu ya vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro ili kuviwezesha kuongeza udahili wa wanachuo. Katika mwaka wa fedha 2019/20 Chuo cha Ardhi Morogoro kimeongeza udahili kufikia wanafunzi **427** kutoka wanafunzi **274** waliodahiliwa mwaka 2018/19. Aidha, Chuo cha Ardhi Tabora kimeongeza udahili kufikia wanafunzi **1,271** mwaka 2019/20 kutoka wanafunzi **1,011** mwaka 2018/19.

*131.* ***Mheshimiwa Spika;*** ili kukidhi mahitaji ya fani mbalimbali za ardhi, vyuo vinakamilisha mapitio ya mitaala ya mafunzo yanayotolewa katika ngazi ya astashahada na stashahada za upangaji wa miji na vijiji, upimaji wa ardhi, usimamizi wa ardhi, uthamini na usajili, urasimu ramani, ubunifu na uchapishaji. Katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro iliahidi kuandaa mwongozo wa Upangaji wa Makazi Vijijini utakaowezesha utoaji wa Mafunzo ya muda mfupi yatakayowajengea uwezo watendaji wa vijiji nchini. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 Wizara imekamilisha mwongozo

huo na kuainisha aina za kozi mbalimbali zitakazofundishwa kwa watendaji wa vijiji nchini. Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutekeleza mwongozo huu kwa mwaka wa fedha 2020/21. **Natoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kushirikiana na vyuo hivyo Kutoa Mafunzo kwa watendaji wote wa vijiji ili kuimarisha utawala wa ardhi katika maeneo ya vijiji.**

### 5.7 UTAWALA NA RASILIMALI WATU

*132.* ***Mheshimiwa Spika;*** Utawala na Rasilimali Watu ni sehemu muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Usimamizi huo unafuata sera, sheria na miongozo ya Utumishi wa Umma. Katika kipindi cha miaka mitano, Wizara imeweza (i) kuhuisha muundo wa Wizara ili kuendana na mahitaji halisi na mabadiliko ya sekta ya ardhi, (ii) kuhamisha watumishi wa sekta ya ardhi waliokuwa chini ya mamlaka ya OR-TAMISEMI kuwa chini ya mamlaka ya Wizara (iii) kuwapanga upya watumishi wa sekta ya ardhi katika halmashauri mbalimbali nchini kwa uwiano, (iv) kuanzisha Ofisi za Ardhi za Mikoa na kupeleka watumishi wa sekta ya ardhi ili kusogeza huduma za ardhi kwa wananchi, (v) Kusimamia nidhamu ya watumishi (vi) Upandishaji madaraja watumishi **442** kwa kuzingatia Miundo na Kada.

*133.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kuwapanga upya watumishi wa sekta ya ardhi kwa uwiano. Katika kutekeleza azma hiyo na kwa kuzingatia agizo la Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuwahamishia watumishi wote wa sekta ya ardhi katika Wizara yangu, jumla ya watumishi **1,812** waliokuwa chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wamehamishiwa katika Wizara na kupangwa upya kwa kuzingatia uwiano na mahitaji katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri nchini.

#### *Utawala Bora na Uwajibikaji*

*134.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara ilipanga kuhuisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja ili kuongeza kasi ya utoaji wa huduma kwa ufanisi sawia na maboresho ya mifumo yanayofanyika katika Sekta ya Ardhi.

Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara imeandaa rasimu ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Katika mwaka 2020/21, Wizara itakamilisha rasimu hiyo na kusambaza nakala katika Ofisi za Ardhi nchini na kwa wadau wa sekta ya ardhi. Pia Mkataba huo utawekwa katika Tovuti ya Wizara.

*135.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara iliahidi kutekeleza mkakati wa kupambana na viashiria vya rushwa kwenye Sekta ya Ardhi kama sehemu ya mikakati ya kuboresha huduma zinazotolewa kwa umma. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Mafunzo kuhusu maadili ya utumishi wa umma na mapambano dhidi ya rushwa yalitolewa kwa viongozi na watumishi pamoja na kula kiapo cha ahadi ya uadilifu. Aidha, watumishi **47** waliotuhumiwa kwa rushwa taarifa zao ziliwasilishwa kwa mamlaka husika kwa hatua.

*136.* ***Mheshimiwa Spika*;** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara iliahidi kuajiri watumishi **56** kadri vibali vitakavyokuwa vinatolewa. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara imeajiri jumla ya watumishi **42** wa kada mbalimbali kati ya hao, watumishi tisa **(9)** ni wa sekta ya ardhi na **33** wa kada saidizi. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara imepanga kuajiri watumishi wa kada mbalimbali **270** kadri vibali vya ajira vitakavyokuwa vinatolewa ikiwa ni pamoja na kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa sababu mbalimbali ikiwemo kustaafu.

***Mafunzo kwa Watumishi***

*137.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliahidi kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi **304** kwa kuzingatia mahitaji ya mafunzo. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020, Wizara yangu imewezesha utoaji wa mafunzo kwa watumishi **154.** Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara inaahidi kuwezesha utoaji wa mafunzo kwa watumishi **700** kwa kuzingatia mahitaji ya mafunzo ya watumishi wa Wizara na watumishi wa sekta ya ardhi waliohamishiwa Wizarani kutoka OR- TAMISEMI.

***Habari na Elimu kwa Umma***

*138.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara iliahidi kuendelea na utaratibu wa upashanaji habari

na elimu kwa umma kuhusu masuala yanayohusu Sekta ya Ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Wizara iliandaa na kusambaza nakala **500** za kijarida cha Mwongozo wa Sheria za Mahakama za Ardhi, nakala **3,000** za vipeperushi (fliers) na nakala **1,500** za machapisho mengine kuhusu shughuli za Sekta ya Ardhi. Aidha, vipindi **131** vya televisheni na redio kuhusu shughuli za Wizara viliandaliwa na kurushwa kupitia mitandao ya kijamii. Pia elimu ilitolewa kupitia mitandao ya kijamii ikiwemo *facebook, instagram, youtube* na *twitter* na magazeti mbalimbali nchini. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea na utaratibu wa upashanaji habari na elimu kwa umma kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi.

## 6.0 SHUKRANI

*139.* ***Mheshimiwa Spika;*** naomba kumalizia hotuba yangu kwa kumshukuru Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuiongoza na kuisimamia Wizara hii na kwa maelekezo yake yaliyochochea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi chote cha Awamu hii. Kwa kipekee napenda kuwashukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo yao yaliyoboresha utendaji wa Wizara yangu. Aidha, nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu kutoka katika Wizara mbalimbali tulioshirikiana katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa lengo la kuwahudumia watanzania. Nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa umahiri wenu katika kuongoza vikao vya Bunge. Napenda pia, kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Bunge na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango, maoni na ushauri wenu kwa kipindi chote cha Bunge hili.

*140.* ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kwa namna ya kipekee kutumia fursa hii kumshukuru Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Angelina Sylvester Lubala Mabula (Mb.), kwa kunisaidia katika

kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Katibu Mkuu Bi. Mary Gasper Makondo, Naibu Katibu Mkuu Bw. Nicholas Mkapa, Dkt. Stephen Nindi Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Dkt. Maulid Banyani Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, napenda kuwashukuru Wakuu wa Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro pamoja na watumishi wote wa Wizara, kwa kuendelea kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kuhudumia umma wa Watanzania bila ubaguzi.

*141.* ***Mheshimiwa Spika;*** vilevile, napenda kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Ardhi ikiwa ni pamoja na Mamlaka za Upangaji, na wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na nje ikijumuisha Benki ya Dunia, Jamhuri ya Korea ya Kusini, Mashirika ya Maendeleo ya DFID, SIDA na DANIDA. Wizara yangu inatambua na kuthamini michango inayotolewa na wadau hawa katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

*142.* ***Mheshimiwa Spika;*** napenda pia, kutoa shukrani kwa wadau mbalimbali wakiwemo Wakuu wa Mikoa kwa kufanikisha upatikanaji wa Ofisi za Ardhi za Mikoa. Aidha, napenda kuzishukuru kampuni binafsi na Taasisi za Fedha zikiwemo *NMB, CRDB, NBC, Azania Bank, Stanbic Bank na TPB* kwa michango yao. Pia nizishukuru taasisi binafsi na mamlaka mbalimbali tulizoshirikiana nazo katika kutekekeza majukumu ya Wizara ikiwemo Bodi za Kitaaluma za Wataalamu wa Mipangomiji, Wathamini na Wapima Ardhi na wamiliki wa kampuni za Upangaji na Upimaji. Vilevile, ninawashukuru wajumbe wa Kamati ya Ugawaji Ardhi, Baraza la Kitaifa la Ushauri wa Ardhi na Wenyeviti na Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

## 7.0 HITIMISHO

*143.* ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kuhitimisha kwa kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara yangu imedhamiria kuendelea kufanya mageuzi kwa kutumia

teknolojia za kisasa katika utoaji wa huduma za ardhi. Mageuzi hayo yanalenga kuwawezesha wananchi kiuchumi na kijamii, kuimarisha usalama wa milki za ardhi pamoja na kuongeza thamani ya ardhi na hivyo kuongezeka kwa pato la Taifa.

## 8.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2020/21

***Makadirio ya Mapato***

*144.* ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi **bilioni 200** kutokana na kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na shughuli za Sekta ya Ardhi kwa kutekeleza mikakati ambayo imeainishwa katika hotuba hii.

***Makadirio ya Matumizi***

*145.* ***Mheshimiwa Spika;*** ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu niliyoyaeleza katika hotuba hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu **48**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03**: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kama ifuatavyo: -

***Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi***

| **AINA** | **MAPATO** | **SHILINGI** |
|---|---|---|
| A | Mapato ya Serikali | **200,000,000,000** |
| | **AINA YA MATUMIZI** | **FEDHA** |
| B | Matumizi ya Kawaida: | |
| | Matumizi ya Mishahara | 19,496,335,00 |
| | Matumizi Mengineyo | 27,482,305,00 |
| | **Jumla Ndogo** | **46,978,640,000** |
| C | Matumizi ya Maendeleo: | |
| | Fedha za Ndani | 16,300,000,00 |
| | Fedha za Nje | 66,300,839,00 |
| | **Jumla Ndogo** | **82,600,839,000** |
| | **JUMLA KUU (B+C)** | **129,579,479,000** |

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo shilingi **129,579,479,000/=**.

***Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi***

| AINA | AINA YA MATUMIZI | FEDHA |
|---|---|---|
| A | Matumizi ya Mishahara | 1,509,468,000 |
| B | Matumizi Mengineyo | 979,822,000 |
| C | Matumizi ya Maendeleo | 1,500,000,000 |
| | **Jumla** | **3,989,290,000** |

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni shilingi **3,989,290,000/=**.

*146.* ***Mheshimiwa Spika,*** jumla kuu ya fedha zote zinazoombwa kwa Wizara (Fungu **48** na Fungu **03**) ili muweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi **133,568,769,000/=**.

*147.* ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii yameambatishwa majedwali ambayo yanafafanua kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Wizara. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni ***www.lands.go.tz.***

148. Mheshimiwa *Spika,* naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa William Lukuvi kwa hotuba yako nzuri kabisa iliyojaa taarifa njema sana kwa Watanzania. Hakika pamekuwa na mabadiliko makubwa kwenye Wizara hii, nasi sote ni mashuhuda wa haya ambayo Mheshimiwa Waziri ameelezea, usumbufu mkubwa sasa wa kufuata hati wapi, mbali huko, sasa unazidi kupungua. Kwa kweli tunaona mwanga sasa kwenye Wizara hii ambayo ilikuwa ikilalamikiwa sana huko nyuma. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wasaidizi wenu wote kwa kazi nzuri.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati awakilishe ile hotuba ya Kamati, Mheshimiwa Kemilembe, karibu. *(Makofi)*

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakushukuru kwa fursa. Naomba taarifa hii iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwatumikia Watanzania. Kipekee kabisa nachukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo ameongoza nchi kwa uzalendo na ujasiri wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wote na Watendaji wa Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi mkubwa. Bunge la Kumi na Moja litakumbukwa kwa mambo mengi mazuri ikiwemo ujenzi wa Sekondari ya Wasichana eneo la Kikombo pamoja na uamuzi wako wa kijasiri wa kulifanya Bunge letu kuwa Bunge Mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa michango na ushauri wao kwangu na kwa Serikali vikiwa ndiyo nguzo na utendaji bora wa Kamati hii. Naomba majina yao yatambuliwe katika *Hansard* kama ilivyoorodheshwa katika taarifa iliyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa William Lukuvi; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula; Katibu Mkuu, Ndugu Mary Gaspar Makonda; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Nicholous Mkapa pamoja na Watendaji

wote wa Wizara kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani na pongezi hizo, sasa kwa mujibu wa Kanuni ya ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inajumuisha mafungu mawili ya kibajeti ambayo ni Fungu Na. 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu Na. 3 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa upande wa hali ya upatikanaji wa fedha; katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya shilingi bilioni 57.4. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 33.1 ilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 24.2 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya maendeleo iliyotengwa, shilingi bilioni 18 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 6.2 ni fedha za nje. Katika uchambuzi wa Kamati ilibaini kwamba hadi kufikia Februari, 2020 Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 27.7 ikiwa ni sawa na asilimia 48.3 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni 20.4 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 61.6 ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo na shilingi bilioni 7.2 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 28 ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mirdi hiyo. Katika bajeti ya maendeleo iliyopokelewa, shilingi bilioni 4.6 ni fedha za ndani sawa na asilimia 25.9 na shilingi bilioni 2.6 ni fedha za nje sawa na asilimia 41 ya mapokezi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ziliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 17 Machi, 2020 Tume ilipokea jumla ya shilingi bilioni 1.1 sawa na asilimia 53 ya fedha iliyoidhinishiwa. Kwa upande wa bajeti ya maendeleo, Tume iliidhinishiwa shilingi bilioni tatu na hadi kufikia tarehe 17 Machi, 2020 Tume ilikuwa bado haijapokea fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa upatikanaji wa fedha hususan utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa namna yoyote Kamati ilitarajia kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020 walau nusu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge iwe imepokelewa na Wizara ili kutekeleza miradi iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ilijiwekea malengo ya kukusanya jumla ya shilingi bilioni 180. Hadi kufikia Februari, 2020 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 72.8 sawa na asilimia 48 ya malengo hayo. Kamati imebaini kwamba kasi ndogo ya ukusanyaji imechangiwa na mwamko mdogo wa wananchi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na ukusanyaji hafifu wa mapato katika Wizara hii kulingana na malengo waliyojiwekea. Aidha, Wajumbe hawakuridhishwa na sababu zilizotolewa na Wizara kuhusu mwamko mdogo wa wananchi uliosababisha makusanyo kuwa hafifu. Kamati ilitegemea kwamba wakati Wizara inajiwekea malengo ya ukusanyaji iwe imejipanga katika kuhakikisha kuwa elimu ya kutosha inatolewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ya pango la ardhi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilikuwa na lengo la kupata fedha jumla ya shilingi milioni 706 katika mwaka wa fedha 2019/2020. Hadi kufikia tarehe 17 Machi, 2020, Tume ilikuwa imepata kiasi cha shilingi milioni 446 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato vya Tume hiyo, sawa na asilimia 63.3 ya malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilipanga kutembelea ili kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020 katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Lengo la ukaguzi huo ilikuwa ni kujionea hali halisi ya utekelezaji wake kulinga na bajeti iliyotengwa katika miradi iliyokaguliwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo katika Mkoa wa Mara, Mwanza, Tabora na Shinyanga, kati ya tarehe 12 mpaka tarehe 18 Machi, 2020. Maelezo kuhusu matokeo ya ukaguzi wa miradi hiyo yanapatikana katika ukurasa wa nane wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020; kutokana na matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ya Kamati ina maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kandarasi za ujenzi na ushauri elekezi. Kamati imebaini kwamba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekuwa ikitumia Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo baadhi ya miradi iliyokaguliwa na Kamati katika mwaka wa fedha 2019/2020. Hata hivyo, Wakala huu umekuwa ukishindwa kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu kutokana na ama kuzidiwa na idadi ya miradi waliyokabidhiwa kushirikiana na Wizara au kwa sababu nyingine za kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, miradi hiyo imekuwa ikisuasua na mingine kutokukamilika kwa wakati kama ambavyo ilishuhudiwa katika miradi ya ujenzi wa Maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora katika ukurasa wa nane wa taarifa hii. Kamati inashauri kwamba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ifanye tathmini iwapo kuna ilazima wa kuendelea kutumia Wakala huyu katika miradi hiyo na ikiwezekana kuja na mkakati mbadala wa

kandarasi za ujenzi na ushauri elekezi wa miradi yote ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtiririko wa fedha iliyotengwa kwa miradi. Katika miradi yote ambayo Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi changamoto kubwa imekuwa ni kutotolewa kwa wakati na kwa ukamilifu kwa fedha za bajeti za maendeleo iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha husika. Manufaa ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii yataonekana pale tu Serikali itakapotoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati na kwa ukamilifu ili kukamilisha miradi inayosimamiwa na inayoendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 200. Kiwango hiki ni ongezeko la asilimia 11 ya makadirio ya makusanyo ya Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha ambapo Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 180. Kwa upande mwingine Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imepanga kukusanya jumla ya shilingi milioni 600 sawa na kiwango kama hicho kilichopangwa kukusanya katika mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara inaomba kuidhinishwa shilingi bilioni 46.97 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ukilinganisha na shilingi bilioni 33.1 zilizopangwa katika mwaka wa fedha unaoisha. Kati ya fedha zinazoombwa, shilingi bilioni 19.4 ni kwa ajili ya mishahara ambayo imeongezeka kwa takribani shilingi bilioni mbili ukilinganisha na bajeti ya mishahara ya mwaka unaoisha; na shilingi bilioni 27.4 inayoombwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ikiwa imeongezeka kwa takribani shilingi bilioni 11.7.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.2 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa kuidhinishiwa, shilingi

bilioni 1.5 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 979 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 82.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mbalimbali ya Wizara ukilinganisha na shilingi bilioni 24.2 zilizoidhinishwa mwaka wa fedha 2019/ 2020. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 241. Kati ya fedha inayoombwa shilingi bilioni 16.3 ni fedha za ndani ikilinganishwa na shilingi bilioni 18 zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha unaoisha na shilingi bilioni 66.3 ni fedha za nje ikilinganishwa na shilingi biloni 6.2 zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba ongezeko la bajeti ya mpango wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 inatokana na Wizara kupanga utekelezaji wa miradi miwili inayotarajiwa kupata fedha za nje kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Korea Kusini. Mradi wa kwanza ni *Land Tenure Improvement Project* ambapo Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 37.1. Ambapo kati ya hizo shilingi bilioni 2.3 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 34 ni fedha za nje ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili ni *The National Spatial Data Infrastructure Project* ambapo Wizara inaomba Bunge liidhinishie shilingi bilioni 31.9. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 500 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 31.4 ni fedha za nje kwa ajili ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Korea.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kubuni miradi hii kwa kuwa itakuwa ni mwanzo wa utekelezaji wa maoni ya mara kwa mara ya Kamati ya kwamba Serikali inapaswa kuwa na mkakati wa Kudumu wa kuhakikisha kuwa kila kipande cha nchi hii kinapangwa kupimwa na kumilikishwa. Hatua hii itapunguza migogoro ya ardhi nchini. Hata hivyo, Kamati inadhani kwamba Wizara kwa kushirikiana na Hazina inapaswa kuwa na mpango kabambe wa upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini bila kutegemea fedha za nje au hisani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi ya mradi wa upangaji wa matumizi ya ardhi. Kiasi hiki ni pungufu ya asilimia 50 ukilinganisha na shilingi biloni tatu zilizotengwa mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuwa kiwango kilichotengwa kutekeleza miradi ya maendeleo ni pungufu, ni dhahiri kwamba baadhi ya majukumu hayo hayatatekelezeka kwa ufanisi, Kamati inaishauri Serikali itenge fedha za kutosha kutengeneza miradi ya Tume ili iweze kufikia malengo yake.

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe maoni na ushauri wa Kamati. Kwa upande wa Muundo wa Bajeti na hali ya upatikanaji wa fedha; kwa kuwa Kamati imebaini kuwepo na mtiririko usioridhisha wa mapato katika bajeti inayotengwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, hivyo basi, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuona bajeti zijazo zinaakisi hali halisi ya mapokeo ya fedha. Kwa kufanya hivyo, Wizara itakuwa na uwezo wa kupanga kulingana na vipaumbele na utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba kumekuwepo na mwenendo usioridhisha wa kutotolewa fedha za maendeleo kwa wakati. Kamati inashauri kwamba Wizara ya Fedha itoe fedha kwa wakati na kwa ukamilifu ili Wizara iweze kutekeleza kwa ukamilifu mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina taarifa kuhusu uamuzi wa Serikali kurudisha kesi na migogoro ya ardhi katika Mahakama ambapo awali ilikuwa inashughulikiwa na Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya. Hatua hii inatokana na ukweli kwamba mabaraza yaliyokuwepo ni machache na pia

kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika utendaji wa mabaraza hayo ikiwa ni ukiukaji wa maadili kwa baadhi ya watendaji, elimu ndogo na pia kuwa na watumishi hao wasio waajiriwa wa Kudumu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba Serikali inapaswa kukaa kwa pamoja na kushirikiana na kuja na namna bora ambayo itawezesha baadhi ya Kanuni za uendeshaji wa mabaraza hayo zitumike katika vyombo vya Mahakama ili kuwe na mazingira rafiki ya kusikiliza mashauri yanayowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa mabadiliko haya yatasababisha kubadilika kwa sheria mbalimbali za ardhi, Kamati inashauri kwamba wakati wa mabadiliko haya ya sheria *(Miscellaneous Amendments)* Bungeni, Kamati zitakazokuwa na mamlaka ya kushughulika na masuala ya ardhi, sheria na Serikali za Mitaa zishirikishwe kikamilifu ili kupata maoni yao katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri na kusisitiza Wizara kuja na mpango madhubuti wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi ambapo itatumia fedha za ndani. Kwa kuzingatia hali ya uchumi wa dunia kwa sasa, ni wakati muafaka nchi yetu ikatambua kwamba ardhi ndiyo rasilimali kuu katika uchumi wa Taifa lolote. Hivyo basi, Serikali iweke kipaumbele katika sekta hii kwa kuitengea fedha za kutosha ili tuweke mipango ya muda mfupi na mrefu ya matumizi ya ardhi yetu ambayo mahitaji yanaongezeka kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako lipokee taarifa hii ili ijadili kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii ina sehemu kuu tano (5) ambapo Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya Pili inabainisha Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka Wa Fedha 2019/2020. Sehemu ya Tatu ni Uchambuzi wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Sehemu ya Nne ya taarifa hii ni maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati na Sehemu ya Tano ni Hitimisho.

### 1.2 Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (6) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinatoa mamlaka mahsusi kwa Kamati hii kushughulikia Bajeti za Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inajumuisha Mafungu mawili (2) ya kibajeti ambayo ni yafuatayo:-

**i) Fungu 48** - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**ii) Fungu 03** - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika**, jukumu la uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hiyo lilitanguliwa na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/ 2020. Ukaguzi huo ulifanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI YA KWA MWAKA FEDHA 2019/2020

### 2.1 Hali ya Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, **Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi** iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu bajeti ya **shilingi bilioni 57.43**. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 33.15** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi bilioni 24.28** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika bajeti ya maendeleo iliyotengwa, **shilingi bilioni 18** ni fedha za ndani na shilingi **bilioni 6.28** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2020 Wizara ilipokea jumla ya **shilingi bilioni 27.74** ikiwa ni sawa na **asilimia 48.3** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kati ya fedha zilizopokelewa, **shilingi bilioni 20.45** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 61.68** ya bajeti iliyotengwa kwa shughuli hiyo na shilingi **bilioni 7.28** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ikiwa ni sawa na **asilimia 29.98** ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Katika Bajeti ya Maendeleo iliyopokelewa, **shilingi bilioni 4.66** ni fedha za ndani sawa na **asilimia 25.9** na shilingi **bilioni 2.63** ni fedha za nje sawa na **asilimia 41.8** ya mapokezi.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, **Fungu 03 - Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi** iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 2.24** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia tarehe 17 Machi, 2020 Tume ilipokea jumla ya **shilingi 1.18** sawa na **asilimia 53** ya fedha iliyoidhinishwa. Kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo, Tume iliidhinishiwa **shilingi bilioni 3** na hadi kufikia tarehe 17 Machi, 2020 Tume ilikuwa bado haijapokea fedha za maendeleo kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi yake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa upatikanaji wa fedha hususan za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kwa namna yoyote, Kamati ilitarajia kwamba kufikia Robo ya Tatu ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 walau nusu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge iwe imepokelewa na Wizara kutekeleza miradi hiyo.

**2.2 Ukusanyaji wa Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilijiwekea malengo ya kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 180**. Hadi kufikia Februari, 2020 Wizara ilikuwa imekusanya **shilingi bilioni 72.8** sawa na **asilimia 48** ya malengo hayo. Kwa maelezo ya Wizara, kasi ndogo ya ukusanyaji ilichangiwa na mwamko mdogo wa wananchi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na ukusanyaji hafifu wa mapato katika Wizara hii kulingana na malengo waliyojiwekea. Aidha Wajumbe hawakuridhishwa na sababu zilizotolewa na Wizara kuhusu mwamko mdogo wa Wananchi uliosababisha makusanyo kuwa hafifu. Kamati ilitegemea kwamba, wakati Wizara inajiwekea malengo ya ukusanyaji, iwe imejipanga katika kuhakikisha kuwa elimu ya kutosha inatolewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ya pango la ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, **Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi** ilikuwa na lengo la kupata fedha jumla ya

**shilingi milioni 706** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hadi kufikia tarehe 17 Machi, 2020, Tume ilikuwa imepata kiasi cha **shilingi milioni 446** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato vya Tume hiyo sawa na **asilimia 63.2** ya malengo waliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na Taarifa ya Tume kuhusu ukusanyaji wa mapato kulingana na malengo waliyojiwekea.

### 2.3 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti husika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako kwamba, katika masuala yaliyotolewa ushauri, yapo ambayo yamezingatiwa kikamilifu, baadhi yanaendelea kuzingatiwa na mengine hayajazingatiwa kikamilifu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti. Kwa muhtasari, naomba niweke msisitizo katika machache kama ifuatavyo:-

a) Kamati ilishauri Serikali ipitie upya Sheria iliyoanzisha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili ifanyiwe marekebisho na kuifanya Tume hiyo kuwa Mamlaka. Hatua hii, itaipa Tume nguvu ya kusimamia upimaji, upangaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Pamoja na kwamba Tume imekamilisha rasimu ya andiko la kuibadili Tume kuwa Mamlaka, Kamati ilitaarifiwa kwamba rasimu hiyo bado inafanyiwa uchambuzi na mapitio na wadau. Kamati haijaridhishwa na kasi ya Wizara katika hatua za kutekeleza ushauri huu kwa sababu jambo hili limekuwa la muda mrefu.

b) Kamati ilishauri Wizara isimamie mikakati ya makusanyo iliyojiwekea ili kufikia malengo ya makusanyo kwa mwaka

ifikapo Juni, 2020. Pamoja na jitihada ambazo Wizara imefanya kutekeleza ushauri huu, bado Kamati haijaridhishwa na kasi ya ukusanyaji mapato.

c) Kamati ilishauri Serikali iandae mkakati wa kitaifa utakaohakikisha kuwa inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini. Wizara bado imekuwa inatenga fedha wastani wa shilingi bilioni 7.45 kwa mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa ushauri huu katika halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, Wizara ilijinasibu kwamba inapanga kuendelea kutenga fedha katika bajeti kila mwaka ili kuzifikia halmashauri nyingi zaidi ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya **shilingi bilioni 7** zimetengwa kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi.

Hata hivyo, fedha hiyo inayotengwa kwa mwaka haiwezi kutosha kutekeleza ushauri huu kwa haraka. Katika maelezo yao kwa Kamati, Wizara ilitoa maelezo kwamba, kupitia Programu ya Taifa ya Upangaji, Upimaji na Umilikishaji ardhi Serikali imebuni miradi miwili (2) ya kimkakati ambayo itatekelezwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na pamoja na *Exim Bank* ya Korea Kusini.

d) Kamati ilishauri Serikali iharakishe mchakato wa kukamilisha Sera ya Taifa ya Nyumba itakayotoa mwongozo wa kusimamia Sekta ya Nyumba. Hadi kufikia Februari, 2020, Wizara ilikuwa imekamilisha Rasimu ya Sera ya Nyumba na ilikuwa inaboreshwa kwa kuzingatia maoni ya wadau yaliyowasilishwa. Kamati inatoa rai kwa Wizara kuhakikisha kuwa Sera hiyo inakamilika ili kutoa fursa ya hatua nyingine muhimu kufuata, ikiwemo kutunga sheria mbalimbali ambazo zitasimamia sekta hiyo.

### 2.4 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipanga kutembelea ili kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 katika

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Lengo la ukaguzi huo likuwa ni kujionea hali halisi ya utekelezaji wake kulingana na bajeti iliyotengwa katika kila mradi uliokaguliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo katika mikoa ya Mara, Mwanza, Tabora na Shinyanga kati ya tarehe 12 – 18 Machi, 2020. Miradi iliyofanyiwa ukaguzi wa utekelezaji wake ni ifuatayo:-

### 2.4.1 Mradi Na. 6327 – Ujenzi wa Maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora (Arita)

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Bunge lilitenga jumla ya **shilingi bilioni 1.1** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora. Mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA Master Plan 2010 – 2020) ambao pamoja na mambo mengine, ulilenga kukiwezesha chuo hicho kuweza kudahili wanachuo 1,500 ifikapo Mwaka 2020 ili kupunguza uhaba wa watendaji katika sekta ya Ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, Mkataba wa Ujenzi wa mradi huu ulisainiwa baina ya Serikali na Mzabuni mnamo Juni, 2014 na ujenzi ukaanza Julai, 2014. Mradi ulikua unatekelezwa na mzabuni chini ya usimamizi wa Mshauri na Msimamizi wa mradi ambaye ni Meneja wa Mkoa wa Tabora wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) pamoja na Mshauri Msaidizi Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA). Muda wa Mkataba ulitarajiwa kuwa kipindi cha majuma arobaini na nne (44) na kazi ilitarajiwa kukamilika Mei, 2015.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inafanya ziara ya ukaguzi katika mradi huu, ilibaini kwamba ujenzi umesimama tangu Julai, 2014. Kazi ambazo hazijakamilika ni pamoja na kuezekwa kwa jengo, miundombinu ya maji pamoja na kuwekwa kwa milango na madirisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji Wizara sababu za kukwama mradi huukwa zaidi ya miaka sita, na majibu ya Serikali yalikuwa kwamba mradi huo ulikutana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na zifuatazo:-

a) kutopatikana kwa wakati kwa fedha za kutekeleza hatua mbalimbali za mradi;

b) kukosekana kwa kibali cha ujenzi (kwa kuzingatia *Geo Technical Investigation Report*) ambayo ingeweza kumpata mshauri mwenye uwezo wa kusanifu mfumo wa sakafu na nguzo;

c) kuchelewa kupatikana kwa mkandarasi msaidizi wa umeme katika jengo;

d) ucheleweshwaji wa malipo katika madai mbalimbali ya Mkandarasi; na

e) madai mapya ya Mkandarasi ya shilingi milioni 550 kutokana na ongezeko la gharama za ujenzi na bei ya soko kinyume na masharti ya Mkataba ambao haukupaswa kuwa na mabadiliko ya bei *(fixed contract)*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kwamba, kati ya Oktoba, 2016 na Juni, 2019 uongozi wa chuo umefanya jitihada mbalimbali ikiwemo kufanya vikao na mkandarasi pamoja na washauri waelekezi ili kupata suluhisho la kuunusuru mradi huu. Aidha, katika kipindi hicho, Kamati imetaarifiwa kwamba Wizara imefanya mawasiliano na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupitia upya mkataba kwa lengo la kuongeza muda kuwezesha mkandarasi kukamilisha kazi ya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo hayo ya Serikali, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa jumla wa mradi huu. Wajumbe wa Kamati walionesha masikitiko yao baada ya kujionea hali halisi ya mradi ukilinganisha na umuhimu, thamani na kipaumbele cha mradi katika sekta ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza kwamba, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ifanye ukaguzi maalum *(special audit)* ili kubaini iwapo kuna uzembe au/na ubadhirifu katika utekelezaji wa mradi huu. Aidha, ikithibitika kuwepo kwa

uzembe au/na ubadhirifu, hatua stahiki za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa wote waliohusika kusababisha mradi huu usikamilike kwa wakati.

### 2.4.2 Mradi Na. 2326 – Upangaji, Upimaji na Umilikaji Ardhi

**Mheshimiwa Spika**, Mradi Na. 2326 unahusu Upangaji, Upimaji na Umilikishaji Ardhi unatekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini kwa lengo la kuziwezesha kwa kuzikopesha halmashauri hizo fedha kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Katika Mwaka wa Fedha 2019/ 2020 Bunge liliidhinisha kiasi cha **shilingi bilioni 8** ili Wizara itoe mikopo kwa Halmashauri mbalimbali kutekeleza mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichagua kutembelea ili kukagua utekelezaji wa mradi huu katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Mkoa wa Shinyanga na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela katika Mkoa wa Mwanza kati ya halmashauri 24 zilizonufaika na mradi huu. Lengo la kutembelea miradi hii ilikuwa ni kujionea mafanikio ya mradi huu kulingana na fedha inayotolewa kwa halmashauri hizo.

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Kamati ilipokea taarifa kuhusu mradi huo kwa fedha iliyotolewa na Wizara kwa halmashauri hiyo ilikuwa kiasi cha **shilingi milioni 240** na mpaka kufikia Februari, 2020 Halmashauri hiyo ilikuwa imepanga, imepima na kumilikisha viwanja. Aidha, kufikia kipindi hicho, halmshauri hiyo imefanikiwa kurejesha fedha yote ya mkopo kwa Wizara. Mafanikio haya pia yalionekana katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, ambayo ilipokea mkopo wa **shilingi bilioni 1.55** kutekeleza mradi na mpaka kufikia Februari, 2020 halmashauri hiyo ilikuwa imepanga, imepima na kumilikisha viwanja na kurejesha fedha yote ya mkopo kwa Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo na nia njema ya Wizara kuziwezesha halmashauri nchini kupanga maeneo yao, Kamati imebaini kwamba, kuna changamoto mbalimbali katika Mradi huu ambazo zinapunguza ufanisi wa

mradi. Changamoto kubwa ambayo Kamati imebaini ni kiwango kidogo cha fedha ambacho kinatengwa na Wizara kutekeleza mradi huu kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa bajeti unaonesha kwamba katika miaka mitatu iliyopita, Wizara imekuwa ikitenga wastani wa **shilingi bilioni 7.85** kwa mwaka ili kuzikopesha halmashauri ambazo zimekidhi vigezo ili ziweze kutekeleza mradi huo. Kwa hali ilivyo sasa, itaichukua Wizara walau miaka minne (4) kuweza kuzifikia halmashauri zote nchini wakati huo huo ujenzi holela ukiwa bado unaendelea. Aidha, mwenendo wa mapato wa bajeti ya maendeleo pia unaonesha kwamba fedha inayotengwa haitolewi kwa ukamilifu. Kwa mwenendo huu, inaweza ikalichukua Taifa miaka mingi kufanikisha zoezi la Upangaji, Upimaji na Umilikishaji wa Ardhi iwapo Wizara haitachukua jitihada za makusudi za ama kuziwezesha halmashauri, au Wizara yenyewe kutekeleza zoezi hili kwa **asilimia 100**.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine ambayo ilibainika ni kwamba, katika **halmashauri 24** ambazo zimepokea fedha za mkopo kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili kutekeleza mradi huu, ni **halmashauri 5** tu ambazo zimefanikiwa kurejesha fedha za mkopo kwa asilimia 100%. Halmashauri hizo ni Mbeya CC, Shinyanga MC, Bariadi TC, Ilemela MC na Kahama DC. Hali hii ya marejesho hafifu ya fedha za mkopo kutekeleza mradi huu inaweza kuzorotesha jitihada za Wizara kukopesha Halmashauri nyingine ambazo zimekidhi vigezo vya kupokea fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine iliyobainiwa na Kamati ni mauzo hafifu ya viwanja vilivyopimwa katika mradi huu katika halmashauri mbalimbali. Mathalani, kwa Fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 katika halmashauri 24 zilizonufaika na mradi, Wizara ilikuwa na lengo kuhakikisha mradi unazalisha **viwanja 40,651**. Hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2020 jumla ya **viwanja 26,485** vilipimwa na kusajiliwa sawa na **asilimia 65.2** ya lengo. Kati ya hivyo, **viwanja 4,221** vimemilikishwa sawa na **asilimia 15.9** tu ya viwanja vilivyopimwa.

**Mheshimiwa Spika**, ni vyema Wizara kwa kushirikiana na halmashauri ambazo zinapokea mkopo kwa ajili ya kutekeleza mradi huu zikafanya tathmini ya soko iwapo lengo ni kurejesha mkopo kwa wakati. Lakini iwapo lengo ni kuwa na halmashauri zilizopangwa na kupimwa, Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) iwe na Mpango wa Bajeti ya Maendeleo kwa kutumia fedha za ndani ili kuwa na ardhi iliyopangwa na kupimwa, na umilikishaji ukafanyika taratibu na kwa uendelevu *(sustainable land allocation strategies)*.

### 2.4.3 Mradi Na. 2324 – Kuimarisha Mipaka ya Kimataifa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Mradi Na. 2324 – Kuimarisha Mpaka wa Kimataifa wa Tanzania na Kenya, Sirari katika Mkoa wa Mara. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Bunge lako lilitenga **shilingi bilioni 5.4** ili kuimarisha mipaka ya nchi yetu katika maeneo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Mpaka wa Tanzania na Kenya una urefu wa kilometa 760 za nchi kavu kutoka ufukweni mwa Ziwa Victoria hadi ufukweni mwa Bahari ya Hindi Jasini (Tanzania) na Vanga (Kenya) na pia una urefu wa kilometa 59.71 ndani ya maji kwenye Ziwa Victoria na kilomita 401 ndani ya Bahari ya Hindi. Tangu uhuru mwaka 1961, mpaka huu umekaguliwa mwaka 2001 na kubaini kuwepo kwa alama (*pillars*) za mpaka 342 ambazo hazijaharibiwa na alama 123 zinazohitaji kukarabatiwa. Kazi ya kuimarisha mpaka huu ilianza rasmi baada ya makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Kenya kupitia vikao viwili (2) vya wataalam (JTC) vilivyofanyika Migori na Naivasha mwaka 2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, katika awamu ya kwanza, kazi ya uimarishaji wa mpaka ilikubaliwa ifanyike katika kipande cha mpaka wa nchi kavu chenye urefu wa kilometa 238 kuanzia alama BP Mwishoni iliyopo Ziwa Victoria hadi alama BP 33 NEW iliyopo Ziwa Natron. Hadi sasa kazi ya kuimarisha mpaka huu imefanyika kwa **kilometa 172** kutoka alama BP Mwishoni iliyoko kando ya Ziwa Victoria kuelekea Ziwa Natron.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika mradi wa kuimarisha mpaka. Moja kati ya changamoto hizo ni kutokuwepo kwa barabara za usalama *(Security Roads)* zinazopita karibu na mpaka kwa ajili ya kuimarisha mpaka, kuusafisha mpaka pamoja na ulinzi na usalama wa mpaka huo. Hali imesababisha Wizara kulazimika kutumia barabara ya nchi ya jirani ili kuweza kufanya shughuli zinazohusu kuimarisha mpaka huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi na jitihada zinafanywa na Serikali kuhakikisha kuwa kunakuwepo na barabara zinazopitika wakati wote katika mpaka huu na mipaka mingine. Hivyo basi, Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa inatenga fedha za kutosha kujenga barabara katika maeneo husika ili shughuli zote zinazohusu kuimarisha mipaka ya nchi yetu, ikiwemo doria, usafi na ulinzi wa alama zifanyike kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine zilizoainishwa katika taarifa iliyowasilishwa na Wizara kwa Kamati, ni kutokubalina baina ya pande mbili kuhusu ukubwa wa eneo huru *(buffer zone)* pamoja na umbali kati ya alama moja na nyingine katika mpaka. Changamoto hizi zinaweza kutatuliwa kwa kufanyika vikao vya mara kwa mara katika ngazi zote muhimu ili kuhakikisha zinatatuliwa kwa haraka kwa mustakabali wa mahusiano bora ya nchi hizi mbili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali iendelee kutenga na kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya zoezi la kuimarisha mipaka kulingana na makubaliano ya vikao vya pamoja. Aidha, Serikali iharakishe kutoa mwongozo kwa mamlaka husika kuhusu umuhimu wa kusafisha maeneo ya hifadhi za mipaka mara kwa mara pamoja na kutengeneza barabara.

### 2.5 Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Kamati ina maoni ya jumla kama ifuatayo:-

### 2.5.1 Kandarasi za Ujenzi na Ushauri Elekezi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekuwa ikimtumia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo baadhi ya miradi iliyokaguliwa na Kamati katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hata hivyo, Wakala huu umekuwa ukishindwa kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu kutokana na ama kuzidiwa na idadi ya miradi waliyokabidhiwa kushirikiana na Wizara au sababu nyingine za kiutendaji. Kwa sababu hiyo, miradi hiyo imekuwa ikisuasua na mingine kutokukamilika kwa wakati kama ambavyo Kamati ilishuhudia katika Mradi wa Ujenzi wa Maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora.

Kamati inashauri kwamba, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ifanye tathmini iwapo kuna ulazima wa kuendelea kutumia wakala huyu katika miradi hiyo na ikiwezekana kuja na mkakati mbadala wa kandarasi za ujenzi na ushauri elekezi wa miradi yote ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, wakati Kamati inafanya ziara katika Mkoa wa Mara, ilipita kufanya ukaguzi wa ufanisi wa utendaji wa Kampuni Tanzu ya Ukandarasi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara. Kamati ilishuhudia maendeleo mazuri ya utekelezaji wa mradi huo, na ikashauri kwamba, endapo Wizara itaona inafaa, baada ya kufanya tathmini kuhusu uwezo wa Shirika hili, kulipa kandarasi za ujenzi na ushauri elekezi katika miradi mingine ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

### 2.5.2 Mtiririko wa Fedha Iliyotengwa kwa Miradi

**Mheshimiwa Spika**, katika miradi yote ambayo Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi, changamoto kubwa imekuwa ni kutotolewa kwa wakati na kwa ukamilifu kwa Fedha za Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha husika. Manufaa ya Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii yataonekana pale tu Serikali itakapotoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati na kwa ukamilifu ili kukamilisha Miradi iliyosimama na inayoendelea kutekelezwa.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### 3.1 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepanga kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 200**. Kiwango hiki ni ongezeko la **asilimia 11** ya makadirio ya makusanyo ya Wizara ya Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo Wizara ilikadiria kukusanya **shilingi bilioni 180**. Kwa upande mwingine, **Fungu 03 – Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi** imepanga kukusanya jumla ya **shilingi milioni 600** sawa na kiwango kama hicho kilichopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha uliotangulia, Wizara haikuweza kukusanya mapato kulingana na malengo iliyojiwekea. Kamati inapongeza mikakati ambayo Wizara imejiwekea kukusanya mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ikiwa ni pamoja na:-

a) kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wamiliki wa ardhi kulipa kodi kwa wakati;

b) kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na kusambaza mfumo wa kielektroniki katika Ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri; na

c) Kusambaza hati za madai na kufuatilia malipo ya madeni kutoka kwa wadaiwa sugu na kuwafikisha mahakamani kwa wale watakaokaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kwamba, sekta ya ardhi ikisimamiwa ipasavyo, itachangia kwa sehemu kubwa katika kukuza pato la taifa. Hivyo basi, Wizara inapaswa kuhakikisha kwamba inatekeleza malengo yake ya ukusanyaji wa mapato ipasavyo na kuhakikisha kuwa inajiwekea malengo halisi na yanayotekelezeka kulingana na hali ya uchumi pamoja na mahitaji halisi ya matumizi ya ardhi.

### 3.2 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 **Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi** inaomba kuidhinishiwa **shilingi bilioni 46. 97** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ukilinganisha na **shilingi bilioni 33.15** zilizopangwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Kati ya Fedha inayoombwa**, shilingi bilioni 19.49** ni kwa ajili ya mishahara ambayo imeongezeka kwa takriban **shilingi bilioni 2** ukilinganisha na bajeti ya mishahara ya mwaka unaoisha, na **shilingi bilioni 27.48** inaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ikiwa imeongezeka kwa takriban **shilingi bilioni 11.72**.

**Mheshimiwa Spika**, **Fungu 03 – Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**, inaomba kuidhinishiwa **shilingi bilioni 2.48** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi bilioni 2.24** zilizotengwa kwa mwaka 2019/20. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa kuidhinishwa, **shilingi bilioni 1.5** kwa ajili ya mishahara na **shilingi milioni 979** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

### 3.3 Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, **Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi** inaomba kuidhinishiwa **shilingi bilioni 82.6** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Wizara ukilinganisha na **shilingi bilioni 24.2** zilizoidihinishwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 241**. Kati ya fedha inayoombwa, **shilingi bilioni 16.3** ni fedha za ndani ukilinganisha na **shilingi bilioni 18** zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha, na **shilingi bilioni 66.3** ni fedha za nje ukilinganisha na **shilingi bilioni 6.2** zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa maelezo ya Wizara, ongezeko la bajeti ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 linatokana na mipango ya kuanza kutekeleza miradi miwili (2) inayotarajiwa kupata fedha za nje kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Korea Kusini. Mradi wa kwanza ni

*Land Tenure Improvement Project* ambapo Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 37.1** ambapo kati ya hizo, **shilingi bilioni 2.3** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 34.8** ni fedha za nje ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Malengo ya mradi huu ni kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo zifuatazo:-

a) kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo ya Miji na Vijiji kwa kutoa hatimilki, hatimilki za kimila na leseni za makazi; na

b) kujenga ofisi za ardhi za mikoa na kusimika Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (*Integrated Land Management Information System-ILMIS*);

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa pili ni *the National Spatial Data Infrustacture Project* ambapo Wizara inaomba Bunge liidhinishe **shilingi bilioni 31.99**. Kati ya fedha hizo, **shilingi milioni 500** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 31.49** ni fedha za nje kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Korea. Malengo ya mradi huu ni kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo zifuatazo:-

a) kuandaa ramani za msingi *(base maps)* kwa ajili ya kurahisisha upimaji ardhi nchini;

b) kujenga vituo vya *upimaji (Continous Operation Reference Station –CORS)* katika miji mikuu yote ya mikoa na kuongeza alama 300 za upimaji nchini ambazo zitawezesha upimaji na umilikishaji ardhi nchini; na

c) kujenga kanzidata ya taarifa za kijiografia *(geospatial database)* pamoja na mifumo ya kulinda na kusambaza taarifa hizo kwa watumiaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Wizara kwa kubuni miradi hii kwa kuwa itakuwa ni mwanzo wa utekelezaji wa maoni ya mara kwa mara ya Kamati kwamba, Serikali inapaswa kuwa na mkakati wa kudumu wa kuhakikisha kuwa kila kipande cha nchi hii kinapangwa, kupimwa na

kumilikishwa. Hatua hii, itapunguza migogoro ya ardhi nchini. Hata hivyo, Kamati inadhani kwamba, Wizara kwa kushirikiana na HAZINA, inapaswa kuwa na Mpango Kabambe wa upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini bila kutegemea fedha za ufadhili au hisani.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, **Fungu – 03 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi** inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi bilioni 1.5** kwa ajili ya kutekeleza kazi za Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi. Kiasi hiki ni pungufu kwa **asilimia 50** ukilinganisha na **shilingi bilioni 3** zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na masuala mengine, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ina majukumu ya kuratibu, kushauri, kuandaa, kukagua na kusambaza programu za mipango ya matumizi ya ardhi kwa uwiano baina ya Sekta kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Upangaji Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116. Kwa kuwa kiwango kilichotengwa kutekeleza miradi ya maendeleo ni pungufu, ni dhahiri kwamba baadhi ya majukumu hayo hayatatekelezwa kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali itenge fedha za kutosha kutekeleza miradi ya Tume ili iweze kufikia malengo yake.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Masuala ya Jumla

#### 4.1.1 Muundo wa Bajeti na Hali ya Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Kamati imebaini kuwepo kwa mtiririko usioridhisha wa mapato katika bajeti inayotengwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Mandeleo ya Makazi, hivyo basi, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa katika Bajeti zijazo, zinaakisi hali halisi ya mapokeo ya fedha. Kwa kufanya hivi, Wizara itakuwa na uwezo wa kupanga kulingana na vipaumbele vya utekelezaji wa majukumu yake.

### 4.1.2 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ambazo hazikuainishwa katika Taarifa ya Wizara kuhusu hali duni ya makusanyo, ni ukweli kwamba kwa miaka kadhaa iliyopita, halmashauri zimekuwa hazina mwamko wa kukusanya kwa sababu ya mabadiliko ya utaratibu wa makusanyo hayo. Hapo awali, halmashauri zilikuwa zina mamlaka ya kukusanya na kisha kubakiza **asilimia 30** ya mapato yatokanayo na ardhi, kabla ya kutuma Serikali kuu. Fedha hizo zilitumika kwa shughuli za halmashauri husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba, Wizara iweke mikakati madhubuti ya kusimamia maafisa ardhi katika halmashauri nchini, na kuwawekea malengo ya makusanyo ambayo yatakuwa sehemu ya kipimo cha utendaji kazi wao.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Kamati inaishauri Wizara kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu na ulazima wa kushiriki katika kuchangia pato la taifa katika sekta ya ardhi. Aidha, kuna ulazima wa kuweka masharti katika Sheria zetu ambapo Wizara itakuwa na mamlaka ya kushurutisha wananchi waliofanya maombi ya kumilikishwa ardhi, kuchukua na kulipia hati zao. Hatua hii iende sambamba na kuimarisha Ofisi za Ardhi za Mikoa na za Wilaya ili kwamba Wasajili walioko mikoani wawajibike kutoa hati katika wilaya zote nchini ili kuboresha na kupeleka huduma kwa wananchi.

### 4.1.3 Mpango wa Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba kumekuwa na mwenendo usioridhisha wa kutotolewa fedha za maendeleo kwa wakati. Kamati inashauri kwamba, Wizara ya Fedha itoe fedha kwa wakati na kwa ukamilifu ili Wizara iweze kutekeleza kwa ukamilifu Mpango wa Maendeleo.

## 4.2 Masuala Mahsusi

### 4.2.1 Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina taarifa kuhusu uamuzi wa Serikali wa kurudisha kesi na migogoro ya ardhi katika

Mahakama, ambayo awali ilikuwa inashughulikuwa na Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya. Hatua hii, inatokana na ukweli kwamba, mabaraza yaliyopo ni machache na pia kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika utendaji wa mabaraza hayo ikiwemo ukiukwaji wa maadili kwa baadhi ya watendaji, elimu ndogo na pia kwa kuwa watumishi hao sio waajiriwa wa kudumu.

Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba, Serikali inapaswa kukaa kwa pamoja na kushirikiana ili kuja na namna bora ambayo itawezesha baadhi ya Kanuni za uendeshaji wa Mabaraza hayo, zitumike katika vyombo vya mahakama ili kuwe na mazingira rafiki ya kusikiliza mashauri yanayowasilishwa.

Aidha, kwa kuwa mabadiliko haya yatasababisha kubadilika kwa Sheria mbalimbali za ardhi, Kamati inashauri kwamba wakati wa kuleta mabadiliko ya sheria *(miscellenaous amendments)* Bungeni, Kamati zitakazokuwa na mamlaka ya kushughulikia masuala ya ardhi, sheria na Serikali za Mitaa zishirikishwe kikamilifu ili kupata maoni yao katika sula hili.

### 4.2.2 Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na mjadala kuhusu kuipandisha tume hii kuwa Mamlaka. Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba, ni vyema Wizara ikafanya tathmini ya kina na kisha kulitaarifu Bunge, kuhusu umuhimu, ufanisi na mikakati ya kuifanya Tume hii itekeleze majukumu yake kwa ufanisi zaidi na maslahi mapana ya nchi. Kamati inashauri Wizara ifanye tathmini hii haraka iwezekanavyo na taarifa hiyo iwasilishwe mapema ndani ya mikutano mitatu ya Bunge lijalo.

### 4.2.3 Upangaji, Upimaji na Umilikishaji wa Ardhi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kushauri, na kuisisitiza Wizara kuja na Mpango Madhubuti wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi ambao utatumia fedha za ndani. Kwa kuzingatia hali ya uchumi wa dunia kwa sasa, ni wakati nchi

yetu ikatambua kwamba ardhi ndiyo rasilimali kuu katika uchumi wa taifa lolote. Hivyo basi, Serikali iweke kipaumbele katika Sekta hii kwa kuitengea fedha za kutosha ili tuweke mipango ya muda mfupi na muda mrefu ya matumizi ya ardhi yetu ambayo mahitaji yake yanaongezeka kila siku.

### 4.2.4 Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, suala la uimarishaji wa mipaka ya nchi yetu ni suala muhimu sana kwa mustakabali wa ulinzi na usalama na diplomasia ya kimataifa. Suala hili ni mtambuka, na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepewa jukumu la kiutendaji katika masuala yanayohusu miundombinu. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba utekelezaji wa mradi huu una changamoto nyingi ambazo Wizara hii peke yake haiwezi kuzimaliza.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba, Wizara ya Ardhi ikishikirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama, ifanye jitihada za kutatua changamoto zilizopo kwa sababu ya uhusiano mzuri ambao upo baina ya nchi yetu na mataifa ambayo tunapakana nayo. Bila kuwa na makubaliano katika ngazi za juu, Wizara hii haitaweza kuwa na uwezo wa kuimarisha mipaka ya nchi yetu kwa wakati.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* :-

1. Mhe. Kemirembe Rose Julius Lwota, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb
3. Mhe. Boniface Mwita Getere, Mb
4. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb

5. Mhe. Magdalena Hamis Sakaya, Mb
6. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb
7. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
8. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb
9. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb
10. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb
11. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
12. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb
13. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
14. Mhe. Risala Saidi Kabongo, Mb
15. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb
16. Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Mb
17. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb
18. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb
19. Mhe. Zainab Nuhu Mwamwindi, Mb
20. Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb
21. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
22. Mhe. Timotheo Paul Mnzava
23. Mhe. Pauline Philip Gekul, Mb
24. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo, Mb
25. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula (Mb), Katibu Mkuu Ndg. Mary Gasper Makondo, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Nicholas N. Mkapa pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema Shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Yona Kirumbi na Ndg. Monica Mwamunyange wakisaidiwa na Ndg. Mwimbe John,

kwa kuratibu vema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lipokee Taarifa hii ili lijadili na kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Kemirembe Rose Julius Lwota, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

11 Mei, 2020

**MHE. ALLY SALLEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, hoja ya dharura.

**SPIKA:** Ni Msekwa au humu ndani ya ukumbi.

**MHE. ALLY SALLEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, Ally Salleh!

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Salleh.

## HOJA YA DHARURA

**MHE. ALLY SALLEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kutoa hoja ya dharura kwa mujibu wa Kanuni ya 47 na ninajua kwamba inasomwa pamoja na Kanuni ya 48. Hoja hii kusema kweli kwa sasa imeleta taharuki kubwa katika nchi ambapo suala la sukari limekuwa tete sana kiasi ambacho sukari imepanda bei kwa kiasi kikubwa katika muda huu, lakini...

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Salleh, samahani. Hoja hiyo imeshatolewa na Mheshimiwa Mlinga kabla, labda niitolee tu mwongozo moja kwa moja kwamba kesho ni Bajeti ya Wizara ya Kilimo hapa kwenye ukumbi huu; na moja ya shughuli ambayo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo atafanya pamoja na uwasilisho wa bajeti yake, ni kutoa ufafanuzi wa mambo yanayohusiana na sukari.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tuwe na subira, kesho tu tutapata hiyo nafasi, katika kuchangia kwetu basi itakuwa ni moja ya mambo ambayo tutayazungumzia. Nakushukuru sana.

**MHE. ALLY SALLEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa uvumilivu. Sasa tunaingia kwenye uchangiaji, tuanze na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Wizara hii. Awali ya yote nipende kutoa pongezi za dhati sana kwa Mheshimiwa Lukuvi pamoja na Naibu wake, mtani wangu, mama yangu Mheshimiwa Angelina Mabula. Wizara hii imefanya kazi kubwa sana kazi ambayo leo hii inakwenda kuifanya hata mjadala katika Wizara hii uwe rahisi sana, lakini kipekee sijui walikuwa wanaipendelea sana Lushoto maana Mheshimiwa Waziri amekuja Lushoto mara mbili na Naibu wake pia amekuja mara mbili. Naamini ni katika uchapakazi hasa baada ya Mheshimiwa Lukuvi kuchezewa ngoma ya *mdumange* kule Mnazi naona hata kasi ya utendaji imezidi kuongezeka.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imefanyakazi nzuri sana. Tukianza katika Mabaraza ya Ardhi; sisi kule tumebahatika kufunguliwa Baraza la Ardhi na tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri tumepata pia Mwenyekiti. Zipo

changamoto chache lakini ambazo naamini ziko ndani ya uwezo wa Wizara:-

Mheshimiwa Spika, changamoto ya kwanza ni kwamba bado watumishi siyo wa kutosha katika eneo hili, kwa maana kwamba tunaye Mwenyekiti na Karani pake yake, nasi tulitamani tupate angalau na Katibu Muhtasi wa kumsaidia japo hata kuandika hukumu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo la usafiri; kamamnavyofahamu migogoro mingi ya ardhi iko vijijini kwahiyo inawapasa waweze kusafiri kwenda maeneo ya *site* kwa ajili ya kupata ushahidi na kadhalika. Kwahiyo Mabaraza mengi hayana usafiri na wanatumia zaidi kwa Wakurugenzi wa Wilaya lakini pia kwa *DC* kwa wakati mwingine. Kwahiyo, tunamwomba Waziri pia katika eneo hili alitazame huko mbeleni waweze kupatiwa usafiri.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili, tumeona pia kuna changamoto ya elimu katika Mabaraza ya Kata na Vijiji huko ambako ndiko msingi wa kesi unakojengwa. Huku kuna changamoto kubwa sana ya kwamba wale Wajumbe wayale Mabaraza ya Vijiji na Kata hawapati uzoefu wa kutosha kwa maana ya uwezeshaji kielimu. Kwahiyo, nimwombe Waziri sasa katika Wizara yake aweze kupanga semina mbalimbali katika Mabaraza haya ya Kata na Vijiji ili waweze kuzichambua hizi kesi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya tatu; nikija katika Halmashauri yetu ya Lushoto tuna tatizo la uhaba wa Wapima, hatuna Mpima kabisa kiasi kwamba tunapokuwana shida ya upimaji ni lazima tuazime kutoka Wilaya jirani ya Same, Kilimanjaro ama katika Wilaya ya Korogwe. Kwahiyo, ningemwomba sana Waziri aangalie eneo hili nalo, tuweze kupata Wapima ili angalau mambo yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sanaMheshimiwa Waziri; miongoni mwa Ofisi chache ambazo amezitaja za Mikoa ni pamoja naya Mkoa wa Tanga. Tumemkabidhi Ofisi pale eneo la Chumbageni karibu nakijiji maarufu kama Kijiji

cha 21, Ofisi nzuri ya kisasa. Naamini katika Mikoa yote, Tanga ndiyo tumemkabidhi Ofisi ambayo ni nzuri na ya kisasa.

Mheshimiwa Spika,pia tunashukuru kwamba mafaili tayari yaliyokuwa yanahusu Mkoa wa Tanga takribani mafaili 3,000 yaliyokuwa Kanda kule Kilimanjaro yameshahamishiwa Mkoani. Kwahiyo, sasa tumefarijika pia Waziri amesema kwamba wananchi kule wilayani hawana sababu ya kwenda mkoani, hati hizi atazishusha katika Ofisi za Ardhi za Wilaya waweze kuwapatia wananchi. Kwahiyo, tunamwombea sana kwamba jambo hili nalo linakwenda kuondoa adha kwa wananchi kusafiri pasi na sababu lakini pia linakwenda sasa kufanya urasimishaji wa ardhi uwe rahisi zaidi kwasababu naamini huduma hii itafika vijijini.

Mheshimiwa Spika,jambo ambalo ningependa sasa nishauri kwa upande wa Wizara hii ni suala zima la uanzishaji wa *Real Estate Regulatory Authority* (Mamlaka ya Kudhibiti Upangishaji na Uwekezaji Katika Ardhi na Nyumba). Hili ni jambo muhimu sana. Tunatambua kwamba kuna maboresho ya Sera ya Ardhi yanafanyika, kwahiyo tungeomba kwamba suala hili la uboreshaji wa sera liende kwa haraka zaidi ili baadaye sheria na yenyewe iweze kutungwa tuweze kuwasaidia Watanzania. Watanzania wengi wanapata adha wanavyolipa kodi. Kodi zinaanzia kuanzia miezi mitatu, miezi sita namwaka siyo wote ambao wanaweza hasa kipindi hiki ambacho tuna *crises* hii ya *corona,*utaona kwamba wananchi wengi vipato vimekuwa vya shida, wanapata shida kubwa sana katika kulipa kodi za nyumba.

Mheshimiwa Spika,nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hii Mamlaka ya Nyumba na Upangishaji ni muhimu sana, ni jambo ambalo litakwenda kutua mzigo mkubwa sana kwa wananchi wa kawaida, lakini hasa pia watumishi kwasababu mtumishi analipwa ujira wake kwa mwezi, lakini analazimika alipe kodi ya miezi sita au mwaka. Kwahiyo, nimwombe sana katika eneo hili atusaidie.

Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze sana Msanii wa kizazi kipya, *Diamond Platinum,* Nasib Abdul ameweza

angalau kwa mwezi huu kulipia takribani wananchi 5,000 kodi ya miezi japo mitatu. Kwahiyo ni jambo ambalo naliona lina ugumu ndiyo maana hata watu wenye nafasi mbalimbali wanaona kwamba wanaweza wakasaidia katika eneo hili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa nafasi, huo ndiyo ulikuwa mchango wangu katika siku ya leo. Ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rashid Shangazi. Nilishakutaja Mheshimiwa Lwakatare na atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Massay ambaye yuko kule Msekwa. Mheshimiwa Lwakatare.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu na nikushukuru kwa nafasi hiiambayo unanipa wewe, nimeshaongea humu ndani ya Bunge kama mara nne, lakini safari zote nilizoongea bahati nzuri wala sitaki kusema kwamba ni bahati mbaya, ambaye alikuwa amekalia Kiti ni Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo uko mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kama hali itakuwa shwari huenda ikifika tarehe 28 kwamba mimi nilishatangaza kutoendelea kugombea kuwa Mbunge pale Bukoba na nikatangaza kwamba nastaafu siasa za kugombea Ubunge. Umri uliobaki nataka niutumie kuisaidia familia yangu, lakini kuwasaidia marafiki zangu hata na wengine nao tusaidiane kwa umri ambao bado naweza nikakimbia na nilifanya hivyo na umekuwa msimamo wangu miaka mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Spika, tangu miaka mitatu iliyopita nilieleza bayana kwenye Chama changu, kwenye tawi langu, kwawananchi wa Bukoba, kwa Viongozi wangu wa Chama Taifa na kwa Wabunge wengi ambao ni rafiki zangu waliopo humu kwamba sitaendelea kugombea. Kwahiyo mtu yoyote asijeakaichukulia kwamba labda kwasababu ya mambo yanayoendelea ndiyo maana ameamua kuchomoka. Mimi mara nyingi huwa najipanga kwa mambo yangu na

namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ananisaidia kwenda na ndoto zangu.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Lukuvi na Naibu wake na Watumishi wake wote. Wizara hii nimekuwa Waziri Kivuli kwa kipindi chote ambacho nimekuwa Mbunge ndani ya Bunge hili na hata pale alipobadilisha kuniondoa kwenye Kamati inayohusiana na Wizara hii na nikaenda Nishati na Madini bado Kiongozi wangu (KUB), Mheshimiwa Freeman Mbowe aliendelea kuniamini kwamba pamoja na kuhamishwa Kamati, lakini nakuamini ukae kwenye Wizara hii na kweli nimeitumikia kwa miaka yote mpaka leo hii ninapozungumza.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Lukuvi kwa nini? Nilipoteuliwa kuwa Waziri Kivuli au Msemaji wa Wizara ya Ardhi aliniita Wizarani kwake nikaenda, sikujua ananiitia nini, lakini muda niliokwenda nikafika Ofisini kwake naingia ndani nakuta jopo la Wasaidizi wake wote; Makamishina, Katibu Mkuu, Naibu Waziri wake na wote aliowaona wanafaa ukumbi ulikuwa umejaa. Akaniita na baada ya kufika pale akasema kwasababu sijui shughuli alizonazo Mheshimiwa Lwakatare lakini Mheshimiwa huyu nimemkaribisha kwa muda mchache ili baadaye aendelee na shughuli zake na wao waendelee na kikao chake.

Mheshimiwa Spika, aliwaambia kwa ufupi; huyu ni Msemaji wa upande wa Upinzani kwenye Wizara yetu, nawaagiza wakati wowote na muda wowote akihitaji kwenda kwenye ofisi yoyote iliyo chini yake wanipokee kama ambavyo na yeye wanampokea au kumsikiliza, maana yake nini? Tangu siku hiyo sijawahi kurudi kwa Mheshimiwa Lukuvi kwasababu mambo mengi ya Wizara yangu kama Waziri Kivuli nilikuwa nayamaliza na Wasaidizi wake na tulimaliza kabisa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Lukuvi tuna historia; wakati anajitutumua kuanza kufahamika alipewa kazi ya kwanza ya kuteuliwa ya *U-DC* pale Bukoba *Town.* Alipokuja mimi nilikuwa bado kijana sana na yeye alikuwa bado kijana

japo huwa sura yake haizeeki. Alipokuja alinikuta mimi nikiwa Afisa Utumishi na Utawala wa Manispaa ya Bukoba, kwahiyo ni mojawapo ya watu waliompokea, kumtembeza Mjini ili asiwe mshamba kwa pale Bukoba *Town* ikiwa ni pamoja na kumwonyesha vilinge vile ambavyo kama *DC* na kama mwananchi wa Bukoba avijue. Nazungumza kuna mtu anasema eti Kagera *technology*, hiyo haipo kwenye Jimbo langu iko kwaMheshimiwa Rweikiza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasaMheshimiwa Lukuvi huyu ukweli wenyewe na yeye anajua, mambo yalianza kumnyookea tangu wakati ule alipokuja kuwa *DC* Bukoba. Tangu alipotoka Bukoba mambo yake na*graph* ikawa inapanda tu mpaka hapa alipo. Kwahiyo sisi Bukoba japo hatufanyi miujiza lakini pale panawafungulia watu wengi njia. Kwahiyo,hata nilipopangwa kwenye Wizara yake nilipewa Wizara kwa mtu ninayemfahamu, anapenda nini, anachukia nini, siyo mtu wa majivuno, ni mtu wa kupenda kusaidia, amenisaidia sana, sana, sana na nakumbuka wakati ule Manispaa ya Bukoba ilikuwa bado inajulikana kama Halmashauri ya MjiBukoba.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa kitu alichonisaidia; pale msimamizi wangu Mkuu na Kamati ya Fedha na Uongozi iliniteua niandike andiko la kuibadilisha Bukoba, Halmashauri ya Mji kuwa Manispaa. Kwahiyo nikaandika hiyo *paper*na yeye mwenyewe kama *DC* alinisaidia sana na kwa kuwa nilijenga hoja kitaalam kwa kweli Bukoba kupitia mkono wangu na Waheshimiwa Madiwani tukapata Manispaa. Nimeona niyazungumze haraka haraka maneno haya ili watu wajue wapi tumetoka.

Mheshimiwa Spika,labda niulize maana yake wenzangu walinipa nafasi ya watu watatu wao waka-*withdraw.* Sasa ninachotaka kusema; Mheshimiwa Lukuvi ametosha katika Wizara hii na ameweka, mimi kama Waziri mwenzake ametosha siyo kwasababu ya historia niliyoizungumza, lakini ingieni kwneye historia; Waziri ambaye ameweza kuimudu kwa asilimia kubwa Wizara hii yenye matatizo miaka kwa miaka ni Mheshimiwa Lukuvi. Sasa sielewi

anatumia ndumba gani kwa sababu nimeingia mpaka kwenye *google* kuona amesomea nini, sijaona kama ana *profession* yoyote ya mambo ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, hii maana yake kama alikwenda shule, ile *theory* aliyoipata ya kiuongozi na kiutawala basi anaitendea haki. Anaitendea haki, anawaongoza watu wake vizuri, anapanga mipango yake kwa ubunifu wake pamoja na kuangalia Ilani ya Chama chake, lakini ukija kugundua yeye mara nyingi ni mbunifu na kila anachokibuni anakisimamia mwanzo, mwisho na hilo linamtofautisha na Mawaziri wenzake wengi ambao naamini hawatendi kama yeye anavyofanya. Kwa hiyo,naweza kusema Mheshimiwa Lukuvi anaweza akawa *mentor* mzuri wa Mawaziri walio wengi kwasababu ana uthubutu.

Mheshimiwa Spika, sasa niingie kwenye hoja; ni kwamba kwa Kagera nimshukuru Mheshimiwa Lukuvi, suala lilikuwa linaniamsha usiku, mchana kwenda kwake na hata Wizarani amelifanya. Amezungumza hapa, sasa Hati inaweza kupatikana pale Bukoba Mjini Ofisini. Watu wangu hawaendi tena Mwanza.maana yake tangu ule Mji ulipokuwepo ulikuwa na hati zisizozidi 5,000.

Kipindi changu pamoja na kurasimisha na kufanya mambo yote na kufanya ubunifu tumepandisha viwanja ndani ya muda wa miaka mitano mpaka viwanja 15,000 ndani ya Mji kupata Hati. Sasa hivi kwa mpango wa kurasimisha makazi najua tutakwenda kwenye *target* yetu ya 50,000 ya Hati.

Mheshimiwa Spika,kwa kuwa muda unakwisha, dakika moja mimi nishukuru, nilikuwa na mambo mengi, sasa kwa Uwaziri Kivuli wa Ardhi nilikuwa na hotuba yangu nzuri, lakini mchanganyiko uliotokea hapa katikati siwezi kuwasilisha mezani japo wataalam wameniletea hotuba ninayo hapa, kama atakubali katika kujumuisha aniruhusu mimi nitakuletea hotuba yangu kama utaona inakufaa chukua yanayofaa ambayo hayatakiwi achana nayo, lakini ni kwa faida ya Watanzania.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sanana Mungu akusaidie, ahsante sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rwakatare. Nilishakutaja Mheshimiwa Flatei Gregory Massay kule Msekwa na utafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul huko huko Msekwa. Mheshimiwa Massay

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa uhai wa kusimama mbele hapa na kutoa mchango wangu. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Joseph Magufuli kwa jinsi ya utendaji wake mzuri wa kazi ambako umeonekana katika nchi yetu na mara nyingi maeneo mengi hasa vijijini na katika maeneo haya ya ardhi amekuwa mtetezi wa wanyonge.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ameunda Wizara chache na kuzituma zikaangalie kero hii ya ardhi, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa ajili hii. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Ardhi, kwa jinsia ambavyo wametutendea haki sisi wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini. Tulikuwa na shida ya migogoro mingi ya ardhi.

Katika Mkoa wa Manyara ukiangalia historia Jimbo la Mbulu na Wilaya ya Mbulu ilikuwa na migogoro mingi sana ya ardhi, lakini walituzindulia Baraza la Ardhi pale Dongobesh na limekuwa liki-*operate* na kuondoa migogoro mingi sana ambayo likuwepo katika eneo la Jimbo langu. Kwahiyo, kwa hatua hii namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na nimwombee kwa Mungu aendelee zaidi na Naibu wake pia. Katibu Mkuu naye nimpongeze pia, maana sijawahi kumpongeza ameteuliwa juzi kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Ardhi, Mungu ambariki sana dada yangu Mary aendelee kulinda ardhi ya wananchi wanyonge ili wanyonge hao wapate haki katika Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi; nimesoma na nimeona jinsi ambavyo Waziri na leo ametangaza kwa *GN No. 308* ya mwaka 2020 kuwa Mabaraza haya ya Wilaya na haya ya Kata yanakwenda kuondoshwa sasa na kupelekwa kusimamiwa chini ya Mahakama. Sina shida na hilo, lakini naona zipo changamoto chache ambazo kwanza zinaonekana kabisa katika muundo wa Mabaraza haya na kwasababu wanapeleka Mabaraza haya chini ya Mahakama, niombe pia basi Waziri na Serikali kwa ujumla iangalie, yake maswali mawili nimekuwa nikijiuliza. Swali la kwanza,kwanini Mabaraza haya mwanzoni yalianzishwa yakapelekwa chini ya Wizara ya Ardhi na sasa tunayapeleka chini ya Mahakama?

Mheshimiwa Spika, Serikali ikiweza kujibu maswali haya vizuri na kuturidhisha vizuri, ndiyo ione namna gani sasa ya kusaidia wananchi wanyonge kwasababu kwa Baraza ambalo sasa sisi tumeshapata lina mwaka mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, sikatai apelekwe katika maeneo haya, lakini naomba zile changamoto ambazo zinaikumba eneo hili la baraza hili iweze kutatuliwa vizuri na Serikali. Kwa mfano wananchi wanyonge sana ndiyo wenye maeneo haya na ndiyo ambao wanazulumiwa maeneo au ardhi zao kwa maana hiyo basi ukiangalia hata hukumu zenyewe zinavyotolewa, zinaandikwa kwa lugha ya kingereza hasa.

Mheshimiwa Spika, sasa tuombe na nishauri, Serikali iangalie namna rahisi sana ya kuwasaidia wananchi wetu wanyonge ambao watasaidika ili wapate ukumu wanaoielewa. Kwa mfano, ukiangalia nchi za wenzetu katika sheria nyingi kwa mfano Norway sheria zao nyingi ziko kilugha ya kwao *Norwegian* na mimi na *declare* hapa kwa nini sisi kama watanzania tusirahisishe ile hukumu inayotolewa katika mahakama zetu najua itapelekwa kwenye mfumo wa mahakama hasa Mahakama ya mwanzo kwanini basi tusibadilishe zile sheria tukawaundia sheria mpya ya kuwasaidia wale majaji hao mahakimu waweze kutoa hukumu kwa lugha ya Kiswahili ili watu watu wetu wakaweza kuelewa.

Mheshimiwa Spika, kwasababu ukiangalia sasa hivi hali halisi inaonyesha kwamba hukumu anapopewa mlalamikaji ama mlalamikiwa anahitaji kwenda kumtafuta mwanasheria ambaye atamtafisiria hiyo hukumu ndiyo aje kukata rufaa. Na kwa kufanya namna hii inaongeza usumbufu kwa wananchi lakini siyo hilo tu inamfanya mwananchi yule awe wa tatu maana anakuwa anatafsiriwa hiyo ukumu lakini pia anatafuta fedha za kumtafuta wakili na wakili mwenyewe katika maeneo ya vijijini hawapo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiweka sheria hii kwa lugha ya Kiswahili na ikatafsiriwa vizuri kwa Kiswahili ni rahisi kwa mwananchi wa kijijini akaweza kuitetea mbele ya mahakama na kuilinda haki yake mbele ya mahakama na ushahidi ukawepo mbele ya mahakama. Kwa kuwa sasa nimesoma vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri natangazo hili la *Government Notes* ya 2020 yenye namba 308. Basi niombe pia pamoja na kwamba mnapeleka huko basi muende kuhakikisha na muunde taratibu ili basi mnapopeleka mabaraza hayo mahakamani kule pawepo na namna nzuri hasa ya usafiri kwa mfano basi wanapofanya hukumu za ardhi waende *site* wakaangalie je, hiki wanachokihukumu ndiyo kile?

Mheshimiwa Spika, pamoja naona muda umeenda sana lakini ushauri mwingine naomba nishauri sasa kwenye bajeti ijayo Serikali ione itafute fedha ya kupima nchi nzima ili unavyopima nchi hii mkipata fedha mtakuwa mmejua eneo la nchi na mkipata fedha ya kupima nchi hii migogoro ya ardhi itapungua, naona kengele imeshalia lakini niombe Serikali katika bajeti hii maana ni mjumbe wa wizara, basi tuone kwamba miradi yote iliyoombewa pesa wizara ya fedha ione namna gani ya kusaidia kupata pesa katika wizara hii ili miradi ya wizara ikaweze kutumizwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tumekwenda kutembelea sisi kama kamati tumefika kwenye Mikoa ya Tabora tumekwenda maeneo ya Mwanza kuna miradi ambayo bado haijakamilika na yote hii haijakamilika kwasababu tu ya fedha kutopatikana kwa hiyo niombe

Wizara ya Fedha ione namna gani ya kupele fedha kwa wakati. Mheshimiwa Lukuvi hana namna yoyote ya kufanya kazi kama hajapewa pesa lakini pia siku halmashauri ambazo zimepewa mujibu wa kupima na kurasimisha ardhi sasa basi changamoto zilizoko kwenye halmashauri zetu tuna tatizo karibu halmashauri nchi nzima hatuna wataalam wapimaji wa ardhi. Kwa hiyo, basi Serikali iangalie changamoto ikawasaidie kupeleka wapimaji katika wilaya zote.

Mheshimiwa Spika, lakini pili Serikali pia ione namna gani ya kusaidia halmsashauri hizi aidha kuzikopesha zinunue hizo vifaa vya upimaji ili basi ardhi ikapimwe na maeneo haya yote na itakuwa nafuu ili wananchi wetu waweze kupata ardhi kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa nitakuwa mchoyo wa fadhili kama sijampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa mara nyingine, lakini nimpongeze Mheshimiwa Lukuvi umeitendea haki wizara hii umetembea na umekuja katika majimbo ya Wabunge mbalimbali, lakini kubwa ume *stabilize* na umeweka migogo vizuri na hata kule watu wetu wananchi wetu wanalia wakimfurahia Rais kwasababu ya kazi yako unayoifanya wewe na Naibu waziri niwapongeze sana na Mungu akubariki na wananchi wa Ismani wakurundishe bunge lijalo tukutane huku tukiitetea na kuwatetea wananchi wengi ambao wananyanyaswa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nikushukuru kwasababu umeisimamia ardhi iliyo kule Mbulu inayoendelea kufanyiwa mambo na wale wa piga dili Mungu akubarika ahsante sana huu ndiyo mchango wangu naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Ahsante sana. Ndiyo! Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, japo ameshakaa nilitaka niinyooshe kidogo taarifa kidogo Mheshimiwa Flatei ili

wengine wanafutilie vizuri *GN* nilioyochapisha namba 308 haihusiani na uvunjwaji na mabaraza ya ardhi, mabaraza ya ardhi hayajavunjwa na kama ikiamuliwa kufanya hivyo basi sheria itakuja bungeni tutajadili kwa hiyo *GN* niliyotamka nimeanzisha masjala ya kusajili hati miliki na miamala mingine kwenye mikoa kwasababu mwanzo tulikuwa kanda 8 sasa nime *establish* masjala 26 kwa hiyo *GN* ina hamisha mamlaka ya kanda nane kwenda mikoa 26 ni masjala ya hati siyo mabaraza ya ardhi nilitaka kumuondoa wasiwasi Mheshimiwa Flatei. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri nilishakutaja Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul alafu tutarudi hapa kwa Mheheshimiwa Stephen Kiluswa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa fursa ili niweke mawazo jioni ya leo katika wizara hii muhimu wizara ya ardhi. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetupa nafasi ya pumzi hii ya uhai kwa kweli ni kwa neema zake, ametulinda tangu tumeanza Bunge hili na sasa tunamalizia malizia awamu hii, ametupa afya njema, ametupa moyo wa kutumikia watanzania nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa haya ambayo ametujalia.

Mheshimiwa Spika, lakini nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amekuwa akiongoza Taifa, tangu Mheshimiwa Rais alivyotoa kauli pale Chato kuhusu corona mioyo yetu imeshuka tumepata nguvu mpya ya kutumikia watanzania lakini watanzania wameona ni kwa kiasi gani wanaweza wakaishi na corona na wakachapa kazi, Mheshimiwa Rais tunakushukuru na tunakupongeza kwa jinsi ambavyo umekuwa ukitutia moyo.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe pamoja na Naibu Spika na wenyeviti wa Bunge kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkiongoza Bunge letu kwa muda wote huu wa miaka mitano. Kwa kweli mmekuwa msaada kwetu kwa wabunge lakini mmekuwa mkituongoza katika kazi zetu mbalimbali hapa bungeni. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake na Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo

wametumikia wizara hiii kwa muda mrefu. Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa dada Angellah pamoja na dada Maria Katibu wetu Mkuu katika wizara hii mmeitendea haki wizara hii.

Mheshimiwa Spika, miaka iliyopita nilikuwa nikisimama kwenye wizara hii nimekuwa nikiongea mambo mengi na kero nyingi sana za wananchi, lakini Mheshimiwa Lukuvi mmezitendea haki, mmefika kwenye majimbo niwashukuru sana babati palikuwa hapakaliki kwa ajili ya migogoro ya ardhi lakini mmefika Mheshimiwa Waziri Lukuvi, umetatua mgogoro wa Sigino ombi langu kwa Serikali Mheshimiwa Waziri anapokuwa ametoa kauli sasa basi wale watendaji wa chini wamalize yale maazimio au watekeleze yale ambayo tumekubaliana. Mheshimiwa waziri hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, leo nina mambo machache ya kuzungumza katika wizara hii ambayo yamenifanya niweze kukubali bajeti hii na niipongeze Serikali kwa jinsi ambavyo amejipanga katika kuhudumia ardhi ya watanzania. Jambo la kwanza ili la kuanzisha la kurudisha kesi ambazo zilikuwa zinapelekwa kwenye mabaraza ya ardhi ya wilaya na kwenye kata sasa kupeleka kwenye mahakama za mwanzo na wilaya Mheshimiwa Waziri hili ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali yangu mtekeleze mapema na kanuni muweze kuitoa mapema kwa sababu haya mabaraza ya wilaya yalikuwa hayazidi 50 nafikiri kwa nchi nzima. Lakini tuna mahakama ya mwanzo na ya wilaya nafikiri ya 100 kwa nchi nzima mantiki yake ni nini kama kesi hizi zitarudi kwenye mahakama na kanuni zikawa zimetungwa mapema wananchi wengi watapunguza gharama za kutafuta haya mabaraza ya ardhi ya wilaya na kesi zao zitakwenda kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba Serikali yangu *staffing* ambayo inahitajika katika mahakama ili hizi kesi ziende vizuri na tuwasaidie wananchi wetu kwasababu huko kuna mahakama ya wilaya na mwanzo na itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Mbulu walikuwa wanahangaika kama alivyosema Mheshimiwa Flatei lakini pale Babati watu walikuwa wanasafiri wanakuja pale mjini kesi zinachukuwa muda mrefu kwasababu pia *staffing* yake ni watu wachache na mwenyekiti akipata dharura kesi zinasimama. Kwa hiyo, niipongeze wizara hii kwa kuona kwamba tuna mahakama ya kutosha na tunawaza kurudisha hizi kesi kwenye mahakama ambazo zipo. Mheshimiwa Waziri litekeleze upesi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo limenifurahisha sana ni hili la vifaa ambavyo vya upimaji vimefika katika mikoa yetu *RTK*. Ambalo nimefurahishwa kabisa umeshatuletea hawa wataalamu hao makamishina ya ardhi wasaidizi katika mikoa sasa na jana Jumapili kamishna wa Mkoa wa Manyara alitutafuta sisi viongozi wenzake akisema ameshawasili tayari kwa kuanza kazi na tumempa maeneo ambayo yalikuwa yakitusumbua hili ni jambo jema naipongeza Serikali mwanzoni tulikuwa tunaangaika tunakwenda mpaka Moshi lakini hati zinachelewa mambo mengi yanachelewa kwa hili Ofisi za mikoa na vifaa hivi vya upimaji kufika kwenye mikoa yetu huu ni ukombozi wa kutosha kwa ardhi za watanzania na nina amini ardhi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwako Mheshimiwa waziri niombe sasa hawa makamishina pamoja na viongozi waelekezwe wasaidiane kupima ardhi za wananchi hivi vifaa visitumike tu kwa ardhi za watu binafsi binafsi hata ardhi za taasisi kama shule, kama Zahanati, mipaka ambayo ilikuwa na migogoro sasa iweze kupimwa mfano kama mimi pale nina migogoro midogo midogo mitaa kwa mitaa, wilaya kwa wilaya basi hivi vifaa viweze kutumika kukamilisha haya.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la tatu hii miradi ya mwaka 2020/21 na hizi fedha za bilioni 66.3 za Benki ya *Exim* ya Korea pamoja na Benki ya Dunia kwa ajili ya upimaji wa ardhi na hatimiliki zaidi ya milioni 2.5 za watanzania ambazo mnategemea kwenda kuzipima. Nikuombe na niombe Serikali yangu pamoja na Waziri wa Fedha tusaidie huu

mkopo uwe *accessed* mapema lakini pia ukishakuwa *process* mapema huu mkopo na Serikali yetu ikaweka fedha hizo ambazo ziko kwenye bajeti wakapime sasa hizi ardhi za watanzania, tukipima ardhi nyingi za watanzania kupitia fedha hizi ambazo tunategemea kupata kwa wenzetu wa Korea banki ya *Exim* na fedha za kitanzania za kwetu itatusaidia hata kuongeza mapato kwa wizara hii na kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi tumepanga kukusanya bilioni 200 kwa wizara hii lakini ardhi ikipimwa ikamilikishwa maana yake kodi ya ardhi sasa itaweza kulipika na tunaweza tukategemea chanzo hiki cha ardhi ikatusaidia sana katika kuongeza bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, niombe hili lifanyike mapema na uhakikishe kwamba fedha hizi zikipatikana tunakwenda kupima upesiupesi.

Mheshimiwa Spika, masuala ya msisitizo ambayo jioni ya leo nilitamani niongee na Serikali yetu na Mheshimiwa Waziri ni hayo matatu:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza niombe muangalie kwenye msisitizo ambayo kwamba nishauri Serikali muangalie *projection* zetu hizi, tumekusanya bilioni 84 mpaka sasa ya kodi ya ardhi, lakini tulitegemea kukusanya bilioni 180, lakini tukawa na hiyo *deficit* lakini tume project bilioni 200.

Mheshimiwa Waziri nikuombe tuangalie vizuri tufanye *review* ya viwanja tulivyonavyo kwa nchi nzima ili tuone kwa nini havikusanyiki labda kodi ya ardhi ipo juu tunaweza tukafikiria kwamba tukapunguza hivyo viwango vikawa *affordable* kwa watanzania wakaweza kulipa au kuna *staffing* ndogo kwenye ofisi za ardhi wanashindwa kufatilia au ile 30 *percent* ya *premier rotation* ya kodi ya ardhi ya halmsahauri zetu imeathiri makusanyo ya kodi ya ardhi kwa hiyo niombe Serikali yangu kwa nia njema muweze kufanya *review* ya makusanyo ya kodi ya ardhi wapi tunakwama kama ni ile 30 *percent retation* ya *premier* kwenye

halmashauri zisaidie kwa ajili ya *movement* ya kukusanya kodi ya ardhi basi Serikali yangu muifanyie maamuzi ya haraka.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili niombe sasa viongozi wetu wakuu Mheshimiwa Rais pia tumuombe kwamba kwenye mipaka kuna *bicons* ambazo zinatakiwa zifufuliwe mimi ni mjumbe wa kamati, tumetembelea Horo horo, tumekwenda Tanga, tumekwenda Namanga tumeona kuna wavamizi wachachewachache, kwasababu tu zile bikoni hazionekani kwa ajili ya mipaka ya nchi yetu, niombe basi viongozi wetu wa nchi hizi mbili wakae, Mheshimiwa Waziri uongee na Mheshimiwa Rais pia wapi tunakwamba kwa nini wakenya wao hawataki kuona tumalize hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hatufurahishwi sisi nchi yetu pawepo na wavamizi na baadhi ya watu wawe na hatimiliki katika ardhi yetu kwa sababu tu tumeshindwa kufufua zile bikoni za mipaka. Niombe wizara yetu na Serikali yetu watoe fedha ambazo zitasaidia kuchonga barabara mipakani katika nchi yetu lakini kufufua zile *bicons* zile ambazo hazionekani itaondoa uvamizi katika mipaka yetu na Serikali iweze kutoa fedha mapema.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwasababu muda hauruhusu niwashukuru sana wana babati kuniamini na kunituma katika Bunge hili niwasemee na amini mengi tumefanya na nimachache ambayo yamesalia ambayo yalikuwa yanafanyiwa kazi na ninaamini Mheshimiwa Waziri tutakapoendelea kukuletea mezani kwako yatatuliwa ikiwemo mgogoro wa shamba la Dudumera ambao mpaka sasa tunashughulikia tuone ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukarekebisha ile mipaka ili wananchi wa Kijiji cha Malangi waweze kuona jinsi gani wanaweza wakapata ile ardhi.

Mheshimiwa Spika, zaidi sana niwatakie kila kheri Serikali yetu hii ni bajeti nzuri mmegusa na mmeonyesha *focus* ya ni jinsi gani mnakwenda kutatua matatizo ya ardhi katika maeneo yetu haya yote tukiyafanyia kazi nina amini ardhi ya watanzania itakuwa imepimwa na itakuwa imemilikishwa na sasa watanzania migogoro ya ardhi itakuwa imeondoka

tutakuwa hatuangaiki kutatua migogoro hizi fedha zitasaidia kupanga ardhi hati zitatolewa wale makamshina wataenda kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba niunge mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Nnauye.

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hoja iliyoko mezani ya Wizara yetu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Pia kama mjumbe wa kamati naungana na wenzangu waliotangulia kumpongeza Waziri Mheshimiwa William Lukuvi, Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula, Katibu Mkuu dada yetu Mary Makondo na Naibu wake Ndugu yetu Nicolaus Mkapa kwa kazi nzuri waliyoifanya katika Wizara hii katika kipindi hiki ambacho tunakuja kukihitimisha leo bajeti hii iliyopita na kuanzisha nyingine pamoja na Watendaji wote wa Wizara. Kwa kweli Wizara hii ndiyo Wizara mama na Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwenye hotuba yake amekiri kwa kusema kwamba ni Wizara wezeshi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama inavyosemekana kwamba ardhi ndiye mama wa kila kitu basi Wizara hii mnayoisimamia ndiye mama wa Wizara zote maana yake zote zinategemea ardhi katika kufanya kazi zake. Nawapongeza sana sana sana bila kumsahau Rais wangu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambaye ndiye mtoa dira ya jinsi nchi hii inavyoendeshwa na hajabakiza pia Wizara hii ya ardhi. Kwa sababu kupitia hekima zake ndiyo maana vile vijiji 900 vilivyokuwa katika maeneo ya hifadhi yaliweza kurejeshwa mikononi mwa jamii.

Mheshimiwa Spika, nachingia tu mambo kama manne katika Wizara hii ambayo tumeshaitolea maoni ya kutosha katika taarifa yetu ya kamati. Sehemu ya kwanza nilipenda kugusia hili suala la kuanzishwa Ofisi za Ardhi za

Mikoa, hili ni jambo la kupongeza sana na ni jambo ambalo binafsi linanitia faraja na hasa endapo watakwenda kufanya kazi kwa kasi kubwa na kuwekeza nguvu nyingi zaidi katika migogoro tuliyonayo katika vijiji mbalimbali, katika kata mbalimbali, tarafa mbalimbali hata mipaka ya wilaya na wilaya na mkoa na mkoa.

Mheshimiwa Spika, namini kwamba Mheshimiwa Waziri pamoja kwamba sijaona scope ya kazi yao kikamilifu hawataishia tu kwenye zoezi la kupima viwanja sijui kurasimisha makazi wataenda mbali zaidi na kukusaidia katika kero za ardhi na migogoro ya mipaka. Wewe mwenyewe nafahamu utendaji wako, nafahamu kule maeneo ya *Lake Natron* kulikuwa na mgogoro wa miaka mingi ambayo uliniahidi ungekuja kuwasaidia wananchi kulimaliza lakini baada ya muingiliano wa mvua nyingi baadaye Corona hatukuweza kwenda. Lakini inawezekana sasa umeshapaleka mkono wako mpaka ngazi ya mkoa na wao utawashusha kule wakamalize ule mgogoro wa mipaka yote ya Longido maana nilishakuorodheshea yote.

Mheshimiwa Spika, kuanzia *Lake Natron* Magharibi kabisa mwa Wilaya yangu panapopakana na Ngorongoro na sehemu kidogo Monduli mpaka mwisho wa Wilaya yangu kule tunapopakana na Wilaya ya Rombo ukazungukia Siha ukaja Arumeru.

Mheshimiwa Spika, nimekutajia sehemu zote zenye migogoro; iwe ni Kijiji iwe ni Kata, iwe ni Tarafa; na ninaamini kwamba moja ya kazi ambayo nitawapa hawa hasa waliokuja Mkoa wa Arusha ni kumaliza migogoro. Sehemu ya kuwatathmini *(performance evaluation)* naomba iwe ni kuangalia ni kwa kiwango gani wamemaliza migogoro sugu tuliyonayo katika Wilaya, Halmashauri na vijiji mbalimbali vya nchi yetu. Hilo lilikuwa ni jambo la kupongeza kwamba umetuanzishia hizo Ofisi za Mkoa, naomba kazi yao kubwa ielekee katika kumaliza migogoro.

Mheshimiwa Spika, tuna migogoro hata mpaka ya mashamba ya watu na watu. Kwa mfano kuna mgogoro wa

mkulima mmoja na wenzake katika Kijiji cha *Olomolo* una miaka miwili sasa. Migogoro tu ya watu wanaogombania mipaka ya mashamba. Labda kwa sababu hatukuwa na chombo mahususi chenye zana na uwezo, tunajikuta migogoro mingi haiishi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo napenda kuchangia ni jambo la hii Tume ya Mipango ya matumizi ya ardhi na yenyewe tumeiandikia kwenye ripoti kwamba ipandwe hadhi iwe wakala. Wakati huo huo nimeona kwenye randama kwamba moja ya majukumu yao muhimu ni kuziwezesha Idara za Ardhi za Halmashauri katika utendaji wao wa kazi wa kuendelea kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi na kufanya mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kabisa Waziri asimamie pia hili ahakikishe kwamba hii Tume ambayo bado ni Tume, lakini tunategemea andiko la kuifanya iwe mamlaka itakwenda kukamilika hivi karibuni, kuhakikisha inaongezewa nguvu ya ziada ili waweze kutimiza wajibu huo wa kuzijengea Halmashauri zetu Idara za Ardhi uwezo wa kutenda kazi za upimaji, upangaji, urasimishaji na uwekaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi hasa katika ngazi ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nimeona kwamba kuna changamoto kubwa hata kwenye randama, Mheshimiwa Waziri mwenyewe amekiri kwamba hii Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ina uhaba mkubwa sana wa wafanyakazi. Watumishi ni wachache, hawafiki hata asilimia 50 ya wanaohitajika. *In fact* wako 50 sasa hivi wakati wanahitajika 130. Sasa nashangaa kwamba Serikali ina mpango gani, kwa sababu iko kwenye mkakati wa kupandisha hadhi iwe mamlaka ya kumaliza huo upungufu wa watumishi katika hiyo Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, nilitaka kuongelea hili suala la uimarishaji wa mipaka ya Kimataifa. Hili ni suala ambalo linaendelea kwa kasi ndogo mno. Kama Wajumbe wa Kamati, tunaelewa kwamba kuna shida pia ya *speed* ya nchi nyingine katika kuitikia makubaliano katika hii mipaka.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo napenda kuliangaliza, kuna mipaka ambayo lile eneo la *noman's land,* lile eneo la kutenga nchi na nchi limevamiwa, watu wameingia mpaka mtu akitema mate dirishani mwa nyumba yake anatemea nchi ya jirani mwenzake. Eneo moja mahususi ni eneo la Kamwanga. Kule Kamwanga kuna eneo linaitwa Esangarine ni Kitongoji, kuna zaidi ya kaya 271 sasa hivi, wameishi pale kwa miaka wakitegemea vibarua vya kupalilia mashamba ya nchi za jirani tunazopakana nayo ya Kenya na mashamba ya miti katika msitu wa Taifa wa Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, wale wananchi hawana maisha yao ya baadaye, wanaishi katika eneo la mpaka wa Kimataifa ambalo leo tukidhibitisha hiyo mipaka, hawana pa kwenda. Kilio chao ni kwamba Serikali iwatafutie ardhi ya mbadala kama wakati wa Serikali ya Mheshimiwa William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu alipowatoa wale waliokuwa wameishi katika misitu ya Londorosi ikawapa eneo la kijiji katika eneo la shamba la *NAFCO* ambalo lilikuwa sasa hivi lina jina linaitwa Mji Mwema katika Wilaya ya Siha.

Mheshimiwa Spika, wale wananchi waondolewe pale maana japo umeme unapita pale, hawawezi kupewa, maana yake siyo makazi rasmi. Hawana shule, watoto hawa wanasoma katika shule za nchi ya jirani. Watoto wengine inabidi wawatafutie mahali pa kwenda kukaa ili waende shule, hawana huduma yoyote, wanaishi kwenye *shacks*.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho kwa sababu ya muda, ni hali halisi ya uhaba wa ardhi katika vijiji vilivyopo katika ukanda wa *West Kilimanjaro*. Tukianzia Ormolok, Leranga, Kitenden, Rikasua, mpaka Kamwanga wale watu wanaishi kwenye *strip* yaani ni uzi mwembamba wa kipande cha ardhi kinachotenga nchi ya jirani ya Kenya na hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, miaka ya 1960 wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza, Rais wa Awamu ya Kwanza, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alishatambua uhaba wa ardhi na haja ya kuwa na maeneo ya malisho ya mifugo,

akawatengea hekta 5,500 ambazo walikuwa wanaruhusiwa kama *buffer zone* wachungie ngombe tu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kwa sababu ya ongezeko la watu, ilifika mahali watu wa Kata ya Ormolok hawana hata pa kujenga sekondari wakati wa suala la kujenga Sekondari za Kata. Wakaomba katika lile eneo la *buffer zone* wakatoa sekondari inaitwa Enduimet Sekondari, watu wa Kamwanga zaidi ya 11,000 hii leo nao wanahitaji kujenga Sekondari ya Kata. Sehemu iliyobaki ni hako ka-*buffer zone* tu. Hao pia walikuwa na kilio hicho, hata wananchi wa Kijiji cha Kitende hawana hata eneo la uwanja wa mpira wa miguu kwa ajili ya vijana. Wanaomba tu pembeni ya ile barabara inayokwenda Kamanga inakuja Siha, hata wapewe hizo mita 100 kwa 50 wapate sehemu ya kujenga uwanja wa mpira. Hiyo ni shida kubwa, lakini vile vijiji vya muhimu vinavyotulindia mipaka, vinahitajika. Kuna haja ya kuangalia suala la mipango ya matumizi bora ya ardhi katika eneo lile na kuthibitisha zile hekta 5,500 ambazo mwalimu aliwapa kwa ajili ya kuendelea kufugia mifugo hasa wakati wa kiangazi na maisha yao yaweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kulikuwa na adha nyingine ambayo imejitokeza sisi kupitia Kamati yetu ya Ardhi, kuna wananchi ambao wanakereka sana na suala hili la urasimishaji wa makazi. Wapo warasimishaji wa Serikali na kuna wakandarasi. Kuna wakandarasi ambao hawana fedha na hawampimii mtu eneo mpaka walipwe na kuna maskini wasio na uwezo wa kurasimishiwa maeneo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ikaliangalie suala hilo, iwe ni suala la kati Halmashauri na Serikali, kwamba mpaka fedha zipatikane, wawekane sawa na mkandarasi. Mkandarasi asiende kuwashikia wananchi bango kwamba hawapimiwi maana hawana fedha, kwa sababu kwa njia hiyo hatutakaa tuweke matumizi bora upangaji, umilikishaji na mipango sahihi ya matumizi ya ardhi yetu ambayo tumeshaamua kwamba tunakwenda sasa kupanga, kupima na kumilikisha.

Mheshimiwa Spika, hayo ni ya kwangu. Nashukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, nilishamtaja Mheshimiwa Nape Nnauye, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kidogo kwenye haya mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Na mimi nampongeza sana ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Lukuvi kwa kazi nzuri aliyoifanya kwenye Wizara hii. Ni ukweli usiofichika kwamba ametumia uzoevu wake kutuliza Sekta ya Ardhi katika nchi yetu na kazi nzuri amefanya yeye pamoja na dada yangu Mheshimiwa Mama Mabula, wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ilikuwa ina kelele nyingi na ilikuwa ina matatizo makubwa, lakini wamefanya kazi nzuri pamoja na Watendaji walioko chini yao; Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja, Makamishna na kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa namshukuru kwa uamuzi wa kutuletea ofisi yetu pale Lindi, maana tulikuwa na taabu ya kwenda kutafuta huduma Mtwara. Tunakushukuru sana wananchi wa Lindi, tunakutakia kila la heri. Tunaamini kwamba kazi hii umeifanya ya kizalendo, tutakukumbuka kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mambo machache sana kwenye taarifa ya Kamati nami ni Mjumbe wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge. Kuna mambo mengi sana yamezungumzwa, sasa nataka nizungumze machache ambayo pengine hatukuyaweka mle ndani. La kwanza, ni suala la Shirika la Nyumba la Taifa. Tunajua limepitia mchakato wa kuliboresha na katikati pale wengine tulipata shida yalipofanyika mabadiliko, lakini kwa kweli inavyoonekana haya mabadiliko yamekuwa na tija. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi wa Shirika hili

la Nyumba, Dkt. Maulid kwa kazi nzuri sana anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesikia hapa kwamba shirika hili sasa linaaminiwa na kupewa kazi; wamepewa kazi ya kujenga Hospitali ya Rufaa Mtwara, kazi ya kujenga Hospitali ya Rufaa Musoma, kazi ya kujenga machinjio pale Dar es Salaam na pia wanapewa na kazi nyingine. Huu ni mwanzo mzuri sana wa kulifanya shirika letu liimarike. Nampongeza Dkt. Maulid na Bodi pamoja na timu nzima ambayo inafanya kazi ya kuimarisha hili shirika letu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, kuna sheria ambayo inaisimamia shirika hili. Sheria ya mwaka 1990 nadhani ya Shirika la Nyumba la Taifa, ukiisoma inaorodhesha mambo mengi, lakini kuna eneo linazungumzia Bodi ya Wakurugenzi ambayo italisimamia hili shirika. Sasa ile orodha ya Wajumbe wa Bodi wanaorodheshwa Wajumbe wengine wote, lakini Mkurugenzi wa Shirika la Nyumba hatajwi popote na matokeo yake anakuwa sio mjumbe halali wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa maboresho ya utendaji wa Bodi nadhani ni vizuri kipengele hiki kikaangaliwa ili Mkurugenzi wa Shirika la Nyumba awe sehemu ya Bodi ya Wakarugenzi, itasaidia sana kuboresha utendaji kazi wa hii Bodi. Nadhani ni jambo ambalo linawezekana, sidhani kama ni jambo gumu.

Katika hizi hatua za maboresho ya kuhakikisha shirika linafanya vizuri, basi sheria hii ipitiwe upya, tumwingize Mkurugenzi wa Bodi na Mkurugenzi wa Shirika la nyumba awe sehemu ya Bodi ili mambo yaende vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tumekuwa tukizungumza namna ya kupanua wigo wa walipa kodi, namna ya kupanua wigo wa kuongeza mapato kwa sababu inavyoonekana kwa mfumo wetu sehemu kubwa ya kodi inabebwa na watu wachache sana. Kama kuna eneo Serikali ingepata fedha za kutosha ni kwenye kuiwezesha Wizara hii ikahakikisha imepima kila kipande cha ardhi na kila kipande

cha ardhi kikamilikiwa. Maana yake tungekuwa na wigo mkubwa sana wa walipa kodi na tungepunguza mzigo wa kubeba kodi kwa watu wachache.

Mheshimiwa Spika, sasa wito wangu, hili jambo limekuwa linazungumzwa mara kwa mara na wenzetu hawa akina Mheshimiwa Lukuvi wamekuwa hawapati fedha za kutosha, matokeo yake upimaji umekuwa unakwenda kidogo kidogo. Nimesikia ipo mipango ya Benki ya Dunia, South Korea na Serikali yenyewe. Wito wangu ni kwamba jambo hili likamilike, tupunguze mzigo wa walipa kodi kwa watu wachache, tuwaingize watu wengi kwa kipima ardhi yote na kuwamilikisha na ukusanyaji wa kodi ya ardhi siyo kazi kubwa, gharama yake ni ndogo ukilinganisha na ukusanyaji wa kodi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilidhani Serikali ingefanya makusudi kabisa tuwape fedha ya kutosha, tuweke mkakati wa kutosha, tujibane kwa muda mfupi tupime tumilikishe ili tukusanye kodi ya kutosha bila tatizo.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, kazi kubwa ya Wizara hii ni kusaidia Watanzania wawe na makazi. Pamoja na makazi, isaidie watu kumiliki nyumba zao. Sasa tumekuwa tukizungumza ndani ya Kamati juu ya ukamilishaji wa Sera ya Nyumba, juu ya ukamilishaji wa Sera ya Makazi. Nadhani hili ni la msingi sana. Limechukua muda mrefu, tumesuasua kwa muda mrefu, hebu likamilike tuwasaidie Watanzania wapate mahali pazuri pa uhakika na watu waweze kumiliki nyumba bila kuwa na migogoro ambayo ipo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukiona wamiliki wengi inabidi wawe na kona nyingi mno kupata fedha, kutafuta namna ya kupata mikopo. Umilikaji wa nyumba unakuwa na shida, lakini naamini sera ikikamilika mambo haya yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, nirudie kuwapongeza Wizara, kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nape Nnauye. Sasa Mheshimiwa Musa Bakari Mbarouk atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia afya njema tukiwa wazima wa afya na kuendelea na shughuli zetu za kila siku za Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kuzungumzia ambayo sasa imekuwa kama agenda ya kudumu, suala la *Corona*. Namwomba Mwenyezi Mungu azidi kutusalimisha na atukinge na maradhi haya ya *Corona* katika nchi yetu, Afrika na Dunia kwa ujumla. Pia kuna changamoto za hapa na pale. Kwa mfano leo nimepigiwa simu na baadhi ya wapiga kura wangu katika Jiji letu la Tanga kwamba kumekuwa na shida kidogo, kwamba mtu anapogundulika kwamba ameathirika na maradhi hayo, basi anapochukuliwa vipimo kama ana maradhi mengine ambayo yameambatana na hayo; labda ana Malaria au *Typhoid* imekuwa sasa hapimwi. Hatibiwi, anaambiwa mpaka yatakaporudi majibu kutoka Muhimbili, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niishauri tu Serikali na Wizara ya Afya kwamba hii itasababisha sasa Watanzania wafe na yale maradhi mbadala ya *Corona*. Kwa hiyo, naishauri Serikali na Wizara ya Afya watu watibiwe maradhi mengine ambayo yameambatana huku wakisubiri majibu kutoka Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, linguine, naishauri tena Serikali kwamba inakuwa ni ngumu sasa kwamba kipimo cha maradhi ya *Corona* lazima mpaka vifikishwe Dar es Saalam. Kwanza inakuwa ni mkusanyiko mkubwa na mlundikano; pia watu wanachelewa kurudishiwa majibu. Sasa naomba uwezekano kama upo Serikali ifanye mpango wa dharura ikibidi kila mkoa wapate kipimo chao ili tuepushe huu

msongamano wa hivyo vipimo ambavyo vyasubiri majibu Dar es Saalam.

Mheshimiwa Spika, lingine, maiti ambazo wanakuwa nazo kwa walioathirika na *Corona,* wamekuwa wananchi wetu nao wana taabu ya kuwapata. Zipo maiti karibu za watu wawili zimezuiwa takribani wiki na kama tunavyojua Waislamu mtu akifa anatakiwa asicheleweshwe kuzikwa. Sasa zinazuiwa hali ya kuwa watu sasa wanapiga simu wakati wote. Mimi nimewasiliana na Daktari wa Mkoa nimpigie Mkuu wa Mkoa. Kwa hiyo, naomba kama mtu ameshakufa, basi ule utaratibu wa kiserikali wa kuwazika ufuatwe ili ndugu zao waridhike kwamba maiti wao wamefika salama mikononi kwa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwenye Jiji letu la Tanga, nami nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi amekuja Tanga mara kadhaa na tumekutana na baadhi ya changamoto zimekwisha, lakini nimjulishe tu kwamba kuna baadhi ya changamoto bado zipo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lukuvi kwenye eneo la Tanga nakumbuka watu walikutana Tangamano wakitoa maoni yao, lakini sasa akatoa maamuzi kwamba wale watu basi walipe. Kama sikosei walipewa miezi mitatu. Sasa katika mazingira ya kawaida mtu kupata shilingi milioni mbili kwa wakati mmoja ndani ya miezi mitatu inakuwa ni ngumu.

Mheshimiwa Spika, sasa watu wa Tanga maeneo ya Kange na kwingine wamenituma, wanaomba wakubaliwe walipe kwa awamu, kidogo kidogo *(installment)* na hata maeneo mengine pia Tanzania kwamba waliopewa siku 90, wakishindwa wapokonywe viwanja, naomba Serikali iwaonee huruma hasa kwa kuwa Serikali hii ya Awamu ya Tano ni sikivu na Serikali ya wanyonge, basi wale wanyonge angalau walipe kidogo kidogo. Wakubaliwe mtu atakapokuwa amemaliza malipo, basi ndio apewe hati yake na risiti. Wengine wanapandwa na *pressure* kuona kwamba

baada ya miezi mitatu sijalipa shilingi milioni mbili za kiwanja, nanyang'anywa. Hilo naomba lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye Kata ya Mabokweni pamoja na Kata ya Kiragi kuna mgogoro. Kuna iliyokuwa Kampuni ya *Amboni Limited* ikishughulika na masuala ya mkonge. Wakati Waziri wa Kilimo akiwa ni Mheshimiwa Edward Lowassa wananchi wa maeneo hayo waliomba, kwa kuwa kuna maeneo yalikuwa hayalimi mkonge, wakaiomba Serikali kupitia Waziri wa Kilimo, wawaombe ile kampuni wawape yale maeneo walime mazao ya chakula. Wakakubaliwa, wakapewa.

Mheshimiwa Spika, wamelima, imepita miaka mingi tu, wamepanda mimea; minazi, michungwa, mikorosho, miembe imekwishazaa sasa, hii kampuni ikaja ikabadilishwa jina kutoka *Amboni limited,* kuna kampuni waliingia nayo ubia sasa inaitwa *Cotel. Cotel* wanasema hawatambui yale maeneo wananchi waliyoombewa na Mheshimiwa Lowassa. Wamechukua hayo maeneo, wamesema wanarudisha kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, sasa watu wanategemea Tanga ulikuwa ni mji wa viwanda, viwanda vingi vimekufa, watu wamejiingiza kwenye kilimo. Sasa wamenyang'anywa maeneo yao, imekabidhiwa Kalmashauri. Hivi ninavyokwambia, imeshapigwa mipaka, minazi imevunjwa, michungwa, milimao, minanasi, mifenesi na miti mingine. Wananchi wale sasa wamerudi katika wimbi la umasikini na wanaambiwa kwamba wao hawatolipwa fidia kwa sababu ni wavamizi.

Mheshimiwa Spika, sasa mvamizi huyu ambaye tangu mche umepandwa wa mnazi au mwembe mpaka umezaa, leo *Cotel* inakuja inasema wao hawatambui wakati miongoni mwao wale waliopewa yale mashamba walikuwa ni wafanyakazi wa Kampuni ya Amboni ambayo sasa ilifilisika, ndiyo ikatafuta ubia na *Cotel!* Sasa hili nalo namwomba Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi kwa sababu wananchi wale sasa wamerudi katika wimbi la umasikini. Tukumbuke

wanasomesha, wana mahitaji yao na kipato cha kila siku. Kwa hiyo, nakuomba ulifanyie kazi. Maeneo hayo ni maeneo ya Kata ya Mabukweni Kata ya Mzizima kwa maana ya Amboni na maeneo ya Kilare.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ayachukue hayo nayo ayafanyie kazi. Maeneo mengine kuna mgogoro kama huo kwenye Kata ya Marungu eneo la Mkembe, kulikuwa na shamba la mkonge, shamba lile likatelekezwa. Waliokuwa wafanyakazi walikuwa hawalipwi mishahara, wakaamua sasa kwa sababu hatulipwi mishahara na ilikuwa ni zaidi ya miaka 20; na kuna Sheria ya Ardhi Na. 4 ile ambayo unaisema mara kwa mara inayosema: "*whether you have titled or not, so long you have been there for long time, customary law recognize you as the owner of the land.*" Sasa wameshakaa. Wanasheria wakaitafsiri hiyo "*long time*" ni zaidi ya miaka 12. Sasa wapo kwa miaka 20, lakini wanaambiwa nao wamevamia, shamba lile sasa hivi wanapelekwa puta, wanaambiwa waondoe mazao yao. Naomba nao pia hilo Mheshimiwa Waziri atusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine kwenye Kata ya Tangasisi kuna eneo lilipangwa viwanja vya wanajeshi, wananchi wa pale nao wamepata athari kidogo kuna mtafaruku. Wamelipwa kama kumi na wapo watu kama 40. Naomba Mheshimiwa Waziri aliingilie kati, walipwe wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, suala la hatimiliki za kimila. Kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri ameeleza watu takriban 3,000 wamepata mikopo, takribani bilioni 60 zimetumika, lakini kwenye Jiji letu la Tanga au Mkoa wetu wa Tanga, kwa sababu najulikana ni Mbunge wananchi wanakuja kuniuliza; hizi hatimiliki mbona wakienda kwenye taasisi za fedha hazitambuliwi? Hebu tuambiwe labda benki gani ambayo inatambua kwa sababu wananchi wanahangaika. Yupo mtu mmoja kutoka Lushoto alipata ajali ya kuunguliwa na duka lake, akawa na hatimiliki akaniambia Mheshimiwa nataka ukawe mdhamini wangu *NMB* nikachukue mkopo. Nimeongozana naye mpaka *NMB,* kufika pale wanasema hizi hati za kimila sisi hatuzitambui.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niombe tu na kuishauri Serikali; kwa kuwa Watanzania asilimia 70 ni wakulima maskini wako vijijini na Serikali yetu inafanya jambo zuri sana la kutoa hati miliki za kimila, lakini basi Serikali iwe dhamana ya kuwadhamini hawa wananchi ambao wana hati za kimila wakopeshwe ili waweze kulima kilimo cha kisasa, wajenge nyumba bora za kisasa, wawe na mifugo mizuri ya kisasa. Tutawasaidia katika kuondokana na wimbi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala zima hili la halmashauri kwenye masuala ya upimaji. Katika eneo la Jiji letu la Tanga, eneo la Ngamiani kwa maana kuanzia Barabara ya Kwanza mpaka Barabara ya 21. Mpaka leo Mheshimiwa Waziri watu wana ofa tu hawana hati. Ukiangalia gharama za kupima ardhi sijui kwa nini zinakuwa ni kubwa hali ya kuwa vile vifaa vya kupima siyo vya kuharibika au havimaliziki kama vile chaki kwamba jinsi unavyopima basi inamalizika, lakini unakuta gharama za kupima ardhi ni kubwa sana. Niiombe Serikali mtuletee fedha Tanga ipimwe sasa Ngamiani yote; kuanzia Barabara ya Kwanza mpaka Barabara ya 21 na ikibidi watu wapewe hizi hati kubwa za kisasa. Kwa sababu inakuwa sasa ni changamoto mtu anapotaka kupimiwa ardhi na kupata hati panakuwa na taabu kidogo. Niiombe Serikali itakapokuwa inapima yenyewe kama Serikali au kama halmashauri, gharama zitakuwa ni ndogo na wananchi wetu wataweza kunufaika na watakuwa na hati zao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kuna suala zima hili la ardhi iliyotwaliwa na Mamlaka ya Majitaka kwa ajili ya kuweka mabwawa ya kusafisha majitaka. Wapo wananchi wenzetu Watanzania ambao maeneo yao yamechukuliwa, takribani kama watu sitini hivi, maeneo ya Machui. Lakini kuna majina ntayataja hapa; kuna Abbas Mwakichui, Zongo Zongo, Kivyere Mchunga na Mburuli Mchunga. Haya maeneo yamechukuliwa lakini Tanga *UWASA* au Mamlaka ya Maji wamekwishatoa milioni 450. Sasa halmashauri wanasema hawawezi wakalipa kwa sababu gharama ya hilo eneo ni milioni 700, mpaka Mamlaka ya Maji watakapotoa milioni 700 zote. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri awaruhusu

Halmashauri ya Jiji la Tanga wale ambao wataweza kunufaika au kama zitatosha hizi pesa kwanza waanze kulipwa milioni 450. Baadaye zikija hizo nyingine hiyo ni awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na namshukuru Mheshimiwa Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk. Nilishakutaja Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Chatanda.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa uhai, lakini nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongea leo katika hotuba hii ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Lukuvi. Mimi niseme ukweli nimekuwepo hapa Bungeni tangu mwaka 2000 kwa hiyo nimekutana na Mawaziri wa Ardhi wengi kwelikweli. Ilikuwa ikifika wakati wa hotuba ya ardhi kama leo basi huyo Waziri lazima apoteze kilo mbili, tatu, ilikuwa ni vurugu kwelikweli, lakini Mheshimiwa Lukuvi kwa moyo wangu wa dhati kabisa nimpongeze kiasi kikubwa sana jinsi ambavyo anaitendea haki Wizara hii ya Ardhi, lakini anamtendea haki pia na aliyemteua kuwa Waziri wa Ardhi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongea suala moja tu kwenye hotuba hii na suala hili Mheshimiwa Waziri analifahamu vizuri, analifahamu vizuri sana na anakumbuka kwamba tarehe 30, Oktoba, 2018 alifunga safari na gari yake vizuri akaenda katika Kata ya Ndungu, akazungumzia mgogoro mkubwa na tatizo kubwa lililopo kwenye Kata ya Ndungu ambako ndiyo Makao Makuu ya Jimbo la Same Mashariki. Nakumbuka alikuta tatizo la ardhi ya makazi kwa vijiji vitatu pale Ndungu; Kijiji cha Ndungu, Kijiji cha Mpirani na Kijiji cha Misufini. Kwenye mkutano ule wananchi walifurika sana na walilalamika sana kwamba hawana ardhi ya makazi na hata mahali pa kuzikia.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, naomba nikiri kwa sababu mimi natoka Kata ya Kihurio, ni kilometa saba tu ufike Kata ya Ndungu. Nimezaliwa pale, nimeishi pale, naifahamu Kata ya Ndungu, ni kata ambayo ina wakazi wengi sana lakini ardhi ni mgogoro mkubwa. Ardhi kubwa iliyopo ina maji, hapa ninapoongea na Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Kijiji cha Misufini akinamama wanapikia nje maana yake ndani ya nyumba kuna maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri sasa nimkumbushe kwamba baada ya wananchi kulalamika sana kwake yeye mwenyewe akatamka kutoa ardhi ekari 100 kwa Kijiji cha Misufini, ekari 100 kwa Kijiji cha Ndungu, ekari 100 kwa Kijiji cha Mpirani, lakini Mheshimiwa Waziri tangu alipoondoka ni kweli wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Same walihamia pale na wakawaambia wananchi wakae waangalie ile ardhi waeleze ni wapi panafaa kugawiwa. Walifanya hivyo, walikuja na wakajadiliana na wananchi wakaelewana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea tangu tarehe 30, Oktoba, 2018 mpaka leo kilio cha wananchi wa Misufini, wananchi wa Ndungu, wananchi wa Mpirani, kipo palepale. Wananachi wanaishi kwa taabu, akifariki mtu Ndungu, Mpirani, Misufini ni shida tutamzika wapi. Maamuzi aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri siku ile ilikuwa ndiyo kuishi kwa wananchi wa Ndungu lakini hakuna kilichotekelezwa mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, leo basi ndani ya Mjengo huu wananchi wa Ndungu, Misufini na Mpirani watapenda wasikie kwamba hili jambo linatekelezwa lini kwa sababu 2018, 2019, 2020. Nimnyenyekee nimwombe kwamba matamko, matendo, maamuzi na utekelezaji wake utakuwa umekitendea haki Chama cha Mapinduzi Oktoba, 2020 kwa sababu hii kero ni kubwa sana kwa wananchi wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme ukweli, nina uhakika nimemkumbusha Mheshimiwa Waziri kwa sababu kazi zake ni nyingi sana na hii Wizara ameishika vizuri. Naomba na nimnyenyekee, wananchi hawa wanamlilia Mheshimiwa

Waziri, hawawezi kuja hapa ndani, kwa hiyo wamenituma, mimi ni Mbunge wa Taifa, kwa hiyo hata wananchi wake wana haki ya kunituma, hata wa Nyang'whale wana haki ya kunituma, hata wananchi wa Peramiho wana haki ya kunituma. Kwa hiyo wananchi wa Same Mashariki wamenituma nami namnyenyekea Mheshimiwa Waziri, awatendee haki, awaangalie wananchi hawa, akiangalie na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, hilo ndilo lililokuwa jambo langu la kuongea. Nakushukuru sana kwa mapenzi makubwa uliyonionesha. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na ndiyo huwa nazungumza kwamba Wabunge wa muda mrefu hawaji na mambo kumi, kama mlivyoona Mheshimiwa Anne Kilango, amekuja na jambo mahususi akaliongelea jambo lake mahususi. Kwa vyovyote vile Mheshimiwa Waziri, Naibu na Maafisa wanakuwa wamelipata vizuri kuliko kurukaruka kuna hili na hili na lile, unakuwa mwisho wa siku hakuna ambacho kimechukuliwa. *(Makofi)*

Nilikutaja Mheshimiwa Mary Chatanda na utafuatiwa na Mheshimiwa Joyce Sokombi.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri, Naibu Waziri na watendaji wakuu wa Wizara hii ya Ardhi kwa namna ambavyo wamefanya kazi kubwa kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge kila mmoja anatoa sifa zile ambazo tunadhani ni halali yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa maneno ya kunukuu ya Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambayo yanaishi mpaka sasa. Nanukuu; *"Nchi hii kamwe haitaongozwa na viongozi wazembe. Naona kuna watu wanadhani Kiti cha Urais ni cha starehe sana; huwezi*

*kuwa Rais kama huna uchungu na Watanzania. Najua Taifa hili limeliwa sana, lakini kuna awamu inakuja itakayoirudisha Tanzania kwenye heshima yake na dunia nzima itashangaa." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona niyaseme haya kwa sababu yako mambo makubwa ambayo yamefanywa ndani ya nchi hii kwa mujibu wa taarifa aliyoiwasilisha Waziri wa Ardhi. Kwanza amesema ujenzi wa reli ya kisasa ya *standard gauge,* amesema kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania, mambo ambayo yamefanyika hayo. Anasema ujenzi wa bwawa la uzalishaji umeme la Julius Nyerere, lakini vilevile ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwa maneno ya Hayati Baba wa Taifa hayo aliyoyasema kwamba kuna awamu inakuja itakayoirudisha Tanzania kwenye heshima yake na dunia nzima itashangaa. Sasa wananchi kwa maana ya wananchi pamoja na dunia kwa ujumla wanashangaa kutokana na matendo makubwa ambayo yamefanywa katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwapongeza hii Wizara ya Ardhi, kazi ambazo wamezifanya ni pamoja na kupunguza migogoro ya ardhi ya wakulima na wafugaji, sasa hivi angalau hatusikii migogoro mikubwa ile iliyokuwepo kila wakati. Ikishafika kipindi cha Wizara hii pamoja na maliasili ilikuwa humu ndani moto unawaka, lakini sasa hivi kumetulia, mambo yanakwenda vizuri na wananchi tayari wamepata watu ambao wamefanya kazi kubwa ya kuwatuliza na kuhakikisha kwamba wanapata haki zao.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kutoa pongezi kwa Wizara hii kwamba kazi kubwa wameifanya pamoja na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na maelekezo yake alivyoagiza kwamba hataki kusikia habari ya migogoro inayohusiana na mambo ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nami katika Wilaya yangu ya Korogwe, Halmashauri ya Mji wa Korogwe, tunalo shamba linaitwa *Korogwe Sisal Estate;* shamba lile hati yake ilikabidhiwa *TBA.* Bahati mbaya sana lipo kwenye Mji wa *Old Korogwe,* lile shamba hakuna hata katani moja, hata shina moja la katani.

Mheshimiwa Spika, wananchi walishaingia na kuanza kuweka makazi yao mule ndani, lakini na sisi Halmashauri ya Mji wa Korogwe kwa sababu tayari tulishaingia kwenye mpango kabambe wa matumizi ya ardhi katika ile miji saba ambayo ameitaja hapa Waziri na sisi Halmashauri ya Mji wa Korogwe tumo. Sasa kwa bahati mbaya sana maeneo yale tulishayatoa na tulishakuwa tumepanga mpango kabambe wa matumizi ya ardhi lakini hati kumbe ipo *TBA.*

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tunavyotoa vile viwanja kwa maana ya kuwapatia wananchi, *TBA* wanaingilia kati kwamba maeneo yale ni yakwao. Hatukatai kwa sababu yote ni Serikali lakini kwa sababu tayari sisi Halmashauri ya Mji wa Korogwe tumeingia katika mpango kabambe wa matumizi ya ardhi na hatuna ardhi nyingine zaidi ya hilo shamba lililopo na kwa sababu si shamba, basi tuwaombe sasa wenzetu wa *TBA,* hususani Katibu Mkuu wa Uchukuzi alichukulie jambo hili kwa maana ya kurudisha ile hati angalau iweze kufutwa tuweze kukabidhiwa sisi, Halmashauri ya Mji wa Korogwe tuweze kutumia kwa ajili ya mipango kabambe ya ardhi ambayo tumeipitisha.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwa sababu hili suala linaonekana liko kwenye Wizara hizi mbili, nimwombe Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi wairudishe hiyo hati ili iweze kufutwa, hatimaye Halmashauri ya Mji wa Korogwe tuweze kupata yale maeneo kwa ajili ya matumizi.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi tulishagawa, eneo lile kwa ajili ya kumpa Mufti Mkuu wa Tanzania. Amepata wafadhili kuja kujenga Chuo Kikuu pale cha Kiislam, lakini anashindwa kuendelea kwa sababu tayari *TBA* wao ndio wenye hati. Kwa hiyo tumeshindwa kuendelea nao kwa

maana ya kumpa lile eneo. Tunaomba tu *TBA* waweze kutusaidia kupitia Katibu Mkuu wa Uchukuzi tulimalize jambo hili ili tusije tukapoteza bahati ambayo tumeipata ya kuja kujengewa Chuo Kikuu cha Kiislam katika Mji wetu ule wa Korogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana kwa kunipa nafasi, nilikuwa na haya machache ya kusema katika Wizara hii, lakini naendelea kuwapongeza sana kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wanaifanya watendaji wote wanaohusiana na Wizara hii ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Kamishna, Mheshimiwa Mary Chatanda. Mheshimiwa Joyce Sokombi, atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda kule Msekwa.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuongea machache kwenye Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Sitaongea mengi sana, nitaongelea tu mambo machache nayo ni hati zitolewe kwa wakati, viwanja vipimwe kwa wakati na fidia zilipwe kwa wakati. Kwa nini nasema kwamba fidia zilipwe kwa wakati; tumeona kabisa kwamba unakuta viwanja vinauzwa mara mbilimbili. Kiwanja kinapouzwa mara mbili, yule mwenye haki kuja kupata kiwanja au aje alipwe fidia inachukua muda mrefu sana na pia kuchukua muda mrefu bado pia suala la usumbufu linakuwa linaingilia sana.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni kwamba kunatokea hali ya utapelitapeli sana. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu hat. Mfano, watu wenye maeneo ya Ilazo *South* na Kisasa, kuna watu wamenunua viwanja na wakajenga nyumba. Na mimi pia ni mhanga wa jambo hilo; nilinunua kiwanja nimejenga nyumba toka mwaka 2016 na nimeshalipia kila kitu,

nimefuatilia hati imekuwa ni shida. Ilikuwa bado ni *CDA* kabla haijabadilishwa ile Mei, 2017 kuwa jiji. Kwa kweli hali kama hii inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, mara ya kwanza baada ya kufuatilia nilikuta *documents* zote zimepotea na hili halitokei kwangu tu, unakuta watu wengi wamejazana pale jiji malalamiko yanakuwa ni hayohayo; faili limepotea, *documents* zote zilizokuwa ndani ya faili zote zimepotea. Kwa hiyo unaona kabisa ni namna gani suala hili linakuwa ni usumbufu kwa wananchi ambao kila siku uamke asubuhi uende ofisi za jiji kwenda kufuatilia hati.

Mheshimiwa Spika, jambo hili pia limetokea kwenye Mkoa wa Mara, Musoma Mjini, hasa maeneo ya Mitaa ya Nyabisale, Songe na Kwangwa B. wananchi walishalipia lakini kitendo tu cha Serikali au wale wahusika kwenda pale kuwapimia ili wawe na umiliki wa viwanja vyao kiuhalali, imekuwa ni shida.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, hawa wananchi wanateseka sana. Unakuta mwingine amelipia, lakini amelipia na ameshapewa tayari kwamba wewe unaruhusiwa kuwa kwenye hiki kiwanja chako, lakini suala la hati kwa haya maeneo pia ni shida sana. Wananchi wanalalamika, wananchi wanalia, Mheshimiwa Waziri naomba awaangalie wananchi hawa wa Nyabisale, Kwangwa na Songe.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nitakiongelea hapa na nimeshakiongelea sana, hili suala lilikuwa kwenye Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, lakini sasa hivi suala hili limegeuzwa limeletwa kwenye Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa kweli nashindwa kuelewa. Ni kuhusiana na wananchi ambao wamejenga pembezoni na Uwanja wa Ndege wa Musoma. Wale wananchi waliwekewa *X* na walitakiwa walipwe, lakini matokeo yake hawajalipwa mpaka leo hii. Ukiwafuata tena wale watu wa Ujenzi na Uchukuzi wanakujibu kabisa kwamba, hili sio suala lao, ni suala la Ardhi, Nyumba na Maendeleo.

Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Lukuvi, wale wananchi walioko pembezoni mwa ule uwanja, wale wananchi toka 2017 wamekaa tu.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi suala hili limegeuzwa limeletwa kwenye Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kweli nashindwa kuelewa, ni kuhusiana na Wananchi ambao wamejenga pembezoni na Uwanja wa Ndege wa Musoma. Wale wananchi waliwekewa X na walitakiwa walipwe, lakini matokeo yake hawajalipwa mpaka leo hii. Ukiwafuata tena wale watu wa ujenzi na uchukuzi wanakujibu kabisa kwamba, hili sio suala lao ni suala la Ardhi, Nyumba na Maendeleo. Mheshimiwa Waziri Lukuvi ninakumba sana, naomba hili suala la wale wananchi walioko pembezoni mwa ule uwanja, wale wananchi toka 2017 wamekaa tu.

Mheshimiwa Spika, wale wazee walikuwa wanapangisha zile nyumba zao, wapangaji wote waliwakimbia. Baada ya wapangaji kuwakimbia wale wazee unategemea na asilimia kubwa, asilimia 90 ya zile nyumba, wakazi wa pale ni wastaafu, mnategemea hawa wastaafu wataishije? Maana mtu ana nyumba yake alitegemea kwamba, awe na mpangaji, ili apate chochote kitu kwa ajili ya kusomesha watoto wake; wapangaji wamekimbia wanakaa tu wao wanatazamana, hivi mnawaweka kwenye wakati gani?

Mheshimiwa Spika, mtambue kabisa mnawaweka kwenye wakati mgumu sana hawa wananchi. Na hali ambayo inaweza kusababisha hata mtu kufa kabla ya wakati wake kwa sababu, watu wengi wanapata ma-*pressure* kila kukicha wanakuwa wanawaza kuhusiana na hizi nyumba hatima yao ni ipi? Kwasababu, ilikuwa walipwe kwamba, waondoke wakapewe sehemu nyingine, matokeo yake wanapigwa danadana, watapigwa danadana hadi lini?

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri lishughulikie hili suala kwa sababu, hawa wananchi wamenituma. Sanasana kuna kipindi kilichopita Waziri wa Ujenzi alijibu hapa kwamba, ni nyumba 138, lakini zile nyumba

ni 114 na waliolipwa ni nyumba 14 eneo la Kamnyonge na nyumba tatu eneo la Nyasho, hali inayosababisha kwamba, nyumba ambazo zimeshalipwa ni nyumba 17 kwa hiyo, bado nyumba kama 100.

Mheshimiwa Waziri naomba hili suala liwe katika mikono yako, uwapigie simu wale wahusika walishughulikie hili suala kwa ukaribu zaidi kwasababu, kuna wazee walishakufa kwaajili ya hiyo; wana *pressure,* watu wengine wameshindwa kusomesha watoto wao kwa ajili ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sana kwa kweli, Wizara yako Mheshimiwa Waziri tunakuamini. Na ninaamini kwamba, unaenda kuwafanyia kazi, ili wale watu wapate haki yao hata kama mtu anakufa anajua kabisa ameacha hali gani katika nyumba yake. Maana hata kama mtu anasema kwamba, leo kama akifa wale watoto mmewaweka katika wakati mgumu sana kwasababu, kama hivyo nyumba imewekwa X, hebu niambie wale watoto yaani kutakuwa kuna shida kubwa sana kwa ajili ya kuhakikisha ile nyumba ni urithi wa baba au ile nyumba sio tena urithi wa wazazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yangu yalikuwa ni hayo. Naomba tu kwa keli, mfuatilie pia, kuna shida sana Jiji la Dodoma kama nilivyosema. Mheshimiwa Waziri naomba tafadhali sana hili suala ulizingatie kwasababu, watu wengi wanateseka sana kwa ajili ya ufuatiliaji wa kupewa hati; naomba tafadhali maana inafikia mtu unaponunua kiwanja mpaka inafikia hatua ya kujenga nyumba bado hati yako hujaipata unapigwa danadana, nakuomba tafadhali hili suala lifuatilie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joyce Sokombi. Nilishakutaja Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda na atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula wote wako Msekwa.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Niungane na wenzangu waliotangulia kuchngia kwenye hotuba hii kutoa shukrani pamoja na pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri Lukuvi, lakini pia na Naibu wake, pamoja na timu yao nzima ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa kazi makini sana ambayo wameendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, niseme tu pongezi hizi naamini zitakwenda kuwa chachu zaidi ya kukupa ari ya kufanya zaidi ya hata ambayo umeyafanya mpaka sasa ambapo Watanzania wameridhika na utendaji wenu.

Nichukue fursa hii pia kumuomba Mwenyezi Mungu atujalie, kama ambavyo tunajiombea sisi wengine wote, lakini pamoja na Mheshimiwa Lukuvi na timu yake na Naibu waweze kurudi, inshallah Mungu akipenda tukarudi wote basi na awamu ijayo pia upate fursa ya kuendelea kufanya kazi iliyotukuka kama ambavyo umeendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na ya kwangu mahususi matatu, lakini kuna moja litakuwa mchanganyiko kidogo. La kwanza ni kuhusiana na suala zima la mpango kabambe; ningetamani sana tuone halmashauri zetu zote nchini zina mipango kabambe kwa ajili ya kutekeleza maendeleo kwenye halmashauri zao. Sina hakika sana kama dhana hii inaeleweka kwenye ngazi ya halmashauri, najua kwenye Mkoa wetu wa Dodoma, Jiji la Dodoma tayari tumeshazindua mpango kabambe na ulizinduliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na maelekezo yakatoka kwamba, halmashauri nyingine zote zifuate utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, najua sio jambo jepesi, lakini kama Wizara ya Ardhi tunaweza tukakaa na kuangalia ni namna gani tunaweza kusaidia kwenye *financing plan,* iwe ya ndani ni wazi inaweza ikawa changamoto, lakini hata ya nje tuje na mkakati ambao unaweza ukasaidia *fincing plan.* Mipango kabambe ifanyike kwenye kila halmashauri, ili hata tunapokuja kufanya maendeleo yetu tuepuke vitu kama Kariakoo ya leo, tuepuke Manzese ya leo.

Mheshimiwa Spika, tuna miji inakuwa kwa kasi, miji inajengwa vizuri, lakini sasa kwa kasi hii kama hatujakuwa na mpango kabambe kweli, tutazungumzia kupima ambapo sasa napongeza kabisa kwa huu utaratibu ambao umeleta ofisi za mikoa na itakuwa karibu na gharama nafuu kwa haraka zaidi. Lakini tutaendeleza hivyo bila ya kuwa na mpangilio wa kuhakikisha tuna matumizi bora kama kwenye kuhakikisha tuna maeneo ya viwanda, maeneo ya makazi, maeneo ya biashara, taasisi za umma, n.k. Hata pale maeneo ambapo unahakikisha nyaya za umeme, mabomba ya maji, barabara zina taa za kutosha, miji inakuwa; kama hatujaiwekea mipango kabambe toka mwanzo inaweza ikawa changamoto sana.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukiongeza pia zaidi hapa, kule kwenye ngazi ya halmashauri labda ingewezekana wizarani kwako kukatoka maelekezo au waraka mahususi ambao unawataka wale wakuu wa idara ya ardhi pale halmashauri, wakishirikiana na ofisi yako ambayo sasa kutoka mkoani nina imani hatua inayofuata. Pia, tutakwenda mpaka wilayani ili kufungamanisha kazi zao na wale waweze kujua kwamba, tunatakiwa kuhakikisha tunatengeneza mipango kabambe. Bahati mbaya sana kitu ambacho nimekigundua kule kwenye Halmashauri wale ambao wanafanya kazi za idara ya ardhi sio wote wanakuwa ni wataalam hasa wa ardhi na maendeleo ya makazi ambao kimsingi tungepata watu kama ma-*planner,* Kiswahili chake sijajua wanaitwa nani, lakini wanasomea *urban and rural planning.*

Mheshimiwa Spika, ndipo watu wa mipango miji tungewapata wale ni kweli hata mnavyozungumzanao mnazungumza lugha moja. Tungepata wasanifu majengo, ma-*architect,* ambao wao wako ma-*architect* wanaofanya *urban planning,* wako wanaofanya *urban design* na *settlement design,* miji yetu inakuja kuwa miji mizuri sana. Kwa kasi hii ambayo tunaongelea KKK – Kupanga, Kupima na Kumilikisha, tutakwenda vizuri kama tutafuata ule utaratibu wa mipango kabambe, lakini wataalam wakawekwa kwenye maeneo mahususi. Na pia tukaweza

kufungamanisha hawa watumishi wa Wizara ya Ardhi, lakini pia tukaangalia na TAMISEMI ni vipi watakavyokwenda kuajiri wale wakuu wa idara ya ardhi kule halmashauri wale watu wenye fani husika.

Mheshimiwa Spika, itawasaidia sana Wizara hii ya Ardhi kwa sababu, mwisho wa siku inapotokea *chaos* kwenye uendelezaji wa miji yetu, uendelezaji wa majiji yetu, uendelezaji wa wilaya zetu, mwisho wa siku migogoro inarudi kwenye Wizara ya Ardhi na, *yes,* tunaanza kutatua migogoro kuanzia ngazi ya halmashauri, lakini mwisho lazima ije kwako wewe Mheshimiwa Waziri. Naomba sana uone ni namna gani tunaweza tukaja na mkakati wa kutoa maelekezo mahususi kwa ajili ya kufanikisha hilo, hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ndio hii nimezungumzia habari ya wataalam wa fani zinazohusu mipango miji, wako wengi sana pale chuo cha ardhi, labda na vyuo vya ardhi sehemu nyingine, lakini unakuja kukuta huku ambapo tunawaajiri wanakuwa labda ni Wanasheria, zipo na fani nyingine tofauti. Sijaelewa msingi wake, lakini naamini linahitaji kufanyiwa fikra zaidi na TAMISEMI na Wizara ya Ardhi tukikaa pamoja tunaweza tukalijenga hili vizuri.

Mheshimiwa Spika,jambo lingine, nilitaka kuongelea kuhusiana, nimeona migogoro mingi sana imetatuliwa tangu umeingia. Na huko mwanzo ulipokuja uliitisha orodha na orodha zikaletwa, migogoro mingi imeshughulikiwa. Ipo migogoro ambayo kimsingi haiko moja kwa moja kwenye Wizara yako, lakini na wewe pia kwa namna moja au nyingine unahusika kwa sababu, inahusiana na ardhi.

Mheshimiwa Spika, pale kwetu Kondoa iko migogoro ya viwanja kabla ya halmashauri hii ya sasa, halmashauri ya mji kuundwa, ilikuwa ni ya viwanja ambavyo watu walilipa hawakuoneshwa vile viwanja mpaka baadaye halmashauri imegawanywa kumekuwa na Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Mji, lakini mpaka leo iliundwa tume ya kuchunguza na kufanya marekebisho kadhaa na iliundwa na Mkuu wa Mkoa na imechukua muda. Najua sasahivi

tunazungumzia kabla ya mwaka 2015 ni zaidi ya miaka mitano kwa hiyo, sijajua wapi tumekwama hatujafikia hitimisho, lakini ningeomba *intervation* yako kwa sababu, idara ya ardhi imehusika moja kwa moja na watu wa ardhi wamekuwepo kwenye hiyo tume; kama unaweza kulifuatilia ili uweze kuchukua hatua tufikie mwisho kwenye hili.

Mheshimiwa Spika, laini hapohapo kwenye mgogoro upo mwingine ambao pia kwa upande wako haujahusika moja kwa moja, lakini idara ya ardhi ipo. Ni mgogoro baina ya eneo la Magereza la King'ang'a na Wananchi wa Kijiji cha Yoli kwenye Kata ya Kingale ambapo kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu. Na kwenyewe tume imeundwa na mkuu wa mkoa, naamini inakwenda vizuri, lakini hatujafika mahali tutafika mwisho na tunafikia hatua Wananchi wanapoteza subira. Nina imani kwa mtindo huu tunao kwenda nao ukifanya *intervention* pale Mheshimiwa Waziri tunamaliza mgogoro huu wa King'ang'a.

Mheshimiwa Spika, vivyohivyo kwenye lile sakata la vijiji ambavyo vimepakana na hifadhi. Kule kwetu kuna Kata y Seria kwenye Kijiji cha Mongoroma na baadhi ya vijiji vingine mpaka huku Chemba, mpaka huku upande wa Kondoa Wilaya vimezunguka Pori lile la Swagaswaga. Najua kazi kubwa imefanyika na wewe mwenyewe ndiye uliyekuwa kiongozi wa ile tume iliyoshirikisha Wizara nane, sasa mpaka sasa hivi tunaona bado ni kimya. Hatuna uhakika tunajua hali imetulia, lakini hatuna uhakika hitimisho ni lini, tungeomba tufike…

**SPIKA:** Ahsante sana, hitimisha!

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Edwin Sannda. Sasa bado tuko Msekwa, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula na atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula Msekwa hukohuko, *no,* Mheshimiwa Kitandula yuko humu ndani. Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii. Walao niseme machache kwa ajili ya mustakabali mzima wa mwenendo wa Wizara yetu ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati na pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri Lukuvi, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, lakini nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuunda tume ya Mawaziri kutoka Wizara nane ambayo ninaamini tume hii imezaa matunda na imeleta matumaini makubwa sana kwa Watanzania. Imefufua ari za kiuchumi na kuondoa mawazo ya umasikini kwa Watanzania, sambamba na zoezi zima la urasimishaji wa makazi kwenye miji ambayo tayari ilishafanya zoezi la upimaji miaka mingi sana.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu kwenye miji mingi maeneo mengi ya ardhi yameshafanyiwa utambuzi na upimaji kwa muda mrefu, mengine yamefanyiwa michoro kwa muda mrefu ambayo imekaa kwa muda mwingi sana karibu miaka 12 mpaka 20. Sasa ukizungumzia changamoto hizi, nilitaka leo nijikite kwenye suala moja tu ambalo ninadhani limekuwa na matumaini makubwa sana kwetu sisi wakazi wa Jiji la Mwanza pamoja na maeneo mengine nchi nzima Tanzania.

Mheshimiwa Spika, zoezi la urasimishaji wa makazi kama nilivyosema, limerejesha matumaini ya Watanzania wengi. Na ninafikiri waliofanya tafiti kwamba, kwa nini mikoa ya kanda ya ziwa mingi inaonekana kwenye takwimu ni mikoa masikini?

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kutokana na kutokumiliki ardhi zao kwa wingi na kihalali. Na matokeo halisi ya huu urasimishaji wa makazi unaweza kuona kwa mfano, ukizungumza tu viwanja vilivyotambuliwa kwa mara ya kwanza toka Jiji la Mwanza limeundwa ni zaidi ya viwanja 52,773 watu wote hawa walikuwa wanakaa kwenye makazi wasiyokuwa na uhakika nayo, lakini viwanja ambavyo

vimepimwa baada ya utambuzi ni 43,795. Hati ambazo zimetolewa kwenye idadi ya viwanja vyote hivyo ni hati 14,174.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu iko hapa. Unaweza kuona utambuzi wa viwanja, upimaji wa viwanja wenyewe, lakini hauendani sambamba na hati zilizotolewa. Nimewahi kuhudhuria kwenye Kamati ya Maliasili nikasema na Mheshimiwa Waziri akakubaliana na mimi, kazi hii kubwa iliyofanywa bado tunayo changamoto kubwa kwenye Wananchi wenyewe kuwa tayari kumiliki hati. Sasa ninemuomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie, inawezekana wananchi wetu kwa namna moja au nyingine hawajatambua umuhimu wa kuwa na hati.

Mheshimiwa Spika, akishaona eneo lake limepimwa akaridhika kwamba, amepata kigingi anaona amemaliza, lakini kumbe ziko faida nyingi za kumiliki hati ambazo Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yako umezitaja vizuri sana. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, tuliangalie hili kwa umakini sana. Ukiwa na uwezo wa kupima viwanja 43,000 halafu hati ambazo sio kwamba, hazipo, zipo zimeandaliwa, lakini inawezekana watu hawajui aidha kwasababu ya changamoto ya fedha zimekuwa nyingi kwenye mzunguko mzima wa kuhakikisha kwamba, anapima na baada ya kupima kwasababu anagharamikia yeye, mwisho wa siku anatakiwa alipe malipo mengine ili kwenda kuchukua hati.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa inawezekana kuna changamoto kubwa ambayo bado hatujaijua vizuri, lakini natambua Mheshimiwa Waziri analifahamu hili. Pamoja na jitihada kubwa zilizofanywa na Watendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza kiukweli Mheshimiwa Waziri kwa dhamira kabisa ya moyo wangu wa dhati niwapongeze sana Watendaji wa Ardhi wa Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Spika, wewe utakuwa ni shahidi, Mheshimiwa Waziri ulitoa makisio au malengo ya kupima viwanja 24,000 kwa Jiji la Mwanza, lakini wamevuka malengo zaidi ya asilimia 120. Hii ni kazi kubwa na sio hivyo tu,

wameenda mbali zaidi tunalazimika kupeleka ofisi kwenye kata. Amekuja Mheshimiwa Waziri akahudhuria kwenye Kata ya Mwananchi ambako Ofisi ya Halmasahuri ya Jiji Kitengo cha Ardhi kilihamia kule kuhakikisha wanapima, wanarasimisha, lakini wanatoa hati kwa wananchi ambao walikuwepo pale. Mheshimiwa Waziri halikadhalika umetembelea Kata ya Buhongwa kule Buguku ukashuhudia namna ambavyo ofisi zinahama na kushughulika vizuri. Na leo tunapozungumza hapa Ofisi ya Ardhi iko kule Kata ya Rwanima, eneo moja linaitwa Semba.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ningetamani sana kuona Wananchi wetu wengi ambao wamefanya kazi hii kubwa, na Mheshimiwa Waziri nataka nikuhakikishie kati ya kata 18 kata 13 zote zilikuwa kwa sasa zimefanyiwa urasimishaji wa makazi, zaidi ya mitaa 102. Hii ni hatua kubwa sana ya kujivunia. Na toka nimeinga mpaka sasa Mheshimiwa Waziri Lukuvi pamoja na Naibu wako mama yangu Mheshimiwa Angelina Mabula bado huwa napata tabu hapa; Mheshimiwa Waziri inawezekana na wewe una kadamu ka kisukuma kidogo kwasababu, hii *speed* sio ya kawaida hii.

Mheshimiwa Spika, hata *speed* yake na yeye ni kutokana na kadamu ka usukuma haka. Mtakuwa mnakubaliana na mimi kwamba, kasi mnayoendanayo ni kasi halisi ya Awamu ya Tano na ni kasi ambayo inawasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwenye mfumo mzima wa utoaji hati, gharama zimeonekana kuwa kubwa, inawezekana sana mkatusaidia kujua. Ziko gharama ambazo mwananchi akishamiliki ardhi yake anazilipa katika maendelezo ya ulipaji wa kodi za kawaida pale anapomiliki ardhi. Sasa inawezekana tukitumia kodi zile kama kodi za Serikali na tukapunguza gharama kwenye umilikishaji wa hati, inaweza ikasaidia wananchi wengi sana wakamili hati.

Mheshimiwa Spika, migogoro ipo, nami nashukuru sana kwa mara ya kwanza Jiji la Mwanza leo tunamaliza

miaka mitano, migogoro ya ardhi kutoka asilimia 100; Mheshimiwa Lukuvi unaweza kuwa umebakisha asilimia tatu peke yake; na kati ya hizo asilimia tatu ni migogoro miwili tu; mmoja ulioko kule Kata ya Lwanima na mwingine uko pale pale Kata ya Lwanima kule kwenye Mtaa wa Semba pamoja na Mtaa wa Mwalukila na Bugayamba ambako kuna eneo kubwa sana la eneo ambalo lilitengwa zamani kwa ajili ya makaburi. Mheshimiwa Naibu Waziri amefika pale na kuna barua imeshaandikwa na wataalam kutoka Halmashauri kuja kwenye Wizara.

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana Mheshimiwa Lukuvi, Mwanza hii ukiondoa kazi hiyo na hii uliyoruhusu sasa ya leseni za makazi ikaanza, tutakuwa tumemaliza changamoto za ardhi na zitakazobaki zitakuwa za kawaida sana. Nami naendelea kukuombea sana na mara hii ukija tutaandaa kale kambwa kadogo kadogo kazuri kwa sababu tunajua kule kwako unakotoka mtani, hivi ndivyo vyakula vizuri, katakufaa sana. Nakushukuru sana kwa kazi nzuri, hongera sana, endelea kushikilia hapo pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wa Tanzania watafaidika kwa kumiliki ardhi yao wenyewe na hasa pale wanapokuwa wameshika hati mkononi, wanaweza kujipatia kipato na wakaendeleza maisha yao na familia zao na tukasonga mbele zaidi na Taifa likaendelea kuimarika zaidi. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, sasa nimeshamtaja Mheshimiwa Dunstan Kitandula, atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ajiandae.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye kwa upendo wake

amezidi kutulinda na kutustahilisha katikati ya Watanzania. Nitumie fursa hii vile vile kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wananchi wa Mkinga, kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa watu wa Mkinga hususan kwenye Sekta hii ya Ardhi. Tumekuwa na tatizo la muda mrefu la ardhi na ninyi mnajua kwamba watu wa Mkoa wa Tanga ni wahanga wa ardhi yao kubwa kutwaliwa kwa ajili ya mashamba ya mkonge na kwa muda mrefu mashamba haya yamekuwa yametelekezwa. Tulileta kilio hiki, Wizara ikashughulikia, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alikuja mwenyewe na Naibu wake pia alikuja kutukabidhi ekari 15,000 za mashamba matatu yaliyofutiwa hati kule Mkinga. Wananchi wa Kijiji cha Duga, Kilulu Duga, Zingibari, Mwaboza, Mwakikoya, Mahandakini, Kanyezi, Sigaya, Mayomboni, Ndumbani na Moa, wanashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile yapo baadhi ya maeneo tulikuwa tumeleta maombi yafanyiwe kazi na Mheshimiwa Waziri akatoa maagizo lakini vile vile alipokuja Waziri Mkuu, tulimweleza tatizo kwenye Kata ya Maramba, shamba la Mwele ambalo limetelekezwa kwa takriban zaidi ya miaka 25. Tulimweleza kwamba wananchi wale wa Maramba hawana ardhi. Maramba ina takribani watu 13,000 na kaya karibu 2,700. Wananchi wa Maramba A, kwa ardhi waliyonayo kila mmoja anamiliki asilimia 0.39 ya hekta. Maramba B, wanamiliki asilimia 0.66 ya hekta. Kwa hiyo, ukiangalia kwa haraka wananchi hawa wana tatizo kubwa sana la ardhi lakini katikati yao kuna shamba limetelekezwa kwa zaidi ya miaka 25, hekta 990.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliposikia kilio hiki akatoa maagizo kwamba Serikali imeshaamua kwamba popote penye ardhi iliyotelekezwa hata kama ni ya Serikali, Serikali itafanya jitihada za kufanya mapitio ya ardhi hiyo ili ardhi iweze kugawanywa kwa wananchi. Sisi kama Halmashauri tumeshafanya kazi ya kufanya mapitio. Tumepeleka mapendekezo mkoani, Mkoa umeshaleta mapendekezo Wizarani. Ninakuomba agizo lile la

Mheshimiwa Waziri Mkuu la watu wa Maramba kupatiwa ardhi liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuja, vile vile alijua tatizo la shamba la Kwa Mtili, na tulikuwa na tatizo pale la kiasi halisi cha ardhi tulichokiombea ifutiwe. Ardhi iliyokuwa imeombwa ilikuwa na makosa. Shamba lenye ukubwa wa hekta 1,200 na hekari zilizokuwa zimeombewa zilikuwa ni 58, akaagiza kazi ya uhakiki ifanyike.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba kazi ile imefanyika. Nakushukuru sana kwa msukumo wake, wataalam kutoka Kanda, Mkoa walishirikiana na wataalam wetu, uhakiki umefanyika na imebainika kwamba hati ile namba 1,450 na vile vile hati namba 4,722 ambazo zinatuletea hekta 1,173 zimetelekezwa, hazijaendelezwa. Tunakuomba sana mchakato wa ardhi hii, hati hizi zifutwe ili ardhi ile irudi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri vile vile kwa kutuletea ofisi pale pale Tanga. Ameturahisishia, sasa ile kadhia tuliyokuwa tunaipata watu wa Tanga kufunga safari mpaka Moshi sasa imekwisha, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru vile vile kwa Serikali kuanzisha mchakato wa mapitio ya maeneo yaliyokuwa na migogoro kwenye maeneo ya mapori yetu tengefu na mbuga za wanyama; nasi wa Mkinga ni miongoni mwa maeneo hayo kwenye Kata ile ya Mwakijembe, Kijiji cha Mkota, Kitongoji cha Kimuni. Tunaomba ufumbuzi wa jambo lile upatikane kwa haraka ili wananchi wetu waweze kupata ahueni ya maisha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, hili namatani niliseme kwa sauti kubwa lakini kwa *sensitivity* ya usalama na uhusiano na wenzetu wa nchi jirani, naomba niliseme kwa sauti ndogo. Mkinga tuna tatizo kubwa. Mpaka wa Mkinga ni *porous;* nchi kavu na baharini. Naomba tushughulikie tatizo la mpaka hasa kule baharini. Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuja alijionea. Tulimkaribisha kwenye nyumba upande mmoja tuko

Tanzania, upande mmoja ni Kenya. Vyombo vya ulinzi vya Kenya huwa vinakuja kufanya doria kwenye ardhi yetu.

Mheshimiwa Spika, hapa nataka nimshukuru sana na nimpongeze Mkuu wetu wa Wilaya, kama siyo busara yake, nchi hii tungekuwa tumeingia kwenye migogoro ya kivita na wenzetu, kwa sababu vyombo vyao vya ulinzi na usalama vinaingia mpaka kwenye makazi ya wananchi wetu. Mheshimiwa Waziri, naomba mtoe kipaumbele kwenye eneo hili. Nawasihi sana. Tusije tukaingia kwenye matatizo ambayo tungeweza kuyaepuka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dunstan Kitandula kwa hotuba yako nzuri. Sasa nimwite Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo atafuatia. Mheshimiwa Bura kutokea Msekwa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii. Nachukua nafasi ya kukupongeza wewe kwa uongozi wako mzuri wa Bunge letu Tukufu na amekuwa Spika wa mfano sio kwa Tanzania tu, lakini hata kwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Lukuvi pamoja na Mheshimiwa Angelina Mabula na Katibu Mkuu dada Mary Makondo kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. Mheshimiwa Lukuvi tangu aanze kuteuliwa, tangu aanze kuwa Waziri amepitia Wizara mbalimbali na hajawahi kuiangusha Serikali kwa utendaji wake.

Kwa hiyo, nampongeza sana, kwani tangu aingie Wizara ya Ardhi, malalamiko yamepungua. Njoo kesho, njoo keshokutwa, imepungua na wananchi wanapata haki zao, kama siyo kwa wakati lakini malalamiko yamepungua mno. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Lukuvi, Katibu Mkuu, na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Angelina Mabula. Mmeonesha uwezo mkubwa sana na Mungu awajalie mrudi

tena. Kama mtarudi, basi mpangwe katika Wizara hii, mwendelee kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, alipoingia madarakani mwaka 2015, alitangaza ardhi ya Dodoma kurudi kwa wananchi. Kabla ya ardhi ya Dodoma kurudi kwa wananchi, wananchi wa Dodoma walipata shida sana. *CDA* iliweza kupima viwanja siyo zaidi ya 300 kwa mwaka lakini sasa hivi viwanja vinapimwa zaidi ya 50,000 na vinauzwa kama anayeuza kitu chochote dukani.

Mheshimiwa Spika, ukienda Jiji pale wakati wowote unanunua kiwanja unachokitaka kwa *size* ya kiwanja unachotaka na kwa wakati unaotaka wewe mwenyewe. Kwa hiyo, haya yote ni kwa ajili ya usimamizi mzuri wa Mheshimiwa Lukuvi na Wizara yake akishirikiana na Jiji letu la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nimesikia Mheshimiwa mmoja amesema kwamba kufuatilia hati inachukua muda mrefu. Nadhani inawezekana anakwenda maeneo yasiyohusika, lakini nimhakikishie tu kwamba Jiji la Dodoma kwa sasa kwa utoaji wa hati ni wa haraka sana. Kwa upimaji wa viwanja ni wa haraka sana, unakwenda wala hupangi hata foleni. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba Dodoma tuko vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, Mheshimiwa Lukuvi nikupongeze kwamba Kamonga ambaye alikuwa anawahudumia Watanzania umempandisha cheo na kuwa Kamishna Msaidizi na najua ataendeleza utendaji aliokuwa nao katika Jiji hili kule ulikompeleka.

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Serikali kwa mpango kabambe wa Jiji la Dodoma. Ni mpango ambao utaifanya Dodoma kuwa Jiji zuri lililopangika na la kipekee sana. Naiomba sasa Serikali, ikiwezekana viunga vya Dodoma kwa mfano, Wilaya ya Bahi ni karibu sana na Dodoma Jiji na wananchi wawekezaji watakwenda Bahi kuwekeza. Wilaya ya Kongwa, napenda pia ihusike kwenye mpango kabambe. Najua wawekezaji na wananchi watapenda kuendeleza

Wilaya ya Kongwa. Kwa hiyo, ikijumuishwa kwenye mpango kabambe, Dodoma itakuwa mkoa wa kupendeza na mkoa wa mfano kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chamwino iko karibu sana na mpango kabambe wa Jiji la Dodoma. Naomba mpango kabambe uhusishe pia Wilaya ya Chamwino. Kwa sasa mpango kabambe umehusisha Kata tatu za Wilaya ya Chamwino, lakini Wilaya ya Chamwino iko jirani sana na Jiji la Dodoma. Kwa hiyo, naomba kwamba mpango huo kabambe ukahusishe viunga vya Dodoma kama Wilaya ya Chamwino, Kongwa, Bahi na hata Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Spika, nina jambo moja tu ambalo pia napenda nilizungumze kwamba katika hotuba ya Waziri; na ninampongeza sana kwamba sasa hivi kuna shughuli za urasimishaji makazi na umetusaidia sana kuboresha miji yetu, kwamba kuna kupima hasa ukiwashirikisha wananchi na pia kuweka miundombinu ya huduma za jamii. Kwa hiyo, imesaidia sana kurahisisha upimaji na inawezekana siyo kwa Wilaya zote au Halmashauri zote. Kama mpango huo haujahusisha Halmashauri zote, huu mpango umesaidia sana hasa Jiji la Dodoma. Kwa hiyo, naomba mpango wa urasimishaji uende maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, nina jambo ambalo nimeona Mheshimiwa Waziri ameliongelea. Suala la upimaji maeneo, mipaka na hasa mipaka inayohusiana na hifadhi za Taifa. Mheshimiwa Rais aliunda Tume iliyoshughulika na kuangalia migogoro katika mipaka ya vijiji na hifadhi za Taifa. Amesema katika hotuba yake aya namba 51 kwamba Baraza la Mawaziri liliketi Septemba mwaka 2019 na likafanya maamuzi, likaridhia kwamba vijiji 920 waachiwe maeneo kwa ajili ya kilimo, hifadhi na kwa ajili ya matumizi mengine. Vijiji hivi ni vile vijiji ambavyo wanafanya shughuli katika maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, sisi hapa Dodoma Wilaya ya Kondoa na Wilaya ya chemba, wananchi wanalima, wala hawajajenga kwenye hifadhi. Katika kulima kule kuna

mgogoro mkubwa sana kati ya wananchi wale wa vijiji 12 na hifadhi. Tume hii ilipoundwa tulipata matumaini kwamba wananchi sasa watajua hatima yao; wanaachiwa zile kilometa 50 au hawaachiwi zile kilometa. Kwa hiyo, mgogoro umeendelea, wananchi wanagombana na maaskari na hata kufikia hatua ya kuuana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sasa, vijiji 920 vitajwe kwa majina, maana ukiweka kwenye *blanket* kwamba ni vijiji 920 wameruhusiwa wananchi watumie maeneo ya hifadhi, bila kujua ni vijiji gani wananchi hawawezi kujua na bado tunaulizwa na hivi tunaenda kwenye uchaguzi itatuletea shida tutakosa majibu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Wizara ikiridhia, kwa sababu Tume ile ilisharidhia na Baraza la Mawaziri mwezi Septemba, 2019 iliridhia. Sasa basi waone namna ya kutaja vile vijiji kwenye gazeti la Serikali nasi Wawakilishi wao tukawaambie kwamba vijiji vyenu vimekubalika mvitumie kwa kilimo au kwa ufugaji au kwa huduma zozote ambazo ni za kijamii. Itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, ninajua Mheshimiwa Lukuvi ana uwezo na bado anaweza akafanya jambo hili hata kabla Bunge halijavunjwa. Kwa hiyo, naomba sana wananchi wetu wajue hatma yao. Badala ya kuendelea kugombana na wahifadhi, wanapigana na wahifadhi, wanachukua mifugo yao wanabaki masikini, suala hili sasa lifikie mwisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana kwa kunipa muda wa kuchangia. Mungu akubariki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Felister Aloyce Bura. Sasa naomba waliobaki tujitahidi tu-*focus* moja kwa moja twende kwa dakika tano tano na tumebaki Wabunge wanne tu ili sasa nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Tunaanza na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE.DKT.JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo kwenye hii bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Naomba ku-*declare interest,* mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Wizara hii, kwa hiyo sitakuwa na mengi sana ya kusema, sana sana ni kuboreshaboresha.

Mheshimiwa Spika, nianze sasa kwa kumpongeza Waziri Mheshimiwa Lukuvi kwa hotuba yake nzuri sana. Pia nampongeza Naibu wake, Katibu Mkuu, watendaji wote wa Wizara na Wakuu wa Taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hiyo kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Mheshimiwa Lukuvi nimemfahamu muda mrefu, utendaji wakekwa kweli naukubali; kule kwetu Arumeru amekuja akijamara kwa mara kutatua matatizo ya migogoro ya ardhi na kila akifika amekuwa anatatua kwelikweli, nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, tukubaliane kwamba umakini wa Wizara hii unatokana pia na umakini wa Mkuu wa Nchi yetu, Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambaye kusema yale ya kweli amefanya kazi nzuri sana. Nimesha-*declare* kwamba ni mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ambayo inahusika na Wizara hii, maoni na ushauri ambavyo ni sehemu ya hotuba hii tulihusika na imetaja kazi nzuri aliyofanya Rais, sina haja ya kurudia lakini nampongeza sana Rais kwa kazi nzuri ambayo anawafanyia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa hekima na utu wa hali ya juu kwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambao ulipelekea kuundwa jopo la Mawaziri nane wa kushughulikia migogoro ambayo ilikuwa inaonekana inatesa Watanzania kati ya vijiji na maeneo ambayo yamehifadhiwa. Naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu hili kwamba kule Meru, Kitongoji cha Momela nacho kilikuwa ni*victim* na Mheshimiwa Waziri alihusika katika kuja kuweka mpaka ule ambapo sasa umekaa sawa. Mpaka ule umepita kandokando ya nyumba za watu, sehemu nyingine mtu anatoka mlangoni kwake mita

moja ameshakanyaga hifadhi. Kwa hiyo kwa kweli imekuwa ni tatizo kubwa sana, wale wananchi wanaendelea kuteseka.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba vijiji 920 vimekubalika kwamba vitarudishiwa ardhi yake, lakini bahati mbaya hatujajua kama Momela nao wapo katika kundi hilo. Nimwombe Waziri kwamba kwa kuwa alikuja kunyoosha ule mpaka, atenge tena nafasi aje akaurekebishe uwe kidogo wa kibinadamu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wananchi kule wanateseka, mifugo yao inatekwa na inauawa, wanabaki kuwa maskini, ifike mahali sasa tuwasaidie.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kwamba Watanzania wanaongezeka, mwaka huu tupo milioni 58 lakini pia wanyama; ng'ombe wameongezeka milioni 32.2, mbuzi milioni 20 na kondoo milioni 5.5, bado kuna maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya uhifadhi lakini eneo la Tanzania bado ni *squarekilometer*zilezile 947 *point something;* inafikia mahali migogoro itakuwa mikubwa kama hazitachukuliwa hatua madhubuti za kuweka utaratibu mzuri wa ardhi tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu chini ya Mheshimiwa Lukuvi inafanya kazi nzuri sana. Ajenda aliyonayo ya kuhakikisha kwamba kila kipande cha ardhi kinapimwa, kinapangiwa matumizina kitamilikishwa naomba ajenda hiyo iendelee vizuri. Mheshimiwa Lukuvi tunamwombea Mungu apambane ahakikishe kwamba nchi yetu inapimwana matumizi ya ardhi yanawekwa sawasawa, huo ndio utakuwa mwarobaini wa kuondoa migogoro kati ya vijiji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Pallangyo.

**MHE.DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo. Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Willy Qambalo na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer atatufungia mjadala, Mheshimiwa Taska huko Msekwa.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya kwa kipindi chote kwa ajili ya Watanzania, kurudisha heshima ofisi za Serikali na namwomba Mwenyezi Mungu azidi kumlinda. Pia Nakupongeza wewe na Naibu wako Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kutulea hapa Bungeni na kutulinda kipindi chote cha miaka mitano tuliyokuwa hapa Bungeni. Nawashukuru sana wafanyakazi wote wa Bunge na watendaji wote kwa jinsi ambavyo wameshirikiana na sisi kwa kipindi chote tulichokuwepo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Lukuvi na Naibu wake Mheshimiwa Angelina Mabula kwa kazi nzuri sana walizozifanya kwenye Wizara hii ya Ardhi. Ni Wizara ambayo ilikuwa na matatizo makubwa sana kipindi cha nyuma; ilikuwa na watendaji wengi ambao walikuwa siyo waaminifu, walikuwa wanaweza kutoa hati za viwanja mara mbilimbili, lakini tangu kuingia Mheshimiwa Lukuvi, Wizara hii kwa kweli imekaa vizuri na wafanyakazi niseme tu kwa kifupi wanafanya kazi zao vizuri. Pia watendaji wa Wizara hii kwa kweli wameweka mipangilio mizuri na wanafanya kazi vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Wizara hii kwa kuanzisha Ofisi za Makamishna Mikoani kote. Ofisi hizi zitasaidia sana maendeleo ya ardhi kwenye mikoa yote nchini Tanzania. Nitoe mfano kwenye Mkoa wetu wa Katavi, wananchi wa Mkoa wa Katavi walikuwa wanawajibika kutembea kilometa takribani 360 kwenda kwenye Mkoa mwingine wa Tabora kufuata nyaraka za viwanja kama hati, kupitisha ramani kama wanataka kujenga na gharama za kufuatilia hizo hati ilikuwa ni kubwa na ilikuwa ni usumbufu mkubwa na hii ililetea wananchi wengi wa Mkoa wa Katavi kukosa hati za viwanja vyao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishukuru sana kwa kuanzisha hicho kitengo cha Wizara kwenye mikoa yote na hiki kitasukuma sana maendeleo ya wananchi wa Mkoa wa Katavi, lakini siyo Mkoa wa Katavi tu ni pamoja na mikoa mingine, maendeleo ya upimaji wa ardhi yataharakishwa na wananchi wataweza kufaidika na ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, Mkoa wangu wa Katavi una upungufu ufuatao; Mkoa wa Katavi una upungufu wa wafanyakazi wa kitengo cha ardhi. Mkoa wa Katavi una Halmashauri tano, lakini katika Halmashauri tano ni Halmashauri moja tu yenye wafanyakazi wa kada zote kwenye Kitengo cha Ardhi. Kwa mfano, Halmashauri ya Mpimbwe na Halmashauri ya Mlele ina wafanyakazi wawiliwawili tu kwenye Idara ya Ardhi. Ukosefu wa wafanyakazi kwenye idara hiyounasababisha kurudisha maendeleo ya upimaji wa ardhi kwenye Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, ukiwa unafahamu fika kwamba Wizara ya Ardhi kwenye zile kada zinashirikiana lazima kuwe na mpimaji na mthamini ili ardhi iweze kupimwa. Sasa ukosefu wa wafanyakazi wa kada hizi mbalimbali unasababisha maendeleo ya ardhi kwenye Mkoa wa Katavi yawe nyuma. Ningeomba Wizara ya Ardhi na kwa sababu Waziri yupo hapa aweze kutupatia wafanyakazi wa kada mbalimbali kwenye Halmashauri zote za Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ningependa kukiongelea kipengele cha 19 na 20 cha Sheria za Ardhi nchini. Kwenye *The Land Act,* 1999 kipengele cha 19 kinatoa fursa kwa mwekezaji kuwekeza nchini na kumilikishwa ardhi, lakini kipengele cha 20 cha *The Land Act* ya nchini Tanzania kinasema kwamba mtu ambaye siyo Mtanzania hawezi kumiliki ardhi nchini Tanzania. Sasa kwa nini nimeoanisha hivi vipengele viwili.

Mheshimiwa Spika, nimevioanisha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Taska, nakushukuru sana.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, kengele ya kwanza.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini ungenipa dakika moja nilitaka kuonesha tofauti ya vipengele hivyo…

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Willy Qambalo atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer ajiandae.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ya jioni hii ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ambayo tunaongelea masuala mazima ya ardhi. Ardhi ni rasilimali muhimu sana ambayo haiongezeki bali inazidi kupungua kila kukicha. Kwa hiyo, tunapaswa kwa kweli kuitunza ili itutunzena sisi.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kipindi hiki amefika Karatu mara mbili; mara ya kwanza alikuja kukabidhi hati ya kimila kwa jamii ya Kihadzabe ambayo ardhi yao ipo kwenye hatari ya kutoweka. Alifanya kazi nzuri sana, lakini pili alikuja kwa ajili ya kutatua migogoro ambayo iliwasilishwa ofisini kwake kwenye kile kipindi chake maarufu cha Funguka kwa Waziri wa Ardhi. Tulikaa mazingira bora wananchi zaidi ya 100 walipeleka kero zao kwake, zingine zimepata suluhisho, lakini bado zingine zipo palepale.

Mheshimiwa Spika, tunayo migogoro ya ardhi; mimi ningetamani sana Wizara hii siku moja ihame kutoka kwenye kutatua matatizo ya migogoro ya ardhi iwe Wizara ambayo inaendeleza masuala ya ardhi. Namna pekee ya kufika huko ni kile ambacho hata Kamati imesema, ardhi ya nchi hii ipimwe, ipangwe na imilikishwe kwa walio nayo. Bila kufanya hivyo migogoro hii itaendelea kuwepo na Mawaziri kazi yao

itakuwa ni kukimbia kutoka eneo moja kwenda eneo lingine kwenda kutatua migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro hii inasababishwa kutokana na mambo mbalimbali; migogoro mingine inasababishwa na kutokuwa na hati, watu wanavamia ardhi za watu wengine, lakini migogoro mingine inasabishwa na watendaji na viongozi ambao wapo kwenye eneo hilo. Wapo watendaji kwenye eneo hili la ardhi ambao pia hawatendi haki, wao kazi yao imekuwa ni kuzalisha na kusababisha migogoro.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atakumbuka alivyokuwa uwanjani pale Karatu alileteWa mgogoro wa kiwanja cha mzee yule ambaye hata Halmashauri tumekaa, Kamati ya Fedha tumetembelea eneo lile, Baraza limefanya maamuzi kwamba ardhi ile ni ya Mzee Kware wa Kjiji cha Basobish, lakini mpaka leo mzee yule na uzee wake ardhi yake ameendelea kupokonywa.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda kwa Mheshimiwa Waziri tukapeleka na zile nyaraka, akihitaji tutamletea nakala zile, ile ardhi Halmashauri ya Wilaya Karatu inatambua ni ya Mzee Kware, lakini bado yule aliyemilikishwa na watendaji wa ofisi yake ambaye sasa ana nyaraka zote ameendelea kudai ni ya kwake. Tukiweza kusaidia watu wa namna hiyo ambao wanaonewa, nadhani pia hata baraka za Mwenyezi Mungu zitakuja kwetu.

Mheshimiwa Spika, tunayo mashamba ya mikataba; Karatu tuna mashamba zaidi ya 40, wawekezaji wengine wameshindwa kuendeleza mashamba haya. Zaidi ya asilimia 50 au 60 ya mashamba hayo bado yamekuwa mapori, wanyama wa kali kama simba, mbogo na tembo wamehamia huko, wenye mashamba bado hawajaweza kuyaendeleza. Alipotoka Mang'ola alikutana na wananchi wa Mang'ola Juu wakamlalamikia juu ya mashamba hayo ambayo yametelekezwa na wale ambao wanamiliki na Halmashauri tumejaribu kufuatilia mashamba hayo, tunalo tatizo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwenye mkutano ule alikiri kwamba anaondoka Karatu akijua hana watendaji wenye weledi. Bado tatizo lile limeendelea kuwepo, wakitumwa kwenda kufanya tathmini kwenye mashamba yale, shamba unaona pori ni kutoka hapa mpaka Ihumwa lakini unaambiwa limeendelezwa kwa asilimia 80. Sasa unajiuliza limeendelezwaje wakati shamba ni pori, kwa hiyo, hawaleti tathmini ambayo ni sahihi matokeo yake wale watu wameendelea kushikilia yale mashamba.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ikiwezekana tupate watumishi ambao kwa kweli Mheshimiwa Waziri anawaamini waje watufanyie tathmini ya mashamba yale ili yule ambaye kwa kweli ameyatelekeza, ameshindwa kuyaendeleza basi iwe ni zamu ya kuyaondoa.

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo la wataalam kwenye kitengo hiki, wataalam hawatoshi, lakini vitendea kazi pia havitoshi. Hivi vijiji ambavyo vinakwenda kuwa miji midogo vinakuwa kwa kasi sana; tunashindwa kuvipanga kwa sababu watendaji hawatoshi lakini pia rasilimali fedha hakuna na vifaa vile vya kufanyia kazi vipo vichache sana. Miaka ya nyuma ile asilimia 30 ya kodi ya ardhi inaporudi tunakuwa na nguvu ya kufanya kazi hiyo, lakini sasa Halmashauri hazina hela za kutosha ndiyo maana miji hiyo haipimwi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Willy Qambalo. Sasa Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer atakuwa wa mwisho.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsantesanakwa kunipa nafasi hii jioni hii ili nipate kutoa mchango wangu. Awali ya yote nimshukuru Mungu na niwashukuru pia wapiga kura wangu wote wa Zanzibar, Pemba na Unguja, niko vizuri na Mungu ananilinda, nipo imara na nipo kwenye mfungo mtukufu wa Ramadhani na wanisubiri mwezi wa sita tutakuwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wametoa mchango mkubwa sana kwenye Wizara hii, wametatua migogoro mingi sana. Tunaona hata hapa walipofika basi ni kudra za Mwenyezi Mungu na Mungu awafanyie wepesi kila penye uzito.

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala, hizi mvua ambazo zinaendelea hasa Jiji la Dar es Salaam kuna watu wamejenga kwenye vyanzo vya maji na mito, sasa na maji yamekuwa kero hayaendi. Sasa nimwambie Mheshimiwa Waziri aangalie namna gani hawa watu waondoshwe kwenye maeneo haya kama wamevamia. Kama ni wa kupewa fidia wapewe ili hivi vyanzo vya maji viwe salama na hata mvua ikinyesha basi mafuriko yasiwaathiri wananchi wengine ambao wapo pembezoni na karibu ya hawa waliojenga viwanda na nyumba kubwakubwa waondolewe. Hata kwenye fukwe za bahari pia tumeona kuna baadhi ya watu wanavamia zile fukwe za bahari wanajenga maeneo yale, sasa wale ambao hawapo kwa mujibu wa sheria na wamekiuka kanuni pia waondoshwe kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala hili la upimaji wamaeneo, lakini sasa gharama nazo zimekuwa ni kubwa. Tuangalie haya maeneo ambayo hayajapimwa, hivi viwanja ambavyo vinapimwa kuna gharama ambazo zinakuwa ni changamoto kwa hawa wahusika. Kwa hiyo pia Mheshimiwa Waziri aangalie namna gani ya kulitatua suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu madeni; kuna viongozi pia wanakaa kwenye hizi nyumba za mashirika ya nyumba ambazo zipo kwenye Wizara yako, lakini sasa kuna changamoto, kuna baadhi ya wengine pia wanadaiwa tukiwemo na sisi Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tujitahidi tulipe madeni ambayo tunadaiwa ili na Serikali nayo ipate mapato na wafanyakazi wapate kujikimu na kutatua changamoto ambazo zinalikabili Shirika hili la Nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tuangalie na punguzo pia kwenye hizi nyumba mmesema kila mahali panajengwa nyumba tumeona huo mradi wa Kawe tumeona mradi wa Arusha, tumeona hata hapa Dodoma mlivyojitahidi lakini pia sasa wananchi wanalalamika kuwa kodi ni kubwa. Kwa hiyo, tuangalie punguzo la kodi Mheshimiwa Waziri ili angalau sasa na Serikali nayo ipate siyo kumkamua tu yule mwananchi ambaye amekodisha nyumba tuangalie kitu ambacho ni rafiki na yule mpangaji.

Mheshimiwa Spika, kuna hawa wajane hawa wakinamama wanaopoteza wenza wao wakaachiwa mali wengine wanaachiwa majumba wengine wanaachiwa viwanja sasa unakuta wengine wamechuma zamani yale maeneo yanakuwa sehemu ambazo ni nzuri sana maeneo ya mjini. Kumekuwa na utapeli na umeona ni namna gani mpaka Rais anaingilia migogoro hii kuwasaidia hawa wajane.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe na Mheshimiwa Lukuvi amekuwa mkali sana sasa inapofika pahala hawa wanaodhulumiwa wanafika mpaka ngazi za juu mkishafikia maamuzi basi nao wapate zile stahiki zao kwa wakati muafaka. Kwa hiyo, tumeona ni namna gani hawa wamama wengine wanakufa na *pressure* wengine si wanasheria wengine hawana taaluma za kudai mirathi kwa hiyo wale wajanja wengine wanacheza na watu ambao wanajua ujanja ujanja wa kutapeli kwa hiyo muangalie namna gani ya kuwasaidia hawa wajane.

Mheshimiwa Spika, tuangalie hata maeneo ya mjini nayo pia upimaji wake siyo mzuri sana, haya maeneo ya mjini muangalie namna gani ya kupitia maeneo yote ya mjini ili yapimwe tuangalie hizi nyumba ambazo hazijakaa katika muelekeo mzuri sana na wengine unakuta kwenye maeneo ya wazi wanavamia wanajenga maeneo ya mjini. Kwa hiyo, muangalie namna gani ya kupima haya maeneo ya mjini.

Mheshimiwa Spika, kuna wengi watashangaa watasema nimechangia Wizara hii mimi ni Mbunge wa Taifa kila pahala popote nitachangia tu. Nakushukuru sana kwa

kunipa nafasi hii na niwanasihi ndugu zangu waislamu wenzangu na viongozi wote wa dini wazidi kutoa elimu ya corona na wafuate maelekezo ya Serikali Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Libariki Bunge la Tanzania, Mungu Mbariki Spika wetu ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Maryamu Msabaha Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer kule Msekwa Mbunge wa Monduli

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kukushukuru kwa nafasi hii ambayo umetupa kuchangia jioni ya leo, lakini nikupongeze pia kwa namna ambavyo umesimamia Bunge letu kwa miaka mitano, na hakika tumeona uongozi wako sisi vijana tutaiga mengi mazuri ambayo umetufundisha pamoja na ustahimilivu mkubwa na kusimamia haki kwa wote pamoja na changamoto zote ambazo Bunge letu limepitia. Wewe ni Mbunge na Spika mahiri ambaye pamoja na historia ya Bunge letu kwamba ni Bunge ambalo lilikuwa na bunge wengi wa upinzani ambao kwa vyovyote vile wangeleta changamoto lakini umesimamia Bunge letu imara umeilinda nchi yako na umeilinda heshima ya Bunge letu tunakushukuru sana pamoja na viongozi wote wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, leo nitasema juzi nilisema habari ya Wizara ya Maji, lakini leo pia nitasema kwamba ni miaka mitano nasimama mbele ya Bunge lako hili tukufu nikijivunia mafanikio makubwa sana ambayo yametekelezwa na Wizara ya Ardhi katika Jimbo letu la Monduli na kwa kweli nimpongeze sana Mheshimiwa Lukuvi kwa uadilifu wake mkubwa na utayari wake wa kufanya kazi usiku na mchana kuwatetea Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lukuvi amekuja Jimbo la Monduli mara tano nadhani ni historia hakuna Waziri aliyewahi kufika katika Jimbo hilo kwa miaka mara tano katika historia ya jimbo hilo. Lakini katika nyakati zote ambazo amekuja ametufanyia mambo makubwa na Mheshimiwa Lukuvi sisi watu wa Monduli unajua kuna wenzetu wako

kwenye jimbo lako kule Isimani, sisi tutaendelea kuwashawishi kwamba wewe ni Mbunge mwenye heshima na uadilifu mkubwa katika Taifa hili waendelee kukuenzi na kukupa nafasi ya kuendelea kuwatumikia watanzania katika maeneo mbalimbali kwasababu umegusa maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaingia katika Bunge hili kwa miaka mitano iliyopita tumefanikiwa kurejeshewa sisi peke yake katika Jimbo la Monduli ekari zaidi ya 60,000 ambazo zimesimamiwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia Waziri wake huyu wa Ardhi. Sisi watu wa Monduli tutawaombea dua Mungu awalinde na kuwapa afya njema wakati wote.

Mheshimiwa Spika, wakati nakuja hapa tulikuwa na tatizo kubwa sana la ardhi katika shamba la Manyara *Ranch*, Waziri Mkuu alikuja kutukabidhi shamba hilo mwaka 2017 na sasa ni hati miliki ya wananchi kwa Vijiji vya Luksari. Lakini si hilo tu tumerejeshewa mashamba 13 yenye ekari 13,000 katika maeneo ya Luksari na Lehoti. Tumerejeshewa mashamba karibu 5,000 katika maeneo ya Nalalan haya yote ni mafanikio katika uongozi huu na katika kipindi chetu hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri ninaomba nikukumbushe mambo makubwa matatu ili utusaidie, jambo la kwanza ulipokuja Monduli mwaka jana uliagiza mgogoro wa Monduli na Arumeru katika eneo la mfereji uwe umekamilika kabla mwezi wa 12. Mheshimiwa Waziri jambo hilo bado halijakamilika pamoja na kwamba halmashauri yetu imeshatoa fedha hizo ambazo ilipaswa kutoa tangu mwezi wa kumi mwaka jana kazi hiyo naomba uimalizie ili wananchi wetu wapate amani kwasababu wameshapata madhara makubwa sana tangu mwaka 1980 mpaka leo ni nyinyi ndiyo mmekuja kuwa wakombozi wa eneo hilo naomba mtusaidie tumalize mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna mgogoro kati ya Monduli na Babati tunaomba hilo na lenyewe mlimalizie lakini

tuna tatizo kati ya Mswakini na eneo hili la Tarangire *National Park,* naomba na lenyewe muweze kutumalizia lakini Mheshimiwa Waziri ninaomba pia kwamba tatizo la ardhi nyingi kuwa na mgogoro kwa mtazamo wangu Mheshimiwa Waziri ni kwasababu watumiaji wengine wa ardhi wamekuwa wakiingia katika matumizi ya ardhi mbalimbali bila kupata baraka ya *custodian* ya ardhi ambayo ni Wizara yako na sehemu kubwa ambayo imekuwa ikivamia ardhi nyingi za wananchi na za vijiji ni Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nafikiri katika eneo hili asiwepo mtumiaji mwingine yeyote anayeruhusiwa kuvamia ardhi yeyote ambayo imetengwa kwa kusudi fulani mpaka wamepata baraka za Wizara yenu kuliko sasa ambavyo nyinyi kazi kubwa mnaenda kuwapimia lakini kabla ya kuwapimia ni muhimu sana kutambua kama misingi ya upatikanaji ardhi imefuatwa katika maeneo mbalimbali tukifanya hivyo tutakuwa tumedhibiti migogoro mingi ya ardhi ambayo imekuwa ikiendelea katika nchi yetu kwasababu ya uvamizi ya watu katika ardhi ambayo tayari imeshatengwa kwa majukumu mengine.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa niseme hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi naunga mkono hoja nakushukuru sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa

Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge hasa katika kipindi hiki tunapopambana na janga la Covid-19.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imetekeleza kwa ufanisi mkubwa masuala ya ardhi na pia kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi wa Wizara na Maafisa Ardhi Tanzania nzima. Changamoto nyingi za migogoro ya ardhi imetatuliwa na hata utolewaji wa hati za umiliki wa ardhi imeboreshwa na kupunguza kabisa vishawishi vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kuendelea na mikakati ya kuboresha mipango miji ili kuondokana na ujenzi holela. Miji mingi inachipuka kutokana na kuongezeka kwa wakazi na hii miji mipya inakumbana na ujenzi holela. Wizara ihakikishe inakuwa na mkakati wa kupima ardhi kulingana na mpangilio mzuri wa matumizi ikiwemo ardhi kwa matumizi ya kilimo na mifugo. Mpangilio mzuri wa ardhi uwezeshe kutambua mashamba makubwa ya kilimo na mifugo inayoangukia ndani ya mipaka ya Halmashauri za Miji.

Mheshimiwa Spika, nashauri uwepo mkakati wa mipango miji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya hasa kwa Mji Mdogo wa Mbalizi; Kata ya Swaya; Kata ya Ijombe; Kata ya Ihango; Kata ya Iwindi; Kata ya Bonde la Songwe na Kata ya Ihango, ambazo zinakuwa haraka kutokana na kulizunguka Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukupongeza wewe kwa juhudi kubwa unayoichukua kuliendesha vyema Bunge letu tukufu. Namuomba Mungu akupe afya njema ili uweze kumudu kazi zako na kuwa umakini zaidi. Aidha, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote kwa kutayarisha hotuba hii na hatimaye kuweza kuiwakilisha kwa ufasaha wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo na nianze na suala la migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumebahatika kuwa na maeneo makubwa sana ukilinganisha na nchi jirani. Lakini bado migogoro kati ya makundi haya mawili inaendelea na kuhatarisha maisha ya jamii hizi. Serikali inajitahidi sana kupunguza migogoro hii lakini bado haiishi. Inawezekana njia zinazotumika katika kutatua tatizo hili sio sahihi. Serikali yetu inatumia njia ya maelekezo ya kiofisi zaidi badala ya kuwashirikisha jamii hizi katika kutatua migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa Serikali kuchukua juhudi maalum za kuwashirikisha wahusika katika kutatua matatizo haya, hii itawafanya wahusika kujiona kuwa wanathaminiwa na ni sehemu ya watu wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, mipango mizuri mingi inayopangwa na Wizara inakwama kutokana na fedha inayotengwa Bungeni kutotolewa kabisa au kwa wakati. Serikali kwa kutambua umuhimu wa kupanga ardhi yote ni kwa nini hawatoi fedha iliyopangwa?

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa uliyokuwa inatekelezwa na shirika la Nyumba *(NHC)* ukiwepo ya *Morocco Square,* Kawe na kadhalika ilisimamishwa na Serikali

kwa mwaka wa tatu sasa. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha miradi hii imekamilika?

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali kurejesha Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya kuwa chini ya Mahakama utakuwa na tija na kuondoa migogoro ya ardhi kwa *level* za chini ikiwa kutakuwepo na umakini mkubwa sana na kuwepo dawati maalum kwenye Mahakama zote kuanzia Mahakama za Awali.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mgogoro wa ardhi lililopo Kata ya Ushokora, Wilaya Kaliua uliodumu tangu mwaka 2003, wananchi zaidi ya 200 waliochukuliwa ardhi yao kwa lengo kuandaa mipango miji mpaka leo hii haujapatiwa ufumbuzi pamoja na maelekezo ya Naibu Waziri aliyoyatoa kwa Halmashauri ya Kaliua bado. Kwa kuwa tayari Halmashauri ya Wilaya walishapata eneo lingine na kujengwa ofisi za Halmashauri na hawana fedha ya kulipa wananchi kufidia maeneo yao. Naomba Serikali ipeleke barua rasmi kutoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa migogoro ya ardhi hapa nchini na kuwa na miji iliyopangwa ni lazima Serikali kujipanga kupima kila kipande cha ardhi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha mipaka ya yetu yote ndani ya nchi yetu imewekwa sawa maeneo yote kwa wakati huu bado tukiwa na amani na mashirikiano mazuri na viongozi wa nchi hizo?

Mheshimiwa Spika, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha migogoro yote ya mipaka katika mikoa maeneo mengi inatatuliwa kwa haraka ili wananchi na viongozi washughulike na maendeleo na sio migogoro isiyokwisha?

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuendelea kukupongeza kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliendesha Bunge kisayansi, umahiri na weledi mkubwa. Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Lukuvi, Waziri

mchapakazi na asiyechoka kwa kazi kubwa ambayo ameifanya tangu amekuwa Waziri wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali katika mambo machache yafuatayo; jambo la kwanza ni kuhusu hati za kimila za kumiliki ardhi. Kwa muda mrefu sasa hati hii imeendelea kutothaminiwa na kuheshimiwa na asasi za fedha hasa mabenki ya biashara katika kutumika kama dhamana ya kupata mikopo. Nashauri Wizara iunde Kamati yenye wataalam kufanya utafiti na tathimini katika jambo hilo ili kuona ukubwa wa tatizo na sababu zinazosababisha hati hizo kunyanyapaliwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni uvamizi wa ardhi ya wanyonge unaofanywa na wenye nguvu ya fedha na kuzitumia Mahakama au Mabaraza ya Ardhi kuchelewesha mashauri na hivyo kupoka haki ya wanyonge. Niishauri Serikali kuweka utaratibu au kuunda idara au kitengo kitakachokuwa na vikosi kazi *(Land Rangers)* kwenye za Wilaya au Kata kwa kuwaondoa mara moja wavamizi pale Wizara inapojiridhisha kuwa kweli kuna uvamizi badala ya kuwaacha wanyonge maskini kupelekana mabarazani.

Jambo la tatu ni ukosefu wa ramani za vijiji katika Ofisi za Ardhi za Wilaya na hivyo kufanya vijiji vingi kuwa na migogoro ya mipaka kati ya vijiji na kijiji. Niishauri Serikali kutoa agizo kwa maafisa watendaji wa vijiji kutoa uthibitisho wa kuwepo au kutokuwepo ramani hizo ili pale ambapo ramani zitakosekana Wizara ione umuhimu wa kupitia upya mipaka hiyo na kutoa ramani upya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mungu kunipa afya na mimi kuweza kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nashauri fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo zipelekwe kwa

wakati ili kutekeleza miradi hiyo. Nashauri Serikali iongeze muda kwa wale wananchi waliojaza fomu za kutaka viwanja maeneo mbalimbali ya nchi yetu, na wanatakiwa ndani ya siku 90 wawe wamemaliza malipo hayo na kama hawajamaliza watapokonywa, hivyo kutokana na janga la Corona mzunguko wa fedha umekuwa mdogo. Naishauri Serikali iongeze muda kutoka siku 90 hadi siku 180.

Mheshimiwa Spika, nashauri vibali vya ujenzi vinavyotolewa na Halmashauri husika wasiruhusu wananchi kujenga maeneo ya milima na vilima kama ilivyo Mkoa wa Morogoro Mjini, ujenzi unaendelea katika maeneo hayo ambapo ni hatari sababu wanaharibu vyanzo vya maji, pia mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mwisho naishauri Serikali kwa wale wananchi waliojenga ndani ya hifadhi ya barabara, reli na kadhalika wasilipishwe kodi za majengo na kodi za ardhi, pia huduma muhimu wasipelekewe, sababu Serikali inapofanya hivyo inawapa matumaini wenye maeneo hayo kuwa wamejenga kihalali, kisha Serikali inapokuja kubomoa na kuwaondoa wananchi hao huona wa wameonewa, hivyo Serikali ijikite kuwaelimisha wananchi kutojenga katika maeneo hayo na pia kuwaelimisha watendaji wa Halmashauri zetu wasitoe vibali kwa wananchi kuwaruhusu kujenga katika hifadhi za barabara, reli na kadhalika.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika Bajeti ya Ardhi kama ifuatavyo; kwa kuwa wataalam wa upimaji wa ardhi hawatoshi naiomba Serikali iongeze wataalam katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha ya upimaji ni kubwa shilingi 150,000 kila kiwanja, naomba Serikali ishushe gharama hiyo na kuwa shilingi 100,000 na hasa upimaji wa mashamba.

Mheshimiwa Spika, urasimishaji wa ardhi hasa katika maeneo ya vijijini unakwenda polepole. Mfano katika Mkoa wa Njombe maeneo mengi bado ardhi haijarasimishwa.

Niiombe Serikali kuharakisha urasimishaji huo ili Serikali isikose mapato.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe fedha za kutosha kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, nianze na urasimishaji wa makazi; zoezi hili lina changamoto nyingi; zoezi linachelewa sana kuhitimishwa, wakandarasi hawana uwezo kulimudu zoezi hili. Mfano, kwa Mkoa wa Dodoma zoezi hili bado lipo nyuma sana; maeneo kama Nkuhungu, Maili Mbili, Chadulu na kadhalika zoezi hili bado. Zoezi hili linachangamoto zaidi wa wasiokuwa na uwezo hususan kwa wazee na watu wenye ulemavu ama walio na kipato duni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi bora ya ardhi, ni muhimu katika muktadha mzima wa usalama wa chakula, afya na maendeleo ya jamii kwa ujumla wake. Ni vyema Wizara ikahakikisha inatekeleza sera yake ya upimaji na utekelezaji wa Mipango Miji. Upatikanaji wa haki za umiliki kwa wakati, hufanikisha maendeleo endelevu na kutunza mazingira. Mifumo bora ya umiliki wa ardhi itasaidia kuweka miongozo wa namna ya kuratibu wanajamii na husaidia katika uzalishaji, na hivyo kuondoa/kudhibiti migogoro.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuijalia nchi yetu neema, baraka, amani na mafanikio kwa muda wote, mimi nasema haya kwa kuwa tuna mifano mingi sana kwa kulinganisha na mataifa mengi sana hususan Bara la Afrika. Aidha tuendelee kumwomba sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kutuondoshea janga hili la Corona linalotikisa nchi yetu na dunia nzima kwa ujumla. "Ewe Mwenyezi Mungu Uturehemu."

Mheshimiwa Spika, kama desturi yetu Watanzania tunawapa pole nyingi sana wale wote waliofiwa na

wapendwa wao kwa namna mbalimbali Mwenyezi Mungu awarehemu na kuwapokea katika ufalme wake usio na mwisho.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli, Rais wetu mpendwa, pamoja na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika wetu, Baraza la Mawaziri wote na waandamizi wote Serikalini kwa jinsi walivyosimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015 - 2020. "Hongera sana Serikali ya Awamu ya Tano." "CCM tuko kidedea kuelekea uchaguzi mkuu."

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kuishauri Serikali kupitia Wizara hii; pamoja na salamu zangu za pongezi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini kwa Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nyingi walizofanya toka mwaka 2016 mpaka sasa, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa kutupatia Baraza la Ardhi la Wilaya ya Mbulu.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI watazame uwezekano wa kila Halmashauri kupata Maafisa Wapima Ardhi ili kuepuka ujenzi, hongera, mfano huo upo Halmashauri ya Mji wa Mbulu hatuna Maafisa Ardhi kabisa.

Kwa kuwa Wazee wa Mabaraza ya Ardhi kote nchini hawana posho hali inayoshawishi mianya ya rushwa na wenye uwezo kuwarubuni kunyang'anywa haki za wanyonge. Serikali itazame namna ya kutafuta chanzo cha kuwapatia posho Wazee wa Mabaraza ya Ardhi kote nchini.

Kwa kuwa Maafisa Tathimini ngazi za Wilaya, Mikoa wamekuwa na desturi ya kutoa uthamini wa ardhi kwa gharama kubwa sana kwa ajili ya matumizi ya umma Serikali itoe maelekezo katika kutwaa ardhi na kufidia kulingana na

maeneo ardhi hiyo iliko katika eneo la Halmashauri za Wilaya na Miji ili kuzuia udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Mbulu ina migogoro mingi tunaishauri Serikali iweke kipaumbele kupima na kurasimisha ardhi ya Wilaya ya Mbulu ili wananchi wawe na hati miliki za kimila. Serikali itafute mpango wa kuvipatia Halmashauri vifaa vya upimaji hata kwa kuzilipia kwani kwa sasa changamoto kubwa kwenye Halmashauri ni ukosefu wa vifaa na wataalam wa ardhi hali inayochangia ujenzi holela mijini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ifanye tathimini migogoro ya ardhi kwenye mipaka, taasisi, mtu na mtu ili kuona baadhi ya migogoro kutatuliwa na ngazi za Wilaya na Mkoa hali hii itapunguza mzigo mkubwa unaobebwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, maombi kwa Wizara kwa kuwa *NHC* ina majengo yake chakavu katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu eneo lililopo katikati ya mji. Naiomba Wizara ielekeze kujenga majengo ya biashara ya ghorofa ili kutoa fursa za *shopping mall* kwa kuwa Mji wa Mbulu unakua haraka kuelekea kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shughuli za kiuchumi, kijamii na mabadiliko ya tabia ardhi inatupa changamoto nyingi Serikali itumie Maafisa Ardhi, Mazingira katika Halmashauri, kuainisha baadhi ya maeneo ambayo tayari yanahitaji matumizi bora ya ardhi.

Kwa kuwa mchakato wa upatikanaji wa hati katika Manispaa ya Dodoma inachukua muda mrefu sana hata kwa sisi Wabunge, je, kwa wananchi wa kawaida hali hii ikoje? Hivyo basi Serikali itazame utatuzi wa jambo hili kuleta ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa viwanja vingi vilivyopimwa havilipwi kodi ya ardhi hali inayokosesha mapato ya Serikali, hivyo basi Serikali iandae utaratibu wa kila Halmashauri kuhaulisha kumbukumbu ya viwanja vyote

ili kuona utaratibu wa kodi limbikizi ubadilishwe na kulipwa kwa miaka miwili ya mwisho ili kutoa hamasa na kupata *data* halisia.

Mwisho, naunga hoja kwa 100% na naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi kwa Chama cha Mapinduzi kwa kuipatia nchi Rais mchapakazi, hodari katika maeneo mengi, shupavu na mwenye dhamira chanya kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais na Serikali yake awamu ya tano akisaidiwa kwa karibu sana na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu. Pongezi mahsusi kwa Waziri Mheshimiwa Lukuvi na Naibu wake Mheshimiwa Angelina Mabula, pia Katibu Mkuu na timu nzima ya wataalam.

Mheshimiwa Spika, nina mchango wa maoni kwa ufupi kama ifuatavyo; kwanza ufumbuzi wa mgogoro wa ardhi wa shamba la Nambarapi ungepatiwa ufumbuzi haraka ungewasaidia wananchi wa vijiji zaidi ya vinne kupata manufaa ya kiuchumi na kijamii na kuwapunguzia umaskini. Hii ni kwa mujibu wa maelekezo ya Ilani ya CCM kwa Serikali yake kuhusu mashamba pori.

Pili, suala la upungufu mkubwa wa wataalam katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru lifanyiwe kazi. Tunaomba jambo hili litazamwe kwa upekee kutokana na Tunduru kuwa mbali, mpakani na kwamba tunahitaji kwenda kasi kufikia maendeleo baada ya kubakia nyuma kwa muda mrefu kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Ardhi la Wilaya halijaanza kazi vema ipasavyo. Serikali ione haja ya kutatua changamoto zilizopo ili Baraza lianze kazi mapema. Hii itaongeza kasi ya Serikali kushughulikia migogoro ya ardhi miongoni mwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Spika, hongera sana kwa jinsi ulivyosimamia na kuliongeza Bunge kwa hii miaka mitano. Mungu awe nawe.!

Napenda kutoa pongezi za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kazi nzuri yenye weledi mkubwa kwa wananchi na maslahi ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, sina zaidi kutokana na kazi yao nzuri na kwa hilo la kuzitoa Ofisi za Kanda na kuwezesha shughuli za upatikanaji wa hati miliki kupatikana mikoani mwetu. Sasa mikoa yetu haitakuwa mchanganyiko ya miji yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa dhati.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Laizer sasa mtaona kwamba Mheshimiwa Waziri tumetumia nafasi kubwa sana Waheshimiwa Wabunge kuchangia katika Wizara hii na hatuna mahali popote pakushika Mshahara wa Waziri.

Kwa hiyo, tumewabakizia dakika si nyingi ili mtoe tu ufafanuzi wa hapa na pale na mengine mnaweza mkafanya kwa maandishi kwasababu Wabunge wote wamekubaliana kwamba kazi mnayofanya ni nzuri, na hata mwaka jana tuliwapangia siku mbili lakini Wabunge hawa hawa wakasema siku moja inatosha na tukaifanya bajeti hii kwa siku moja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri dakida 10, Mheshimiwa Waziri dakika 15 ili tuweze kumaliza. Karibu sana Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt Angelina Mabula.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia katika Wizara hii yetu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nianze kwanza kwa kumshukuru mwenyezi mungu kwa namna ambavyo anatujaalia afya njema ambaye anatuwezesha kuja kuendelea kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameendelea kuniamini na kuniweka katika Wizara hii kwa miaka yote mitano tunayokwenda kuimaliza na nimepata uzoefu mkubwa kabisa chini ya Waziri wangu ambaye ni Waziri mahiri kama mlivyompongeza pamoja na watendaji wetu ambao tunasaidiana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana wewe pamoja na Naibu Spika pamoja na watendaji wote wa Bunge kwa namna ambavyo mmetupa ushirikiano mkubwa katika kufanya kazi zetu ziende vizuri pia, niwashukuru sana Wabunge na hususan pia ni kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa ushauri na maoni yao mazuri ambayo wamekuwa wakituongoza chini ya Mheshimiwa Kemilembe kwa kweli mmetuongoza vizuri tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Ilemela ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini pamoja na majukumu makubwa ya kitaifa ambayo nilipewa na Mheshimiwa Rais lakini sikuwasahau niliwakumbuka kila mara nilipokuwa napata fursa ya kuingia Jimboni na nikafanya nao kazi. Na niwaahidi tu kwamba dhamana waliyonipa nimeifanya vizuri na tutaendelea kufanyakazi kwa ushirikiano na waendelee kuamini kwamba hata unapopewa majukumu na Serikali bado unaweza ukafanya kazi jimboni kwako.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nishukuru familia yangu pamoja na kwamba leo ninasimama nikiwa nimempoteza baba na mama na mume wangu ndani ya hii miaka mitano lakini nashukuru sana wanangu wamezidi kunipa faraja kunitia moyo na nimefanya kazi vizuri sana namshukuru mwanangu David na mke wake Sandra, namshukuru mwanangu Jacqline na mume wake James lakini namshukuru Diana na Dorothy ambao kwa kweli wamekuwa karibu. Lakini niishukuru pia na familia yangu yote kwa ujumla namna walivyoweza kunipa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana Chama Cha Mapinduzi ambacho kimeniweka hapa kutokana na Chama Cha Mapinduzi ndiyo nimepata pia fursa ya kuwakilisha Bunge nasema sijawaangusha tutatekeleza ilani kama ambavyo wanatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii sasa kumpongeza sana Mheshim Rais Dkt. John Pombe Magufuli kama ambavyo hotuba ya Mheshimiwa Waziri imepongeza kama ambavyo Wabunge mbalimbali wamepongeza kwa kweli ni Rais ambaye ni wa mfano ni Rais wa karne, ni Rais ambaye anaishi katika maono yake. Mengi yamesemwa namna ambavyo amewezesha nchi hii kwenda hasa katika ile miradi ya kimikakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie tu kwenye suala la ardhi namna ambavyo ametuwezesha wananchi wengi na walio wanyonge walikuwa wanalalamika sana katika maeneo yao, kwamba wana maeneo, wanaardhi lakini hawawezi kumiliki kwa maana ya kwamba wamejenga majengo katika hali ambayo si ya kuzingatia sheria kwa maana ya sheria walitakiwa wabomolewe. Lakini Mheshimiwa Rais akasema warasimishiwe wote na waweze kupata haki yao waweze kutumia katika shughuli za kimaendeleo, na zoezi hilo limefanyika na limekwenda vizuri kwa nchi nzima na kasi inaendelea na kwa kutumia hizo hizo hati zao kwa kweli wameweza kutumia katika shughuli za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili lilikuwa ni zoezi zuri na ni zoezi gumu lakini wananchi wameweza kuamka, rai yangu kwa wananchi zoezi hili si endelevu kwa miaka yote na ni kwamba halitaendelea kwa muda wote sasa wale ambao bado hawajachangamkia fursa hii niwaombe sana wachangamkia ili waweze kumiliki maeneo yao kihalali waweze kutumia katika shughuli za kimaendeleo Wabunge wamechangia wengi hapa wakizungumzia hilo na mambo mengine na Mheshimiwa Mbunge wa Nyamagana amelizungumzia na akatoa na takwimu jinsi gani ambavyo watu wameweza kuchangamkia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu fursa hii ambayo Mheshimiwa Rais ameitoa tusiichezee, tusiipoteze tuhakikishe kwamba tunachukua hatua katika kuhakikisha tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Makamu wa Rais mlezi wa Halmashari yetu ya Ilemela lakini nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kiongozi wetu katika Serikali hapa anavyotusimamia na kutupa miongozo kadhaa ambayo tunakwenda kufanyakazi vizuri kwa kushirikiana. Katika uchangiaji Wabunge wamechangia 20 kwa kusema lakini Wabunge 7 wamechangia kwa maandishi na kabla muda haujaisha niseme tu kwamba yote tumeyapokea tutayafanyia kazi na majibu watapata.

Mheshimiwa Spika, lakini nilitaka kutoa ufafanuzi tu kidogo changamoto nyingi zinazotokana na migogoro ya ardhi au na yale ambayo mmeyazungumza yanatokana na mambo kama manne ambayo yapo. Jambo la kwanza ni lile suala la wananchi kutoelewa sheria na kujua haki zao wapi waende wakadai haki zao hilo limekuwa ni kikwazo wanashindwa kujua.

Mheshimiwa Spika, lakini pia uhaba wa vitendea kazi mmesema lakini Wizara kama ambavyo hotuba imejipambanua tayari Wizara imeshachukua hatua tunakwenda kumaliza tatizo hilo, tatizo la upungufu wa wafanyakazi tayari linachukuliwa hatua tutakwenda kuwapanga watumishi wote kulingana na mahitaji tunatambua kabisa wazi baada ya kurudi Wizarani tulikuwa bado tunakazi pia ya kujua tunao watumishi wangapi na tuwapange namna gani katika halmashauri zetu kulingana na zile sekta zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili litakwenda kuondoa tatizo lote hilo tumeshusha huduma zile kwenye mikoa kama Waziri alivyosema na tayari iko kisheria lakini sasa tunapoboresha kwenye mkoa bado kule chini kutakuwa na mapungufu kama hatutaweza ku-*balance* watumishi katika

eneo lile. Kazi hii inafanyika na muda si mrefu tayari tutapata majibu yake.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo limezungumziwa na Mheshimiwa Shangazi akawa anazungumzia kwamba masuala ya watu kumiliki nyumba na kupata zile hati zao ni kwamba sheria inachelewa watu wanapunjwa, watu wanadaiwa kodi za miezi mingi niwaombe tu suala hili limefikia hatua nzuri tayari kwa yule mzabuni ambaye anafanya kazi hii ambaye ni Chuo Kikuu cha Ardhi wamefikia katika hatua ya kupokea maoni kutoka kwa wananchi. Sera yeyote na sheria yeyote huwezi kuitoa kama haijaingiza maoni ya wananchi lakini hii sera ya nyumba pamoja na makazi imefikia hatua nzuri ambako ndiyo mwelekeo pia wa kwenda kuanzisha ile mamlaka ya miliki kwa maana ya *Real Estate Regulatory Authority* sasa ile ikikamilika maana yake itakuwa inaumba kitu kizima ambacho hata kikija hapa kitakuwa tayari kimepata uelewa mzuri na watu watakwenda kufanya kazi ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini limezungumziwa suala la migogoro ya kisheria ambayo ipo hasa katika umiliki wa ardhi na kwa wafugaji na wakulima wamesema katika michango ya maandishi kwamba wanaomba makundi yale yawe yanahusishwa. Nadhani katika utatuzi wa migogoro tunahusisha sana katika pande zote unapokwenda kutatua migogoro lazima pia usikilize lakini kwasababu wamelileta tumelichukua kama ushauri tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Suala zima ubatilisho wa maeneo ambayo hayaendelezwi hili ni endelevu litaendelea na watu watambue tu kwamba hatujasimama litaendelea kama taratibu zilivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Lugola pia amezungumzia suala zima la kwamba hati miliki za kimila hazitambuliki naomba nimpe takwimu kidogo tu mpaka tunavyozungumza sasa zaidi ya bilioni 60 na milioni 760 zimetolewa katika mabenki yetu mabenki zaidi ya 13 ikiwemo

*CRDB, NMB, PSPF, Stanbic Bank, Access bank* na mabenki mengine na wametoa katika halmashauri 14 ambazo zimetumia hati hizo hizo hatimiliki za kimila na inayoongoza ni Mbozi wameshakopeshwa bilioni 48 ikifuatiwa na Mbinga bilioni 5.5, Babati milioni 600, Kilombero milioni 550, Arumeru bilioni 1.8 hizo ni chache tu ambazo nimetaja.

Mheshimiwa Spika, sasa pengine kama kuna mabenki mengine ambayo hayatoi ushirikiano katika eneo hilo basi tuombe tupate ili tuweze kufuatilia kwanini wengine wanatoa na wengine hawatoi kwasababu hizi zinatambulika kama hati zingine za kawaida. Kwa hiyo, hili nalo tunasema tunalichukulia maanani kuhakikisha kwamba tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, maana yake muda ni mdogo na unakwenda kama cherehani lakini tunasema bado tutaendelea kuona. Taratibu ya hati kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri amesema sasa tutakuwa tunawafuata kwenye halmashauri lakini kikubwa ni zile halmashauri zenyewe wakishafanya maandalizi ya wale watu wote kama hati ziko tayari wanakuwa wanaletwa kwenye sehemu moja itakuwa ni rahisi zaidi katika kufanya zoezi hilo. Kwasababu hatuwezi kusema kwamba watatoka waende wakakae siku 5, 10 wakigawa hati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukilifanya kama ambavyo tumekwishaanza kufanya sasa unatoa taarifa mapema wanaandaliwa wale watu na kazi inafanyika wanarudi kwenye maeneo yao hili linawezekana kabisa. Na katika ulipiaji wa hati Wizara ilishatoa maelekezo siyo lazima utoe pesa zote kwa mara moja wanaweza wakatoa kwa *installment* ili mradi iwe ndani ya mwaka huo huo wa fedha ili kuweza kupata pesa katika shughuli za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine lilizungumziwa suala la mapato, ni kweli pengine kasi ya mapato imekuwa ndogo kwa wakati huu lakini tukumbuke katikati tulikuwa na zoezi moja kubwa la kuondoa au kutoa maonyo kwa watumishi ambao hawakuwa waaminifu. Kwahiyo kidogo

kasi ilipungua sasa hivi kasi inaenda vizuri na napenda pengine kuwahakikishia kwamba mpaka kufikia mwisho wa bajeti tutakuwa tumefikia yale malengo ambayo tulikuwa tumekusudia kwasababu lengo letu ni kuhakikisha tunakusanya hii ni Wizara wezeshi na Wizara ambayo ikitumika vizuri kama ambavyo inatarajiwa mambo yote haya ya kuwezesha miundombinu ya kitaifa itakwenda vizuri kwasababu bila kupanga, kupima na kumilikisha ardhi vizuri basi mambo mengine hayawezi kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba tu niseme naunga mkono hoja na niwape salamu watu wangu wa Ilemela tuko pamoja na Mungu akijaalia tutaendelea kufanyakazi pamoja ahsanteni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt Mabula tunakushukuru sana. Sasa moja kwa moja nikukaribishe Mheshimiwa Waziri una robo saa karibu sana.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kunipa fursa ya pili ya kumalizia kukamilisha hoja yangu. Kwanza nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati chini ya Mwenyekiti wao kwa mchango mkubwa waliotupa. Nataka kuwahakikishia humu ndani, nina sekretarieti inayoongozwa na Katibu Mkuu. Yote mliyoyasema sisi tunaendelea na kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii haifunjwi, iko mpaka wakati baada ya uchaguzi. Kwa hiyo, tutafuatilia haya na tunayagawa yote haya kwenye mikoa yote na ni lazima tuyatekeleze. Nawashukuru sana kwa maoni yenu, yote mliyoyasema, tutayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Shangazi amechangia vizuri sana kasoro ndogo zilizobakia na ushauri wake tumeupokea. Naibu Waziri ameshazungumzia mapendekezo yake ya *Real Estate Regulatory Authority* tumeshafikia pazuri kama alivyosema. Haya mambo ya kodi ni uungwana tu. Tulishasema mara nyingi, hivi unamdaije mwanafunzi kodi ya miezi 12?

Unamdaije mfanyakazi anayeajiriwa leo kodi ya miezi 12? Haihitaji hata sharia, basi tumezoea kusukumwa na sharia. Ni *common sense* tu, lakini tunasubiri sheria itakuja ambayo itawekea utaratibu wa namna mambo haya yanavyotakiwa kufanyika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana Mheshimiwa Lwakatare, nakutakia maisha marefu, ni kweli tunafahamiana siku nyingi, wewe ni muungwana sana Mheshimiwa Lwakatare; na nimesoma kwenye mtandao umefukuzwa chama, sijui kwa nini wamekufukuza leo! Wewe ni muungwana sana, umefanya makubwa sana kwenye vyama vyako hivyo. Basi nakutakia kila kheri, nafikiri wananchi wa Bukoba wanakuelewa vizuri, utapumpuzika, vizuri. Sisi kwenye Chama cha Mapinduzi tunayo nafasi ya washauri, kama wamekufukuza tunazo kadi za akiba huku, tutakupokea kwa sababu mawazo yako na ustaafu wako tunauthamini.

Mheshimiwa Spika, pia ulisema una maoni ambayo Kambi yako wamekataa usisayome. Kama unayo, wewe bado ni Mbunge hapa. Mheshimiwa Spika hajatangaza kwamba umefukuzwa. Kwa hiyo, wewe niletee mimi nitayaangalia. Yenye tija tutayatumia, kwa sababu wewe unatambulika ni Mbunge. Haya maneno ya kwenye mtandao sijui nini, huwa sipendi sana kusoma, lakini sijui kama ni ya kweli. Nakupongeza sana, wewe ni muungwana, hata humu Bungeni hotuba zako zimekuwa za kiungwana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gekul tumefanya kazi vizuri huko Manyara, nakupongeza sana. Bila shaka wananchi wa Babati wanakuheshimu kwa kazi ulizowapigania kwa kipindi hiki cha miaka mitano. Mheshimiwa Dkt. Kiruswa nakushukuru sana, wewe ni mtu makini kweli, hata kwenye Kamati ni mtu unayejadili vitu kwa hoja. Zipo kero zote hizi kuanzia *Natron* nazijua, nataka kukuhakikishia Kamishna wangu wa kanda ya Arusha, Bwana Komba anayo hiyo orodha na Katibu Mkuu atawaandikia hii *matrix* watashughulikia yote haya na lazima yatekelezwe, kwa sababu sisi tupo kazini. Serikali ipo kazini, hakuna kuahirisha.

Serikali tunaendelea na kazi tu, hii ni awamu tu, miaka mitano inaisha baada ya uchaguzi na hawa Watendaji wa Serikali watafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, tumepata ushauri wako juu ya Makampuni haya yanayofanya kazi ya urasimishaji. Ni kweli tumezungumzia utaratibu mpya, makampuni yote yanayochukua kazi ya urasimishaji yawe na fedha, siyo kutegemea kuchangisha kwa watu. Lazima ukichukua mtaa wenye nyumba 100 uwe na fedha, ukope benki, urasimishe, ukamilishe michoro yote ili wananchi waweze kumilikishwa haraka.

Mheshimiwa Spika, hii ya kuchanga changa ndiyo inayotuchelewesha kwa sababu wanachanga wawili, watu 900 hawachangi, mchoro haupitishwi mwaka mzima, watu hawapati Hati. Tunataka Makampuni yote binafsi ambayo yanayofanya kazi hii, yaige mfano wa makapuni mengine ya ujenzi, wakipata *tender* huwa wanajisogeza wanakwenda kukopa, wanaanza kazi kabla ya kulipwa *down payment.* Tunataka makapuni ya upimaji yaendelee namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nape nakushukuru sana kwa kumpongeza Mkurugenzi, nami nampongeza kasi kubwa ya Bodi. Naipongeza Bodi mpya na Watendaji; Mkurugenzi mpya, wameanza vizuri. Hata kuaminika na Serikali Kuu kupewa miradi mikubwa ya mabilioni haya ni *legacy* kubwa. Sasa wamejipanga vizuri kufanya vizuri. Nashukuru pongezi zako tutamfikishia, sidhani kama hayupo, lazima naye amesikia hapa na ni Mmakonde mwenzako. Kwa hiyo, nakushukuru kwa pongezi hizi. Mapendekezo yako uliyoyasema na ushauri wa namna ya kurekebisha Bodi ya Nyumba tumeupokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Tanga nimemsikia vizuri, tutayaangalia haya maeneo aliyoyasema. Mheshimiwa Kilango, haya maneno uliyoyasema hujaanza leo, umeanza kuzungumza tangu ukiwa Mbunge wa Jimbo lile, nayakumbuka vizuri. Tumeenda tu juzi, lakini najua hawajakutendea haki kwa sababu maneno haya ya Kata

ya Ndungu umeanza kuyazungumza tangu wakati ule. Nataka kukuhakikishia, wananchi wa Ndungu kama wananisikiliza, tutayamaliza kabla ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu yupo hapa na kuna Kamishna mpya mwanamama nimemteua yupo Moshi, nafikiri wananisikiliza kwenye *youtube* sasa hivi, wiki hii nataka nipate taarifa ni nani huyu ambaye hajagawa hizi hekari 300. Maana kwetu sisi Wizara ya Ardhi mambo hayalali na hatushindwi jambo. Nikishaondoka hapo, sirudi kwa sababu naamini waliosikiliza wamefuatilia na wametekeleza. Kwa hiyo, hili jambo lazima litekelezwe na wenye mashamba tulikubaliana wanarudisha hati wanatenga hizi hekari 100. Sasa kilichobaki ni watumishi wa Serikali kwenda na vifaa vilivyolala pale Moshi vya bure, mkakate hizo hekari mia moja, mia moja, halafu mshirikishe wananchi namna ya matumizi bora ya ardhi ile. Wanataka kukaa wapi? Wanataka kufugia wapi? Wanataka kulima wapi? Msiwapangie matumizi, nyie kateni hekari 100 halafu mwasikilize wananchi wanataka kutumia namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chatanda nakushukuru sana, tutakwenda kuliangalia hili jambo la *TBA* tuone limekaaje pale kwako. Nakushukuru kwa mchango wako. Mheshimiwa Joyce nakushukuru sana, umesema maneno mengi kule ya Musoma, wewe una bahati, kwenye mtandao sikuoni, hawajakufukuza. Mheshimiwa Edwin Sannda umetoa mawazo ya kitaalam kwa sababu wewe ni mdau wa jambo hili, tunashukuru, tutashirikiana na kuhakikisha kwamba nao wanakuwa na *Master Plan*.

Mheshimiwa Spika, ushauri wako tumeupokea, ni kweli kwamba kila Halmashauri hasa miji zinahitaji kuwa na *master plan*. Suala la upangaji wa Watendaji Halmashauri yupo humu ndani, nimesikia, nimemwona mahali, nimeagiza mpaka ifikapo mwisho wa mwezi huu kila Halmashauri ya Mji, Manispaa na Jiji nchi hii lazima wawe na Watendaji wote muhimu wa Wizara ya Ardhi. Lazima awepo Mpimaji, Mpangaji na Afisa Ardhi. Ni lazima. Huwezi kuwa na Afisa Ardhi peke yake; nani atapanga na kupima?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, zoezi hilo la upangaji lazima likamilike kabla ya mwisho wa mwezi huu. Katibu Mkuu alipo ananisikia na Wakurugenzi wote ambao wanafikiri wana upungufu au wana Watendaji kwa sababu ndiyo wamerudi kwetu, wanafikiri wana taarifa za siri, wawasiliane na Katibu Mkuu mwezi huu ili wawapangie watumishi kwa namna ambavyo nimeelekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, zoezi hili liishe na kama Katibu Mkuu akikosa fedha, Wakurugenzi mkubali kulipia gharama za uhamisho, watu waje kwenu. Kwa sababu ni wenu wenyewe. Sisi tunao Watendaji tunawapanga vizuri wasilundikane. Nimekwenda Mwanza kuna Watendaji 60 wilaya moja. Sasa watu 60 wakati Mtamba hakuna hata mtu! Wilaya nyingine unakuta wapo 50, 40; ni upangaji tu, hatuhitaji kibali cha ajira mpya kwa sasa, tutawapanga hawa hawa; na fani zote zitatimia kwenye wilaya zote. Hili jambo lazima likamilike mwisho wa mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mabula mwanaume wa Nyamagana wewe umesema vizuri sana, nakupongeza kwa kusimamia. Katika nchi hii kasi ya urasimishaji imepamba moto sana na wamefanya vizuri kama kila mwaka tunavyosema ni Ilemela na Nyamagana, wamefanya vizuri sana. Kwa hiyo, nawapongeza sana Watendaji na Wakurugenzi wa Majiji hayo kwa kazi nzuri waliyofanya, nasi tutashirikiana kuhakikisha wanafanya. Tatizo hapa ni kweli kwamba hata mapato yetu yamepungua kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Mabula, tumepima viwanja zaidi ya milioni moja na nusu, tumeshaweka na mawe kama alivyosema Mheshimiwa Mabula, michoro yote imepitishwa, mawe tumeweka, Sheria yetu ya Ardhi inasema, sasa ni hiyari ya mtu kwenda kuchukua Hati.

Mheshimiwa Spika, tunataka kufanya marekebisho Bunge hili ili kama sisi tukitimiza wajibu wetu kama Serikali, tumeshapima, tumeshaweka na alama na *invoce* tumekupa, basi ndani ya siku 90 lazima kila mmoja mwenye eneo lake mijini awe ameshajitokeza kufuatilia Hati yake na Serikali iwe imeshampa Hati yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima iwe pande mbili, haiwezekani jirani yako hapo mmepima pamoja, mtaa mmoja, mwenzeko ana Hati, analipa kodi ya ardhi, wewe umepimiwa miaka mitano, eti sheria inakutaka hiyari yako tu ukafuate Hati. Kumbe tumekupimia wa nini? Wakati mwingine umechangia mwenyewe na gharama za kupima, ulipima ili upate Hati. Tunataka tukipima kila mtu amilikishwe apewe Hati, ndiyo lengo letu. Hizi fedha zinazokuja tumepewa na Serikali. Mwakani tunataka kupima kila kipande cha ardhi, kila mtu amilikishwe, umilikishaji unaishia kwa Hati. Kama wewe unafikiri una mawe kwenye kona, huna Hati, hujamilikishwa bado.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kila Mtanzania aliyepimiwa eneo lake *whether* eneo jipya au urasimishwaji, mwenye eneo la mjini ahakikishe anamiliki kwa Hati na ndiyo inasaidia; kwanza Serikali inapata mapato na pia inaondoa umigogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sasa kabla marekebisho ya sheria hayajapita, natoa siku 90, kwa wote ambao wanayaona mawe kwenye maeneo ya ardhi ya mjini, wajitokeze kwenye Ofisi za Ardhi za Wilaya wakaombe Hati. Maafisa wangu wa Wilaya na Makamishna wa Mikoa wahakikishe wanafuatilia watu wote. Sasa hivi tuna viwanja 900,000 nchi hii. Watu ambao tumeshawapimia kwa miaka mitano hii hawajachukua Hati.

Mheshimiwa Spika, kama wangekuwa wamechukua Hati hawa watu wote, tungekuwa tumeshakusanya zaidi ya shilingi bilioni 135. Kwa hiyo, tuna fedha zaidi ya shilingi bilioni 135 zimelala tu kwa sababu kuna watu hawapendi kwenda kufikia Hatima ya kuchukua Hati. Kwa hiyo, nataka Makamishna mfuatilie na Maafisa Ardhi mhakikishe watu wote ambao tumewapimia viwanja lazima mwamilikishe katika siku 90. Namkushukuru sana Mheshimiwa Mabula.

Mheshimiwa Spika, nimwambie Mheshimiwa Kitandula tutarudi tena huko kupekua mashamba ambayo hayajafutwa. Tunazo taarifa na Mheshimiwa Bura

ameusemea vizuri, ameutendea haki Mkoa wa Dodoma, tunakushukuru sana. Nataka kurudia, kama alivyosema, Halmashauri zinapima ardhi kama miradi ya kujitegemea. Sawa, lakini sasa tumewaondolea kero ya usimamizi na uidhinishaji wa kazi zenu tumeleta Mkoani. Kwa hiyo, tutasimamia sasa na bei mnazotoza za viwanja vya wananchi. Haiwezekani mmegharamia, ndiyo kulipia fidia, halafu mnawatoza watu mpaka hela za kujenga miundombinu. Zinaingia Halmashauri halafu miundombinu hamjengi. Hamjengi barabara, hampeleki hata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa najua ni *own source yes,* Ardhi ninyi ni wapangaji, ndio, lakini lazima tupange kwa viwango vinavyohimilika. Kwa sababu gharama sasa zimepungua. Vifaa vya upimaji tutawaazima bure, wataalamu tutawapanga, lakini lazima kila Halmashauri inapochukua ardhi ya mtu ilipe fidia kwa wakati.

Kwa hiyo, hili naamini kwamba tutasimamia pamoja, tutahakikisha kwamba Makampuni yanatekeleza wajibu wake. Makampuni yote ambayo yatakuwa hayajatimiza azma ya kumaliza viwanja na kuwapelekea wananchi wao kukamilisha kazi walizopewa mwisho wa mwezi huu tunayafuta yote.

Mheshimiwa Spika, Makampuni binafsi yote ambayo yamechukua kazi ya urasimishaji nimeshatoa muda mpaka mwezi wa Nne tarehe 30, wameomba muda, lakini mwisho wa mwezi huu, kama Kampuni ilichukua hela za wananchi ya urasimishaji, wamechangisha lakini hawajamaliza kazi, Wasajili wa Taasisi hizo lazima wachukue hatua za kufuta Kampuni hizi zote. Tutasajili nyingine kwa sababu wapo Wataalamu wengi waliosomea fani hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Pallangyo nakuheshimu sana, tutafuatilia hili suala la Momela. Mheshimiwa Taska Mbogo, nakushukuru sana kwa ushauri wako, tutaendelea kufuatilia na hii tafsiri ya uwekezaji na wageni kutokumiliki ardhi, tutakutana huko nje nitakwambia.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wanaruhusiwa kumiliki ardhi nchi hii kwa uwekezaji. Hiyo inaruhusiwa. Kwa hiyo, hakuna chochote tofauti. Mheshimiwa Qambalo tutaelewana, tutafuatilia hayo maagizo yangu kama hayajatekelezwa. Mheshimiwa Maryam Msabaha tunakushukuru sana kwa hotuba yako. Mheshimiwa Kalanga Laizer tunakushukuru sana kwa shukrani zako ulizozitoa leo, tunashukuru sana na tutaendelea kufanya kazi na tutamalizia yaliyobaki; na nitaendelea kufuatilia mipaka yako ambayo imebaki.

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Kilango kwamba tutarudi kuhakikisha kwamba tunamaliza. Najua yeye ni mwanasiasa, Jimbo lile wanamhitaji na alianza kuwasemea siku nyingi. Kwa hiyo, nitahakikisha haya yetu tunayafanya yabaki ya wao kama wanataka kutoa shukrani au hapana. Maana yake umewapigania sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lwakatare nimeshakupongeza, nashukuru sana kwa uungwana wako wa kazi uliyofanya, ulikuwa umetoka nje. Nashukuru sana kwa kazi kubwa uliyoifanya na michango yote tunaiheshimu na tutaitilia maanani.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba kukushukuru sana wewe kwa kunivumilia kipindi changu chote cha miaka mitano humu Bungeni, umenipa heshima kubwa sana ya kufanya kazi hizi. Najua wewe ungeweza kunitilia fitina, hata hizi pongezi nisingepata, maana una uwezo. Kiti hicho ukiamua unaweza kufanya lolote, lakini najua kwa namna yako ulivyo, wewe sio mtu wa fitina. Ukisema, ni jambo ambalo kweli lipo; na wanaomwelewa Spika, ndiyo mambo yao yanawanyookea humu ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuheshimu sana, nakupenda sana, nakuombea kila la heri. Tumefanya kazi miaka mingi, nami nimekuwa hapa Dodoma miaka mingi, nakujua sana. Ni mzee wa msimamo sana. Unaweza kuwa unasema sema, wanakuonaga kama unachekacheka lakini

ukishasema ndiyo imeshatoka hiyo. Kwa hiyo, nakushukuru sana kwa usimamizi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunivumilia kwa miaka mitano kukaa katika Wizara hii ambayo naye anaijua sana kwa sababu alikaa hapa. Kwa hiyo, namshukuru sana kwa kunivumilia naamini nimejitahidi. Nataka kumhakikishia kwamba yote aliyotuagiza tutayatimiza na tutayatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wasaidizi wangu kuanzia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa ushirikiano wao tuliopeana. Naomba sana Ofisi za Mikoa mzitumie vizuri tuliowapa Ofisi hizo, kweli zitatue kero za wananchi. Hatutaki kusikia kero ya mipaka ya vijiji, mipaka ya Wilaya, kero ya viwanja, kero za mashamba na Ofisi za Wizara zipo Mkoani. Hatutaki kusikia. Tunataka muwe na majibu. Hakuna jambo lolote ambalo mtashindwa kufanya katika Ofisi zetu za Mikoa. Tunapanga upya na Wilaya, ninyi mtawasimamia ili kuhakikisha kazi zote zinaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Lukuvi kwa kuhitimisha hoja yako vizuri kabisa, kwa umakini mkubwa.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeshawekwa mezani na imehitimishwa, ombi mbele yenu ni kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na

Maendeleo ya Makazi ya mwaka wa fedha 2020/2021 na kura zimeshapigwa, naziona hapa kwa wingi kabisa, kwamba waliosema ndiyo wameshinda. *(Makofi)*

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mwaka wa Fedha 2020/2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na
Maendeleo ya Makazi…….…....Sh. 46,978,640,000

Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya
Matumizi ya Ardhi……….….……...Sh. 2,489,290,000

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na
Maendeleo ya Makazi……..…..Sh.82,600,839,000

Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya
Matumizi ya Ardhi……....................…..Sh.1,500,000,000

**SPIKA:** Nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge kwa mara nyingine, tukushukuru sana Mheshimiwa Waziri Lukuvi sana, sana, sana, sana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Mabula, Katibu Mkuu, Makamishna na kadhalika, kwanza kwa kufanya kazi kubwa sana ya kubadili baadhi ya mifumo ambayo imekuwepo kwa muda mrefu ambayo imesababisha sekta hii imekuwa ni sehemu kubwa sana ya malalamiko kwa watu wengi na hasa watu wengi wanyonge. Watu walikuwa wakidhulumiwa viwanja, mashamba, matatizo moja kwa moja, lakini kwa kweli kazi mmeifanya. Hii inatupa moyo Watanzania kwamba, kumbe tunaweza. Pale tunapoamua, tunaweza. *(Makofi)*

Pia tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, ambaye kama ulivyoeleza aliwahi kukaa katika Wizara hii miaka ya nyuma.

Kwa maelekezo yake, kwa sababu bila *support* yake kubwa kwenu ingekuwa vigumu sana kufanya baadhi ya mambo. Tumeona mkifanya maamuzi bila kupepesa macho, bila wasiwasi wowote. Tena maamuzi mengine mazito, magumu lakini mmeyafanya na tumeweza kufika hapa tulipofika. Tunawatakia kila la heri, mwendelee kufanya kazi vizuri zaidi katika bajeti hii ambayo tumewapitishia.

Ninayo maneno mawili, matatu machache tu niseme. Kwanza mambo ya mitandao, ngoja kwanza tuone tunavyokucha; tunavuka daraja tunapolifikia. Niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge mnaapishwa na Spika na karibu wote nimewaapisha mimi mwenyewe hapa. Sasa Wabunge wangu niliowaapisha yaani wala msiwe na wasiwasi, hakuna cha nini wala nini, vikao vya majungu hivyo, yaani havifanyi kazi. *(Makofi)*

Eti mtu mmoja katika nchi hii anajifanya yeye ana mamlaka ya kufukuza Wabunge anavyotaka. Hivi nani jina lake huyo? Hii haiwezekani bwana! Haiwezekani hiyo biashara. Itaishia huko huko, lakini siyo Tanzania. Tanzania hii huwezi kujenga ufalme wa namna hiyo, unafanya unavyotaka. Wabunge kushoto geuka sawa, kulia geuka sawa; haya inama, nyanyuka, yaani haiwezekani!

Mbunge ukipata mshahara, lete sehemu fulani ya mshahara, lete huku; yaani wananchi mnachagua Mbunge anaenda kuwa mtumwa wa mtu kweli! Hata akihudhuria Kikao cha Bunge, kwa sababu yeye hataki, basi adhabu yake ni kufukuzwa! Hilo jambo halipo duniani wala haliwezi kuwepo Tanzania jambo la namna hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, endeleeni kuhudhuria wale mnaohudhuria, msiwe na mashaka, tutawalinda kwa sababu hakuna jambo lolote ambalo mnalifanya kinyume na sheria. Halipo. Halipo kabisa! Msajili hebu angalia vyama vya namna hii. Tazama vyama vya namna hii. Ndiyo dalili hizi. Sijui kwa sababu anaona yeye mwenyewe Novemba harudi hapa! Sasa anawaharibia wenzake. mambo magumu haya, lakini siyo magumu kivivyo. *(Makofi)*

Pia nikemee tabia za baadhi ya Waheshimwa Wabunge na baadhi ya watu kuwataja baadhi ya Marehemu wetu walioondoka hivi karibuni miongoni mwetu, kwa kusema wamekufa kwa sababu ya ugonjwa huu au ule au ule; tabia hii ni tabia ya ovyo sana. Watanzania hatupo hivyo. Hilo ni jambo linaachiwa familia. Mnaumiza familia za watu kwa sababu ya *political mileage,* ujinga! Tumefika huko kweli! Fulani kafa hivi, fulani; tabia gani hizo? Hamwezi kuheshimu hata Marehemu! Hata wenzenu mliokuwa nao humu Bungeni? *(Makofi)*

Yaani mtu akishakuwa Mpinzani wa Chama fulani anafikiri yeye ana tiketi ya kuropoka tu; hata misingi, mila, desturi, utamaduni hakuna. Vitu vya ajabu sana! Tuwaachie watoto wa Marehemu wabaki kwa amani, wana mengi ya masikitiko kutokana na ndugu zao, wazazi wao kuweza kuondoka hapa duniani, ni mpango wa Mungu, tunamshukuru Mwenyenzi Mungu. Tusivuke ambapo hatutakiwi kwenda na kushangilia sana, mtu akifariki wao ni sherehe kwenye mitandao huko. *(Makofi)*

Niendelee kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmeendelea kuhudhuria Bunge hili la Bajeti; na nawatia moyo mwendelee; na kesho tutatoa orodha, maana yake kesho tunapiga mstari kwa wale ambao hawajatii maelekezo ya Kiti hadi sasa na kwamba maelekezo yale bado yapo pale pale kurudisha zile fedha kwa wale ambao hawajatii. Watakapokuja lazima kila mmoja awe na *clearance certificate* ya kwamba amepima *Covid – 19* na ameonekana ni *negative*. Vinginevyo, kesho tutatoa orodha, vinginevyo hutapokelewa. Haitakubalika kabisa!

Mwisho kabisa, tunaendelea na progamu zetu vizuri. Kesho tuna Wizara ya Kilimo na kesho kutwa itafuata Wizara ya Mambo ya Nje na siku inayoufata Mifugo na Uvuvi na Ijumaa wiki hii Mwenyezi Mungu akijaalia basi tutakuwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa maana ya kwamba Ijumaa wiki hii tunakamilisha *set* ya Wizara karibu zote ili sasa tuweze kuingia awamu ya pili ya mambo mengine yatokanayo na ratiba yetu.

Basi baada ya shughuli za leo kukamilika, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi Kesho Saa 8.00 mchana.

*(Saa 12.05 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 12 Mei, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)*